# KISWAHILI

## MICHEPUO MINGINE

## KITABU CHA MWANAFUNZI

## KIDATO CHA 4

**© 2022 Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi**

Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi . Haki zote zimehifadhiwa. Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi wakati yaliyomo yamenukuliwa.

# DIBAJI

**Mwanafunzi Mpendwa,**

Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi inayo heshima kwa kutoa kitabu hiki cha mwanafunzi cha Somo la Kiswahili, Michepuo mingine, kidato cha nne. Kitabu hiki ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo.

Falsafa ya elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo katika kila ngazi ya elimu ili kumudu vizuri katika jamii na kumpa fursa ya kujipatia ajira.

Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza umuhimu wa kufungamanisha ujifunzaji na ufundishaji na zana pamoja na mitaala ili kuwezesha mchakato wa ujifunzaji. Mambo mengi yanaathiri yale ambayo wanafunzi wanafundishwa, namna nzuri ya kujifunza na uwezo waupatao. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahsusi wa yaliyomo, ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo.

Tumezingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza ambao unakuwezesha kuendeleza mawazo yako na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti yawe ya binafsi au katika makundi, kwa msaada wa walimu ambao majukumu yao ni kufanikisha ufundishaji. Utapata stadi zinazofaa kukuwezesha kutumia yale uliyojifunza katika miktadha ya maisha halisi. Kwa kufanya hivyo, utaonyesha tofauti siyo tu katika maisha yako bali hata kwa taifa.

Hii inatofautiana na mfumo wa zamani kuhusu nadharia ya ujifunzaji, iliyosisitiza mchakato wa kujifunza kama upataji wa maarifa kutoka kwa yule aliyemzidi maarifa na hasa akiwa ni mwalimu.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi ambapo dhana aghalabu huanzishwa kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na upatikanaji chanya wa maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya kujifunza hujishughulisha na wanafunzi kwa kufanya mambo na kufikiri kuhusu yale wanayoyafanya na wanafarijika kuonyesha uzoefu wao halisi na maarifa katika mchakato wa ujifunzaji.

Katika ufahamu huu, ufanisi mzuri kwa kutumia kitabu hiki, jukumu lako litakuwa:

- Kuendeleza maarifa na stadi kwa kufanya kazi, mazoezi yanayolenga kwenye mada. Kuwasiliana na kupeana taarifa sahihi pamoja na wanafunzi wengine kwa kupitia wasilisho, mijadala, kazi katika makundi na mbinu nyingine za ufundishaji kama: michezo ya kuigiza, utafiti, uchunguzi na utafiti katika maktaba, katika mitandao na nje ya shule.
- Kushiriki na kuwajibika kuhusu ujifunzaji wako na Kufanya utafiti, uchunguzi kwenye maandishi yaliyochapishwa / mtandaoni, wataalam na kuwasilisha matokeo ya utafiti.
- Kuhakikisha ufanisi mzuri wa mchango wa kila mwanakundi katika kazi sahihi uliyopewa kupitia maelezo na majadiliano unapoongea hadharani.
- Kutoa hitimisho sahihi kuhusu matokeo ya utafiti uliotokana na mazoezi ya ujifunzaji.

Napenda kutoa shukrani kwa wale wote walioshiriki kutoa mchango wa kuboresha kitabu hiki, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi (CTLR-REB) walioandaa mchakato wa kazi hii tokea ilipoanza.

Pongezi muhimu ziwaendee walimu wa chuo Kikuu cha Rwanda kwa msaada wao wa kutoa wataalamu ambao ni wahadhiri, walimu na wachoraji waliosaidia kusimamia, kuendeleza na kufanikisha uboreshaji wa kazi hii kuhusu picha na michoro sahihi. Maoni au mawazo yoyote yanakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo yatakayofuata.

**Dkt. MBARUSHIMANA Nelson**

**Mkurugenzi Mkuu, REB**

## SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki. Kitabu hiki kisingeliwezekana kufanikiwa bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki, jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati.

Shukrani zangu ziendee vyuo vikuu na shule mbalimbali kwa kuwaruhusu wafanyakazi wao kufanya kazi na Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi katika mradi wa uandikaji wa kitabu hiki. Napenda kutoa shukrani zaidi kwa wahadhiri na walimu ambao juhudi zao na uandikikaji wa kitabu hiki ulikuwa wa thamani.

Mwishowe, neno la mwisho la shukrani liwaendee wafanyakazi wote wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi (CTLR-REB) walioshiriki katika mchakato wa kufanikisha uandikaji wa kitabu hiki.

**Joan Murungi**

**Mkuu wa idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana ( CTLR)**

## YALIYOMO

DIBAJI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .iii

SHUKRANI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .v

UTANGULIZI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . xi

MADA KUU YA 1: MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAZINGIRA MBALIMBALI . . .2

MADA NDOGO: Msamiati katika Mazingira ya Hospitali. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .2

SOMO LA 1: Mazungumzo Hospitalini . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .3

1.1. Kusoma na Ufahamu: Mazungumzo Hospitalini . . . . . . . . . . . . . . . . . . .3

1.2. Msamiati Kuhusu Mazingira ya Hospitali . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .7

1.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi -nge- . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .8

1.4. Matumizi ya lugha: Vifaa vya Hospitalini. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .10

1.5. Kusikiliza na kuzungumza. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .11

1.6. Kuandika . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .11

SOMO LA 2: USAFI WA MAZINGIRA YA HOSPITALI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .11

2.1. Kusoma na Ufahamu: Umuhimu wa Usafi wa Mazingira Hospitalini .12

2.2. Msamiati kuhusu Usafi Hospitalini . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .14

2.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi -ngeli- . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .15

2.4. Matumizi ya Lugha . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .18

2.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano na Mawasilisho . . . . . . . . . .19

2.6. Kuandika: Utungaji wa Kifungu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .19

SOMO LA 3: ADABU HOSPITALINI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .19

3.1. Kusoma na Ufahamu: Maelekezo na Kanuni Hospitalini . . . . . . . . . .19

3.2. Msamiati kuhusu Adabu Hospitalini . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .22

3.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi chenye Dhana ya Masharti -ngali- . . .23

3.4. Matumizi ya Lugha: Msamiati wa Adabu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .25

3.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .25

3.6. Kuandika: Sifa za Aya katika Uandishi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .25

MADA KUU YA 2: MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAZINGIRA MBALIMBALI . . . 28
MADA NDOGO: Msamiati katika michezo . . . 28
SOMO LA 4: MICHEZO SHULENI . . . 29
4.1. Kusoma na Ufahamu: Timu Hodari . . . 29
4.2. Msamiati kuhusu Michezo Shuleni . . . 32
4.3. Sarufi: Matumizi ya majina ya ngeli ya LI-YA . . . 33
4.4. Matumizi ya Lugha: Upambanuzi wa Maneno . . . 34
4.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Zoezi la Kutangaza Mpira wa Miguu Redioni . . . 34
4.6. Kuandika: Utungaji . . . 35
SOMO LA 5: FAIDA ZA MICHEZO . . . 35
5.1. Kusoma na Ufahamu: Faida za Michezo . . . 36
5.2. Msamiati kuhusu Faida za Michezo . . . 38
5.3. Sarufi: Majina ya Ngeli ya Li-YA- Pamoja na Vivumishi vyake . . . 39
5.4. Matumizi ya Lugha: Utambuzi wa Maana za maneno . . . 41
5.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano . . . 42
5.6. Kuandika: Utungaji wa Kifungu cha Habari . . . 42
SOMO LA 6: MASHINDANO KATIKA MICHEZO . . . 43
6.1. Kusoma na Ufahamu: Mchezo wa Kandanda . . . 43
6.2. Msamiati kuhusu Mchezo wa Kandanda . . . 45
6.3. Sarufi: Matumizi ya Vivumishi vya Kuuliza, vya Idadi na vya Sifa . . . 46
6.4. Matumizi ya Lugha: Upangaji wa Maneno katika Sentensi na Miktadha ya Matumizi. . . . 48
6.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano . . . 48
6.6. Kuandika: Utungaji wa Kifungu kuhusu Matukio ya Mchezo . . . 48
MADA KUU YA 3: UHAKIKI WA HADITHI ZA MASIMULIZI KATIKA KISWAHILI . 52
MADA NDOGO: Muhtasari, fani na maudhui . . . 52
SOMO LA 7: MUHTASARI . . . 53
7.1. Kusoma na Ufahamu: Mhunzi Tulia . . . 53

7.2. Msamiati Kuhusu Kifungu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 56
7.3. Sarufi: Majina ya Ngeli ya Pa- na vivumishi vyake . . . . . . . . . . . . . . . 56
7.4. Matumizi ya Lugha: Sifa za Muhtasari . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 59
7.5. Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 61
7.6. Kuandika: Uandishi wa Muhtasari. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 61
SOMO LA 8: FANI KATIKA HADITHI SIMULIZI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 61
8.1. Kusoma na Ufahamu: Kobe na Nyani. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 61
8.2. Msamiati kuhusu kifungu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 65
8.3. Sarufi: Matumizi ya Majina ya Ngeli ya M- na Vivumishi Ambatana. . 66
8.4. Matumizi ya Lugha: Fasihi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 68
8.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 71
8.6. Kuandika: Utungaji wa Hadithi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 71
SOMO LA 9: MAUDHUI KATIKA HADITHI SIMULIZI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 71
9.1. Kusoma na Ufahamu: Wafalme Wawili. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 71
9.2. Msamiati kuhusu Wafalme Wawili. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 74
9.3. Sarufi: Matumizi ya Majina ya Ngeli ya Ku- na Viumishi Ambatana.. . 75
9.4. Matumizi ya Lugha: Maudhui katika Fasihi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 77
9.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 78
9.6. Kuandika: Utungaji wa Hadithi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 78
MADAKUU YA 4: UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO ..........82
MADA NDOGO: MIDAHALO NA MIJADALA . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 82
SOMO LA 10: MDAHALO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 83
10.1. Kusoma na Ufahamu: Mazungumzo Baina ya Wanafunzi . . . . . . . . 83
10.2. Msamiati kuhusu Maana ya Mdahalo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 86
10.3. Sarufi: Matumizi ya Hali ya Kushurutisha kwa Vitenzi . . . . . . . . . . . 87
10.4. Matumizi ya Lugha: Maana ya Mdahalo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 89
10.5. Kusikiliza na Kuzungumza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 91
10.6. Utungaji. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 91

SOMO LA 11: MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA MDAHALO . . . . . . . . . . . . . . 91

11.1. Mdahalo : Dawa za Kulevya Ndilo Tatizo Linaloathiri Maendeleo ya Vijana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 92

11.2. Msamiati kuhusu “Mdahalo” . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 99

11.3. Sarufi: Matumizi ya Vitenzi vya Silabi Moja. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 101

11.4. Matumizi ya lugha: Maandalizi na Utekelezaji wa Mdahalo . . . . . . 103

11.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Mdahalo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 106

11.6. Kundika: Uandishi wa Mdahalo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 106

SOMO LA 12: MJADALA. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 107

12.1. Kusoma na Ufahamu: Maana ya Mjadala . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 107

12.2. Msamiati kuhusu Maana ya Mjadala. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 109

12.3. Sarufi: Hali Shurutishi ya Vitenzi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 111

12.4. Matumizi ya Lugha: Maana ya Mjadala. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 113

12.5. Kusikiliza na Kuzungumza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 115

12.6. Utungaji . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 115

SOMO LA 13: MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA MJADALA . . . . . . . . . . . . . 116

13.1. Mjadala kuhusu: “Mchango wa Wazazi katika Malezi ya Watoto Wao”. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 116

13.2. Msamiati kuhusu “Andalio la Mjadala” . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 121

13.3. Sarufi: Matumizi ya Hali ya Vitenzi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 123

13.4. Matumizi ya lugha: Maandalizi na Utekelezaji wa Mjadala . . . . . . . 125

13.5. Kusikiliza na Kuzungumza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 127

13.6. Utungaji . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 128

MADA KUUYA5: UTUNGAJI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 130

MADA NDOGO: INSHA ZA MASIMULIZI AU ZA KUBUNI . . . . . . . . . . . . . . . . . . 130

SOMO LA 14: MAANA YA INSHA. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 130

14.1. Kusoma na Ufahamu: Tarakilishi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 131

14.2. Msamiati kuhusu Kifungu cha Habari . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 133

14.3. Sarufi: Usemi Halisi na Usemi wa Taarifa. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 134

14.4. Matumizi ya Lugha: Maana ya Insha na Sifa Zake . . . . . . . . . . . . . 136

14.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 137

14.6. Utungaji: Uandishi wa Insha . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 137

SOMO LA 15: AINA ZA INSHA . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 138

15.1. Kusoma na Ufahamu: Nchi Yetu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 138

15.2. Msamiati kuhusu Nchi Yetu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 140

15.3. Sarufi: Usemi wa Taarifa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 141

15.4. Matumizi ya Lugha: Aina za Insha . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 143

15.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 147

15.6. Utungaji: Uandishi wa Insha ya Wasifu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 147

SOMO LA 16: INSHA ZA MASIMULIZI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 148

16.1. Kusoma na Ufahamu: Siku Yangu ya Kwanza katika Shule ya Sekondari Kidato cha Nne . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 148

16.2. Msamiati Kuhusu Insha ya Masimulizi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 150

16.3. Sarufi: Usemi wa Asili na Usemi wa Taarifa. . . . . . . . . . . . . . . . . . . 152

16.4. Matumizi ya Lugha: Sehemu za Insha . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 156

16.5. Kusikiliza na Kuzungumza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 158

16.6. Utungaji . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 159

MAREJEO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 160

# UTANGULIZI

Kiswahili ni lugha ambayo imepewa kipaumbele zaidi kutokana na umuhimu wake wa kutumiwa kama lugha rasmi miongoni mwa lugha nyingine zinazotumiwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchini Rwanda, lugha ya Kiswahili hufundishwa katika shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha tatu katika ngazi ya chini ya sekondari. Zaidi ya hivyo, mbali na mchepuo wa lugha ambapo Kiswahili hufundishwa katika mchepuo wa Fasihi, Kinyarwanda na Kiswahili, lugha hii hufundishwa pia katika michepuo mingine. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili imepiga hatua kimatumizi katika jamii mbalimbali barani Afrika na hata ulimwenguni. Nchi kama vile Marekani, Ujerumani na nchi nyingi za Ulaya, hufundisha Kiswahili na kukitumia katika mazingira tofauti.

Kitabu hiki kimeandikwa kwa kuwalenga wanafunzi wa Shule za Sekondari nchini Rwanda wanaosoma katika kidato cha nne, michepuo isiyokuwa na somo la Kiswahili. Kila mada iliyojadiliwa katika kitabu hiki, imegawanywa katika mada ndogo ndogo ambapo kila mada ndogo huwa na masomo mbalimbali yenye kugusia vipengele vifuatavyo:

- Kusoma na ufahamu,
- Maswali ya ufahamu,
- Matumizi ya msamiati wa msingi,
- Sarufi,
- Matumizi ya lugha,
- Kusikiliza na kuzungumza,
- Kuandika.

Masomo yaliyopendekezwa katika kitabu hiki yamezingatia matakwa na mahitaji ya nchi ya Rwanda kwani Kiswahili kinahitajika kutumiwa katika mawasiliano mapana katika Jumuiya ya Afrika ya mashariki. Aidha, mwanafunzi anatakiwa kujifunza hatua kwa hatua masomo yote yaliyopendekezwa ili aweze kujijengea na kujifungulia milango ya kujiendeleza na kuliendeleza taifa lake kwa ujumla.

Uwezo utakaopatikana kupitia masomo hayo utamwezesha mwanafunzi kukabiliana na matatizo mbalimbali yanayojitokeza katika maisha yake ya kila siku: Kujilinda na magonjwa mbalimbali katika elimu ya afya ya uzazi, kutunza mazingira, elimu kuhusu uzalishaji mali au ujasiriamali, usawa wa jinsia na mafunzo kuhusu amani na maadili.

Ili kufanikisha ujifunzaji wake, ni vyema mwanafunzi ajitahidi kufanya mazoezi yaliyotolewa kwa kila somo. Vilevile, ni jambo muhimu kusoma kwa makini na

kufanya uchunguzi wa mada zilizojadiliwa katika kitabu hiki. Mazoezi mengi yaliyopendekezwa yatamwezesha mwanafunzi kukuza uwezo wake katika kiwango cha utafiti, ushirikiano na utawala binafsi na stadi za maisha na kuendeleza ujifunzaji wa kudumu. Vilevile, mazoezi ya mijadala ya kibinafsi na ya makundi yote yatasaidia kumjenga mwanafunzi kwa kumpa uwezo wa kuwasiliana na watu mbalimbali kwa kutumia Kiswahili fasaha. Mazoezi ya makundi yaliyopendekezwa yatamsaidia mwanafunzi kuelewa nafasi yake katika kujenga desturi ya heshima kwa wengine, uvumilivu, upendo na amani, haki, umoja na mshikamano na demokrasia.

Ili kufanikisha ujifunzaji wake, ni vyema mwanafunzi akumbuke kwamba kitabu hiki kinafuata vitabu vingine vya Kiswahili ambavyo viliandaliwa kwa wanafunzi wa ngazi ya chini ya Sekondari nchini Rwanda. Kwa hivyo, mwanafunzi awe na ujuzi wa awali wa kutosha ambao utamwezesha kuelewa mada zilizotolewa katika kitabu hiki kwa kuhakikisha kwamba amepata uwezo wa kutosha wa kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano na shughuli mbalimbali za maisha.

# MADA KUU YA 1

## MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAZINGIRA MBALIMBALI

# MADA KUU YA 1: MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAZINGIRA MBALIMBALI

## MADA NDOGO: Msamiati katika Mazingira ya Hospitali

**Uwezo upatikanao katika mada**: Kusikiliza kwa makini, kusoma vifungu vya habari na kutumia msamiati muhimu katika mazingira ya hospitali; kuzingatia matumizi ya viambishi -nge-, -ngeli- na -ngali-.

**Malengo ya Ujifunzaji:**

- Kutumia msamiati maalum wa mazingira ya hospitali katika mawasiliano;
- Kuelezea hospitali na mazingira yake kwa mtu yeyote anayehitaji habari kuhusu hospitali hiyo;
- Kulinganisha na kutofautisha hospitali moja na nyingine kwa kuzingatia mazingira na shughuli zinazofanyika hapo;
- Kuelezea uhusiano wa watu wapatikanao hospitalini;
- Kusikiliza kwa makini na kusoma kwa ufasaha kifungu cha habari kinachohusika;
- Kutunga sentensi fupi kwa kuzingatia hali ya masharti.

### Kazi Tangulizi

1. Hospitali ni nini?
2. Taja vifaa vitano vitumiwavyo hospitalini, kisha eleza umuhimu wake.
3. Ainisha kazi na majukumu ya wafanyakazi wapatikanao hospitalini.
4. Ainisha kazi na majukumu ya wafanyakazi wapatikanao hospitalini.
5. Andika aya moja kwa kuelezea umuhimu wa usafi hospitalini.
6. Baadhi ya wagonjwa huonyesha mienendo isiyofaa hospitalini. Jadili.

## SOMO LA 1: MAZUNGUMZO HOSPITALINI

**Tazameni mchoro ufuatao. Jadilini mnayoyaona kwenye mchoro husika.**



**ZOEZI LA 1:**

***Taja angalau vitu vitatu (watu, vifaa, majengo) ambavyo hupatikana katika mazingira ya hospitali au zahanati.***

### 1.1. Kusoma na Ufahamu: Mazungumzo Hospitalini

Wanafunzi wa kidato cha nne kwenye Shule ya Sekondari ya Ntende wametembelea hospitali moja iliyoko mjini Kigali. Wameingia hospitalini na kukaribishwa na mpokezi wageni ambaye anamwita Daktari Mkuu pamoja na muuguzi wake ili wawaelezee mengi kuhusu vifaa na wafanyakazi wa hospitali yao.

**Daktari:** Hamjambo vijana!

**Wanafunzi:** Hatujambo Daktari!

**Daktari:** Asante sana kwa wazo lenu la kutembelea hospitali yetu kwa ajili ya kujua  kuhusu vifaa tofauti vinavyotumiwa, sehemu za hospitali pamoja na wafanyakazi wa hospitali. Kwa hiyo, karibuni nyote! Mimi ni Daktari Mkuu na huyu ni muuguzi wetu, anaitwa Veneranda. Kwa hakika, tunafurahia kuwaonyesha sehemu mbalimbali za hospitali yetu kama mnavyohitaji.

**Mwanafunzi wa kwanza**: Asante sana kwa kutukaribisha. Jina langu ni Bella na mimi ndimi kiranja wa darasa letu. Hawa ni wanafunzi wenzangu. Nasi pia tutanufaika zaidi kutokana na maelezo yenu kuhusu shughuli zinazofanywa

na vifaa vinavyotumiwa hospitalini.

**Daktari:** Asante sana! Sasa ni wakati wa kuwaelezea juu ya sehemu tofauti za hospitali.

**Mwanafunzi wa pili:** Tafadhali Daktari! Kabla ya hayo, ningetaka kujua jina la sehemu hii ambapo tumekaribishiwa na kupata kiti.

**Daktari:** Sehemu hii inaitwa pambajio. Ni sehemu ya kuwapokelea wagonjwa.

**Mwanafunzi wa tatu:** Samahani Daktari! Sisi hatuko wagonjwa, najiuliza ikiwa hamtatudunga sindano! Labda kwa bahati mbaya, mnaweza!

**Daktari:** Usiwe na wasiwasi kijana! Nyie ni wageni siyo wagonjwa. Acheni tuendelee. Sehemu ya pili ni chumba cha matibabu ya dharura, yaani chumba cha kuwatibia wagonjwa wanaohitaji matibabu ya haraka sana kama vile majeruhi wa ajali. Lakini, ni vyema mwelewe kwamba chumba hiki ni tofauti na wodi ya matibabu maalum kwani wodi ya matibabu maalumu ni chumba cha kushughulikia maradhi ambayo si ya kawaida kama vile maradhi ambayo yamezuka ghafla na bado hayaeleweki vizuri.

**Muuguzi:** Kuna wodi nyingine ambayo ni sehemu ya kuwalaza wagonjwa wanaoendelea na matibabu.

**Mwanafunzi wa kwanza:** Samahani Daktari! Nimesoma kwenye mlango ule neno maabara. Kwa hiyo, ningetaka kujua maana ya neno hilo.

**Daktari:** Asante sana! Bado ninaendelea kuwaelezea, ebu tegeni sikio! Maabara ni chumba cha kufanyia uchunguzi wa magonjwa, lakini kuna sehemu nyingine muhimu za hospitali kama vile chumba cha dawa, kungawi ambacho ni chumba cha kujifungulia kwa kina mama wajawazito, chumba cha upasuaji, chumba cha uangalizi maalumu, ambacho ni chumba cha matibabu ya kiwango cha juu sana. Hususan chumba hiki hutumiwa kwa wagonjwa walio katika hali mahututi.

**Muuguzi:** Chumba hiki huwa na mitambo na mashine za hali ya juu sana za kumsaidia mgonjwa. Chumba cha mwisho ni ufuoni au makafani ambacho ni chumba kinachotumiwa kuhifadhia maiti.

**Mwanafunzi wa nne:** Asante sana Daktari kwa maelezo haya. Ningependa sasa utuelezee kuhusu wafanyakazi wa hospitali na vifaa muhimu wanavyotumia.

**Daktari:** Kabla hatujatembelea vyumba vyote vyenye kuhifadhi vifaa mbalimbali tunavyotumia, chunguzeni kwenye picha hizi za vifaa vipatikanavyo hospitalini. Hapa kuna eksrei au uyoka ambayo ni mashine ya kutazamia viungo vya ndani ya mwili. Machela ni kifaa kingine. Kifaa hiki ni kigari au kitanda cha kubebea wagonjwa. Maikroskopu au hadubini hutumiwa kuangalia vijidudu vidogo sana ambavyo haviwezi kuonekana kwa macho tu.

Dipfriza hii mnayoiona ni chombo cha kuhifadhia baadhi ya dawa zinazohitaji kuhifadhiwa katika baridi kali sana. Jiko lile hutumiwa kuchemshia vyombo ili kuulia vijidudu  na bakteria. Hapa mnaona glovu ambayo ni kifaa chenye umbo kama la soksi. Kifaa hiki hutengenezwa kwa mpira na huwekwa mkononi kumkinga muuguzi anayekitumia dhidi ya uchafu. Kwenye mchoro huu mnaona sindano; yaani kifaa cha kupenyezea dawa mwilini. Makasi haya mnayoyaona hapa hutumiwa kwa kukatia. Bendeji hii mnayoiona hapa ni kitambaa cha kufungia jeraha au kidonda ili kisiweze kuchafuliwa. Plasta ni kitambaa kigumu sana cha kufungia sehemu ya mwili iliyovunjika. Koleo hii hapa hutumika kama kifaa cha kushikia vitu vinavyotumiwa na daktari.

**Muuguzi:** Ninaona daktari amewafafanulia vizuri kuhusu vifaa mbalimbali tunavyotumia hospitalini. Ningependa tutembelee sehemu ambapo tutawakuta wafanyakazi mbalimbali ili niwaelezee kazi zao. Kuhusiana na wafanyakazi wanaopatikana hospitalini wengi mnawafahamu. Daktari au tabibu mnayemuona hapa ndiye anawatibu wagonjwa. Huyu mnayemuona hapa upande wa kushoto ni Muuguzi au nesi anayemsaidia daktari katika kazi yake. Na bibi huyu ni Mkunga ambaye anawasaidia wajawazito kujifungua. Huyu anayesimama pembeni mwa Daktari ni Mhazigi ambaye hushughulikia waliovunjika viungo kama vile miguu au mikono. Na huyu ni Msaidizi katika maabara na ndiye huwahudumia wagonjwa.  Mfanyakazi yule anayekaa sehemu ile ni Karani ambaye anaweka rekodi za wagonjwa. Yule anayefuata ni mfamasia anayeweka na kuzitoa dawa kwa wagonjwa. Bwana huyu ni daktari wa meno ambaye anashughulikia wagonjwa walio na matatizo ya meno.

**Mwanafunzi wa tatu:** Kwa upande wangu ninanufaika zaidi kutokana na safari hii. Kwa kweli, tungetembelea hospitali hii mwaka jana, tungejua haya yote tayari. Kwa kweli, “asiyefika kwa mfalme hudanganywa mengi.” Tumebahatika kufika hapa na mengi tumeyaelewa.

**Mwanafunzi wa kwanza:** Sisi sote tunafurahi sana kutokana na maelezo tuliyopewa. Kama mnavyotuona tutafanya iwezekanavyo ili tufike kwenye kiwango hiki. Kwani tungekuwa kama nyinyi, tungewasaidia wagonjwa wa aina tofauti kama mnavyofanya.

**Daktari:** Asanteni sana vijana. Tuna imani kwamba mmenufaika sana kwa ziara yenu. Kwa heri ya kuonana. Twawatakieni kila la kheri. Mungu awabariki.

**Mwanafunzi wa Kwanza:** Asante sana Daktari, nasi twawatakia kazi njema.

## MASWALI YA UFAHAMU

***Jubu maswali yafuatayo:***

1. Ni watu gani wanaozungumza katika kifungu hiki?
2. Wanafunzi walikuwa na lengo gani kwa kuitembelea hospitali inayozungumziwa?
3. Wanafunzi hao walikuwa katika kiwango gani cha elimu?
4. Msimamizi wa wanafunzi hao ni nani?
5. Unadhani wanafunzi hawa wamepokelewa vizuri? Eleza.
6. “Asiyefika kwa mfalme hudanganywa mengi.” Jadili.
7. Baada ya kupata maelezo tofauti kuhusu hospitali, wanafunzi walimwahidi nini daktari?
8. Kulingana na namna mazungumzo yalivyoendelea, onyesha kwamba wanafunzi wameelewa mambo yanayotendeka hospitalini.

## ZOEZI LA 2:

***Jibu maswali haya kwa kuchagua jibu lililo sahihi.***

**1. Kifungu hiki cha habari kinazungumzia:**

a. Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Ntende
b. Daktari
c. Ziara ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Ntende kwenye hospitali.
d. Shule ya Sekondari ya Ntende.

**2. Dipfriza ni mojawapo wa:**

a. Wafanyakazi wa hospitalini
b. Dawa za hospitalini
c. Sehemu za hospitali
d. Vifaa vya hospitalini.

**3. Kungawi ni chumba cha:**

a. Kuwapasulia wajawazito
b. Kuzalia wajawazito
c. Kununulia dawa
d. Kulalia wagonjwa.

**4. Machela inatumiwa kwa kubeba:**

1. Dawa za wagonjwa
2. Walemavu
3. Vifaa vya hospitalini
4. Wagonjwa hospitalini.

**5. Daktari au Muuguzi anatumia bendeji kwa:**

1. Kumfunga kamba mgonjwa
2. Kufungia kidonda
3. Kufungia sehemu iliyovunjika
4. Kumwezesha mgonjwa kutembeatembea.

## 1.2. Msamiati Kuhusu Mazingira ya Hospitali

### ZOEZI LA 3:

***Baada ya kusoma kifungu hiki cha habari, toa maana ya msamiati unaofuata, kisha utunge sentensi zenye maana kamili kwa kutumia msamiati huo.***

1. Kudunga
2. Matibabu
3. Mgonjwa
4. Hali mahututi
5. Kupenyeza
6. Kuhifadhi
7. Uchafu
8. Mjamzito
9. Kujifungua
10. Dharura

### ZOEZI LA 4:

**Oanisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Dobi | a. anayewatibu wagonjwa. |
| 2. Tabibu | b. anayewasaidia wajawazito kujifungua |
| 3. Mkunga | c. anayeshughulikia waliovunjika viungo. |
| 4. Karani | d. anayepokea pesa kutoka huduma mbalimbali. |
| 5. Mhazigi | e. anayeshughulikia vipimo vya afya. |
| 6. Mfamasia | f. anayeweka rekodi za wagonjwa. |
| 7. Maabara fundi | g. anayeweka dawa na kuzitoa kwa wagonjwa. |
| 8. Muuguzi au nesi | h. afuaye nguo na kuzipiga pasi. |
| 9.Afisa wa usalama | i. anayemsaidia mganga kuwatibu wagonjwa. |
| 10. Keshia | j. achunguzaye mwendo wa wanaoingia na kutoka. |

### ZOEZI LA 5:

***Kamilisha sentensi zifuatazo ili zilete maana kamili kwa kutumia maneno haya kama yalivyotumiwa katika mazungumzo: eksirei, plasta, chumba cha matibabu ya dharura, sindano, kuhifadhia baadhi ya dawa.***

1. .........................ni chumba cha kuwatibia wale wanaohitaji matibabu ya haraka sana kama vile majeruhi wa ajali.
2. Kitambaa kigumu sana cha kufungia sehemu iliyovunjika ni..............
3. Dipfriza ni....................................
4. ............................ni kifaa cha kupenyezea dawa mwilini.
5. ............................ ni mashine ya kuonea viungo vya ndani ya mwili.

## 1.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi -nge-

### ZOEZI LA 6:

***Soma sentensi zifuatazo kisha ueleze jinsi vitendo vilivyopo hutegemeana kimoja kwa kingine. Chunguza matumizi ya kiambishi -nge- katika maelezo muhimu hapo chini.***

1. Tungetembelea hospitali hii mwaka jana, tungejua haya yote tayari.
2. M**nge**enda kuyatembelea mashirika mengine, m**nge**elewa zaidi kuhusu vifaa tofauti na majina maalumu ya wafanyakazi.
3. Sisi tu**nge**kuwa kama nyinyi, tu**nge**wasaidia wagonjwa wa aina tofauti kama mnavyofanya.

### ZOEZI LA 7:

***Tunga sentensi zako tano kwa kutumia kiambishi -nge-.***

**Maelezo muhimu kuhusu matumizi ya kiambishi -nge-**

Kiambishi **-nge-** ni kiambishi ambacho hutuarifu juu ya hali ya masharti. Hutuarifu juu ya sharti kwamba tendo moja ni lazima lifanyike ndipo tendo jingine nalo lifanyike. Huonyesha kuwa tendo fulani halijafanyika na kwa hiyo, jambo jingine halijatokea lakini kuwa kuna uwezekano wa kufanyika kwa tendo hilo na kisha jambo hilo litokee.
Matumizi ya kiambishi –nge-:

**Katika hali ya kuonyesha uwezekano**

**MIFANO:**

- Ningekuwa na pesa, ningemjengea mzazi nyumba nzuri. Maana yake ni kuwa mimi sina pesa wala sikujengea mzazi nyumba nzuri, lakini nikipata pesa sasa hivi ninaweza kumjengea nyumba nzuri.
- Ningemjua msichana yule, ningemshauri kuacha tabia mbaya. Maana yake ni kwamba *simjui msichana yule, lakini kumjua kwangu kwasabisha kumpa ushauri wa kuacha tabia yake mbaya.*

**Katika hali ya kuonyesha majuto**

**MIFANO:**

- Ningekuwa msichana mwenye moyo wa utulivu, ningejilinda kujiunga na vijana wenye tabia mbaya za uasherati.

Maana yake ni kuwa mimi sikuwa msichana mwenye moyo wa utulivu ijapokuwa ningehitaji kuwa msichana mwenye moyo wa utulivu ili nijiepushe na urafiki na vijana wenye tabia mbaya za uasherati, lakini ninajuta kwa sababu sikuweza kuwa na moyo wa utulivu.

- Ningekuwa mkristo wa kweli, ningeacha kuvuta sigara au kuchukua dawa za kulevya ambazo zimeniharibia afya.

Maana yake ni kuwa mimi si mkristo wa kweli na ninajuta kuwa uvutaji wa sigara na kuchukua dawa za kulevya kumeniharibia afya.

**Kiambishi -nge- kinaweza kutumiwa katika hali kanushi na vilevile katika hali yakinishi.**

| Hali yakinishi/Tungo yakinishi | Hali kanushi/Tungo kanushi |
|---|---|
| 1. Ningekuwa na koti safi sana, ningekwenda harusini. | Nisingekuwa na koti safi sana, nisingekwenda harusini. |
| 2. Kama ningekuwa na pesa sasa, ningenunua shati hili. | Kama nisingekuwa na pesa sasa, nisingenunua shati hili. |
| 3. Ningejua kuwa mvua itanyesha, ningenunua mwavuli jana. | Nisingejua kuwa mvua itanyesha, nisingenunua mwavuli jana. |
| 4. Kama wangewahi kuondoka siku ile, mvua ingewanyeshea | Kama wasingewahi kuondoka siku ile, mvua isingewanyeshea. |
| 5. Wanafunzi hawa wangechelewa asubuhi hii, wangekosa mtihani wa Kiswahili. | Wanafunzi hawa wasingechelewa asubuhi hii, wasingekosa mtihani wa Kiswahili. |

**Tanbihi**: Katika matumizi ya kiambishi hiki, tunaweza kukanusha kwa kutumia kikanushi -**si**- kama inavyoonyeshwa kwenye mifano hapo juu.

### ZOEZI LA 8:

***Kamilisha sentensi hapo chini ili zilete maana kamili***

**MFANO:**


Wagonjwa wangepata dawa, wangepona haraka haraka.

1. Tu**nge**panda miti kwenye milima, ......................................................
2. Wa**nge**jua nia yangu katika kutetea haki za wanawake, ........................
3. U**nge**onana na daktari, u....................................................................
4. Barabara zote zi**nge**kuwa za lami, kila eneo nchini Rwanda ................
5. Wanafunzi wa**nge**elewa somo vizuri, ................................................
6. Wazazi wa**nge**sikia shauri kutoka walimu wa watoto wao, .....................
7. Wa**nge**jua kuwa usafi hospitalini ni kitu muhimu sana, ..........................
8. ......................................................, wa**nge**tumia chandarua kila usiku.
9. Wa**nge**chezea kiwanjani mwao, ..........................................................
10. ....................... ......, wangemjulisha habari za harusi za dada Mugeni.

## 1.4. Matumizi ya lugha: Vifaa vya Hospitalini

### ZOEZI LA 9:

***Husisha majina haya na vifaa vinavyopatikana hapo chini: machela, sindano, kipimajoto, mizani, bendeji, vidonge.***



**ZOEZI LA 10:**

*Taja zahanati moja uliyoitembelea, kisha ueleze jinsi ulivyoiona na wafanyakazi waliokuwepo.*

### 1.5. Kusikiliza na kuzungumza

**ZOEZI LA 11:**

*Igizeni mazungumzo mliyoyasoma kati ya Daktari, Muuguzi na Wanafunzi.*


## 1.6. Kuandika

**ZOEZI LA 12:**

*Tunga mazungumzo kati ya muuguzi na wagonjwa wawili.*

## SOMO LA 2: USAFI WA MAZINGIRA YA HOSPITALI

***Tazama mchoro huu kwa makini, kisha ujishughulishe na mazoezi yanayofuata.***



**ZOEZI LA 1:**

*Chunguza mchoro huu, kisha ueleze unayoyaona yanayohusiana na usafi.*

### 2.1. Kusoma na Ufahamu: Umuhimu wa Usafi wa Mazingira Hospitalini

Soma kifungu cha habari kuhusu "Umuhimu wa Usafi wa Mazingira Hospitalini" ili ujibu maswali uliyopewa.

Usafi wa mazingira ni jambo ambalo linafaa kutiliwa maanani na kila mtu kwani uchafu unachangia pakubwa kuharibu maisha ya binadamu yeyote yule. Jambo la kusikitisha ni kwamba watu wengi hujitahidi kuwa safi kwenye miili na mavazi yao tu huku wakisahau kuwa usafi huhusu kila kitu kinachopatikana katika mazingira wanamoishi. Watu wengi wangeliepuka na kupatwa na magonjwa mbalimbali yanayotokana na uchafu kama wangelizingatia usafi wa mazingira yao.

Tunapozungumzia usafi hospitalini, watu wengi huelewa shughuli muhimu zinazostahili kufanywa katika kusafisha vyumba vya wagonjwa na kutengeneza bustani zinazozunguka hospitali hiyo.

Lakini, ni lazima kujua kwamba usafi hospitalini huchunguzwa kupitia vifaa vinavyotumiwa, dawa zinazotunzwa na kupewa wagonjwa, mahali pa kutolea huduma tofauti, usafi wa wagonjwa na hata watumishi wote wanaoshughulikia na kuhudumia wagonjwa hao na watu wengine wanaofika kwenye hospitali hiyo.

Mazingira ya hospitali huweza kusafishwa kwa kutumia dawa za kuulia wadudu wenye kuambukiza watu magonjwa mbalimbali. Ufikapo katika hospitali yoyote hutakosa kuwakuta watumishi wanaopiga deki na kusafisha mazingira mengine ya hospitali hiyo. Watu hawa nao huvaa bwelasuti ili waweze kujikinga uchafu na huhakikisha kuwa vyoo vinavyotumiwa ni safi kwa kuwaonya wagonjwa wasitupe uchafu ovyoovyo. Kama vyoo havisafishwi vizuri, nzi huweza kujitafutia makazi yao humo na kusambaza magonjwa mbalimbali kama vile kipindupindu ambacho ni ugonjwa hatari.

Wadudu hawa huweza kugusa kinyesi cha mgonjwa na kutua kwenye chakula cha watu wazima na kuwaambukiza ugonjwa huo.Wadudu wengine hatari kwa maisha ya watu ni kama kombamwiko na viroboto ambao hupatikana jikoni, mahali ambapo chakula hutayarishiwa.

Taka zote zinazotokana na vitu vyote vilivyotumiwa zinafaa kutupwa mahali panapofaa kama vile jalalani au zikachomwa. Nyasi nazo zinazozunguka hospitali zetu zinafaa kukatwa ili kuwafukuza mbu wanaosababisha ugonjwa wa malaria. Panya wanaobeba viroboto wanaosababisha ugonjwa wa tauni hujificha humo pia. Aidha, nyoka wanaweza kujificha humo na kutambaa hadi vyumbani. Mikebe na chupa zilizotumiwa zinafaa kutupwa shimoni na kufukiwa ili kuzuia mbu kuzalia ndani mwake na viluwiluwi vyake kukulia humo, hasa maji ya mvua yanapoingia kwenye vyombo hivyo.

Hali hii ya usafi wa mazingira ya hospitali inafaa kuzingatiwa ili kuzuia magonjwa yanayoweza kujitokeza. Shughuli za usafi ni nyingi na kila mtu anayefika hospitalini ni lazima ajaribu kuimarisha usafi katika mazingira anamoingia. Wagonjwa na watu wote wanaowaangalia au kuwasaidia wanapaswa kutunza usafi kila mahali walipo kwa manufaa ya watu wanaoishi katika maeneo hayo. Wauguzi na madaktari pamoja na wafanyakazi wote lazima wachunguze kama usafi umezingatiwa katika hospitali nzima.

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Chagua jibu moja kati ya haya. Mazingira ni:
    a. Sehemu ya nje au ya ndani ya nyumba iliyotengenezwa maalumu kwa watu kukaa na kuzungumza.
    b. Hali au mambo yanayomzunguka kiumbe katika sehemu anapoishi au maisha yake.
    c. Sehemu ambapo kitu au mtu huweza kukaa.
2. Usafi wa mazingira unachangia nini katika maisha ya binadamu?
3. Usafi wa mazingira utatusaidiaje kutumia rasilimali zetu vizuri?
4. Wadudu hawa husababisha magonjwa yapi?
    1. nzi
    2. mbu
5. Ugonjwa wa kipindupindu husababishwa na nini?
6. Ni nini maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu?
    1. jalala
    2. bwelasuti
7. Taja wadudu wengine wanne uwajuao wanaosababishwa na uchafu.

## 2.2. Msamiati kuhusu Usafi Hospitalini

### ZOEZI LA 2:

***Oanisha maneno katika kundi A na maana zake kutoka kundi B.***

| A. Maneno | B. Maana |
|---|---|
| 1. Kuambukiza | a. Mahali pa kupumzika palipopandwa miti au maua. |
| 2. Kiluwiluwi | b. Jumla ya mali aliyonayo mtu au nchi. |
| 3. Bustani | c. Ugonjwa wa aina yoyote wa binadamu. |
| 4. Rasilimali | d. Kueneza ugonjwa au kitu kibaya |
| 5. Ndwele | e. Mdudu aliyeanguliwa kutoka yai la mbu au nzi. |

### ZOEZI LA 3:

***Tumia maneno yafuatayo katika sentensi fupi.***

1. Kutiliwa maanani
2. Kupiga deki
3. Huduma
4. Kuambukiza
5. Kipindupindu

### ZOEZI LA 4:

***Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yafuatayo (viroboto, bwelasuti, mbu, huchangia parefu, viroboto wa panya, vifaa, nyasi, nyoka, wangezingatia, nzi):***

1. Usafi wa mazingira........................kurefusha umri wa kuishiwa binadamu.
2. Watu wengi wangeelimishwa vizuri, .....................usafi wa mazingira.
3. Ni lazima................vya hospitalini visafishwe vizuri.
4. Mara nyingi wadudu kama ................na hujenga makao yao sakafuni.
5. Watu wanapaswa kuvaa ................................. ili waweze kujikinga na uchafu.
6. ................................zinafaa kukatwa ili kuwafukuza mbu wanaosababisha ugonjwa wa malaria.
7. Wadudu wanaosababisha ugonjwa wa tauni huitwa ................
8. ...................ni mnyama anayetambaa ambaye hujificha nyasini.

## ZOEZI LA 5:

***Wanafunzi wawili wawili, tajeni majina ya vifaa vifuatavyo ambavyo hupatikana katika mazingira ya hospitali pamoja na umuhimu wake.***



## 2.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi -ngeli-

## ZOEZI LA 6:

***Andika upya sentensi zifuatazo kwa kutumia kiambishi -ngeli- badala ya kiambishi -nge-. Fananisha sentensi unazozipata na sentensi za awali.***

**MFANO:**

Sisi tungeshirikiana ipasavyo, tungejenga nchi imara.

Sentensi hizi ingawa zinatumia -ngeli- badala ya -nge- hazitofautiani kimaana na zile za awali.

1. Wanafunzi wangesoma vizuri, wangefaulu mtihani wa taifa.
2. Mungu huwapenda watu; asingewapenda, asingewaumba.
3. Tusingeandika vitabu, tusingepata vitabu vya kufundishia.
4. Wao wangekuwa Wakristo, wangewasaidia walemavu.

Kiambishi -ngeli- kinaweza kutumiwa katika hali kanushi na vilevile katika hali yakinishi.

| Hali yakinishi/Tungo yakinishi | Hali kanushi/Tungo kanushi |
|---|---|
| 1. Ni**ngeli**kuwa na koti safi sana, ni**ngeli**kwenda harusini. | Ni**singeli**kuwa na koti safi sana, ni**singeli**kwenda harusini. |
| 2. Kama ni**ngeli**kuwa na pesa sasa, ni**ngeli**nunua shati hili. | Kama ni**singeli**kuwa na pesa sasa, ni**singeli**nunua shati hili. |
| 3. Ni**ngeli**jua kuwa mvua itanyesha, ni**ngeli**nunua mwavuli jana. | Ni**singeli**jua kuwa mvua itanyesha, ni**singeli**nunua mwavuli jana. |
| 4. Kama wa**ngeli**wahi kuondoka siku ile, mvua i**ngeli**wanyeshea | Kama wa**singeli**wahi kuondoka siku ile, mvua i**singeli**wanyeshea. |
| 5. Wanafunzi hawa wa**ngeli**chelewa asubuhi hii, wa**ngeli**kosa mtihani wa Kiswahili. | Wanafunzi hawa wa**singeli**chelewa asubuhi hii, wa**singeli**kosa mtihani wa Kiswahili. |

**Tanbihi:** Katika matumizi ya kiambishi hiki, tunaweza kukanusha kwa kutumia kikanushi -si- kama ilivyoonyeshwa kwenye mifano hapo juu.

**Chunguza maelezo muhimu kuhusu matumizi ya kiambishi -ngeli-**

Kiambishi -ngeli- ni kiambishi ambacho hutuarifu juu ya hali ya masharti. Kinapotumiwa humaanisha kuwa tendo moja ni lazima lifanyike ndipo tendo jingine nalo lifanyike.

Hali kadhalika, kiambishi -nge- hutumiwa kuonyesha majuto au kuwa kama tendo fulani halifanyiki, tendo jingine nalo haliwezi kutokea. Lakini katika hali hii ya mwisho tunaelewa kwamba kuna uwezekano wa kufanyika kwa tendo hilo na kisha jambo hilo nalo litokee.

**Katika hali ya kuonyesha uwezekano**

**MIFANO:**

- Ningelikuwa na pesa, ningelimjengea mzazi nyumba nzuri. Maana yake ni kuwa mimi sina pesa wala sikujengea mzazi nyumba nzuri, lakini nikipata pesa sasa hivi ninaweza kumjengea nyumba nzuri.
- Ningelimjua msichana yule, ningelimshauri kuacha tabia mbaya. Maana yake ni kwamba simjui msichana yule, lakini kumjua kwangu kwasababisha kumpa ushauri wa kuacha tabia yake mbaya.

**Katika hali ya kuonyesha majuto**

**MIFANO:**

1. Ningelikuwa msichana mwenye moyo wa utulivu, ningelijilinda kujiunga na vijana wenye tabia mbaya za uasherati.

Maana yake ni kuwa mimi sikuwa msichana mwenye moyo wa utulivu ijapokuwa ningelihitaji kuwa msichana mwenye moyo wa utulivu ili nijiepushe na urafiki na vijana wenye tabia mbaya za uasherati, lakini ninajuta kwa sababu sikuweza kuwa na moyo wa utulivu.

2. Ningelikuwa mkristo wa kweli, ningeliacha kuvuta sigara au kuchukua dawa za kulevya ambazo zimeniharibia afya.

Maana yake ni kuwa mimi si mkristo wa kweli na ninajuta kuwa uvutaji wa sigara na kuchukua dawa za kulevya kumeniharibia afya.

**ZOEZI LA 7:**

***Zikamilishe sentensi zifuatazo ili zilete maana kamili.***

**MIFANO:**

- Angelikuwa mfalme, angeliishi raha mustarehe.
- A**singeli**kuwa mfalme, a**singeli**ishi raha mustarehe.

1. Chumba hiki kingelikuwa kikubwa, ……….……….……….......
2. Chumba hiki kisingelikuwa kikubwa, ……………….................
3. Wali usingelikuwa mtamu, ……………………..........................
4. Minazi ingelizaa madafu mengi, …………….......................
5. Minazi isingezaa madafu mengi, ……………………........
6. Mwanafunzi angelisoma kwa bidii, ……………………........
7. Ningelikuwa daktari, .......………………………........................
8. Tungelikuwa na pesa, ……………………………......................
9. Ungelikuwa na ujuzi kamili, …………………........................
10. Wapishi wangelikuwa na viungo, .................................

## 2.4. Matumizi ya Lugha

### ZOEZI LA 8:

***Chagua maneno haya kufuatana na maana zake na kuyaandika katika makundi yake halisi.***

Glovu

Machela

Dobi

Sabuni

Nesi

**A**
**(Vifaa vya hospitalini)**

**B**
**(Wafanyakazi wa hospitalini)**

### ZOEZI LA 9:

***Oanisha maneno yafuatayo hapo chini na maana zake:***

| Maneno | Maelezo |
|---|---|
| Glovu | Mchanganyiko wa vitu vinavyotokana na mafuta na aina mojawapo ya magadi na ambayo hutumiwa kwa kufulia, kuogea au kusafisha vitu. |
| Machela | Kitu kama soksi kinachovaliwa mkononi ambacho hutengenezwa kwa mpira, ngozi au kitambaa na kwa kawaida huwa na nafasi kwa kila kidole. |
| Dobi | Kifaa kinachotengenezwa kwa madini, aghalabu ya chuma, chenye visu viwili vilivyounganishwa kwa msumari mdogo na tundu mbili za kuingizia vidole, kinachotumiwa kukatia kitu k.v. nguo au nywele. |
| Sabuni | Mtu anayefanya kazi ya kufua na kupiga pasi nguo za watu kwa malipo. |
| Nesi | Kitu kama gome gumu kilichotengenezwa kwa unga maalumu na kitambaa kinachofungwa sehemu ya mwili iliyovunjika ili kushikanisha mifupa iliyovunjika. |
| Makasi | Muuguzi wa wagonjwa hospitalini. |
| Plasta | Kitu kama kitanda, aghalabu hutumiwa kubebea mtu aliye mgonjwa au maiti. |

### 2.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano na Mawasilisho

**ZOEZI LA 10:**

***Soma kifungu kuhusu "Umuhimu wa Usafi wa Mazingira Hospitalini", kisha uwasilishe mawazo makuu hadharani.***

### 2.6. Kuandika: Utungaji wa Kifungu

**ZOEZI LA 11:**

***Tunga kifungu kifupi kuhusu umuhimu wa usafi hospitalini kwa kutumia maneno yafuatayo: (usafi, kuhara, wadudu, vyoo, mazingira, uchafu).***

## SOMO LA 3: ADABU HOSPITALINI

**ZOEZI LA 1:**

***Tazama mchoro ufuatao kisha ueleze vitendo vinavyofanywa na watu waliopo katika mchoro.***




### 3.1. Kusoma na Ufahamu: Maelekezo na Kanuni Hospitalini

Soma kifungu cha habari kinachofuata kuhusu maelekezo na kanuni zinazofaa kuzingatiwa hospitalini, kisha jibu maswali yanayofuata hapo chini.

Jina langu ni Mugisha. Juzi nilikuwa ninahisi homa kali. Hivyo nilienda katika hospitali moja iliyopo mjini Rubavu. Nilikuwa na ndugu yangu mdogo

Semana aliyekuwa amenisindikiza hospitalini. Wakati nilipokuwa nangoja usaidizi wowote kutoka kwa daktari, nikikaa kwenye benchi moja mbele ya ofisi yake, nililiona tangazo lililokuwa limebandikwa kwenye ukuta na kumwomba ndugu yangu anisomee kilichoandikwa pale. Nilihofia kuvunja sheria yoyote ya hospitali kutokana na kutosoma kile kilichoandikwa. Ndugu yangu alikubali kunisomea. Hivyo alianza kunisomea tangazo hilo kuanzia mwanzo hadi mwisho. Tangazo lilisomeka ifuatavyo:

Kwa manufaa ya wagonjwa na watu wengine wanaotembelea mazingira ya hospitali hii, uongozi wa hospitali hii unataka kuwajulisha mambo yafuatayo:

1. Wagonjwa wanapaswa kuonyesha maadili mema ya kuwaheshimu wenzao pamoja na wafanyakazi wa hospitali.
2. Inakatazwa kugombana, kutukana, kuiba na kuwadharau watu wengine.
3. Mtu yeyote wa nje haruhusiwi kuingia katika kungawi wala chumba cha upasuaji.
4. Kila mgonjwa inambidi aheshimu masharti ya daktari ya kutumia dawa kama ilivyoagizwa.
5. Usafi ni msingi wa afya. Mazingira yatahifadhiwa ipasavyo na kila mtu anapaswa kuwajibika katika utunzaji wa usafi kila mahali alipo.
6. Ni mwiko kuvuta sigara katika eneo la hospitali.
7. Wagonjwa waliolazwa hospitalini na wengine wanaowahudumia wanaombwa kutopiga kelele wakiwa katika wodi.
8. Hairuhusiwi kamwe kuingiza na kutumia pombe pamoja na dawa za kulevya katika eneo la hosptitali.
9. Mienendo mibaya isiyoendana na maadili mema imepigwa marufuku katika eneo la hospitali.
10. Kila mtu anatakiwa kuwa na moyo wa huruma kwa kusaidia wale wasiojiweza na wenye udhaifu.

Mimi nilifurahia maonyo na mawaidha hayo yaliyotolewa na Daktari Mkuu wa hospitali. Zamu yangu ilifika nikaingia kwa daktari na nikahudumiwa vizuri. Baada ya kupewa dawa, nilianza kutembea kuelekea nyumbani. Ghafla nilisikia sauti za watu wengi: «Piga…, jichoni, mtupe chini wee…, ngumi nyingine!…». Nilipogeuka kuangalia nini kilikuwa kikiendelea pale sikuamini macho yangu! Vijana wawili walikuwa wanapigana! Nilisikitika sana na kumwambia ndugu yangu, «Kwa nini watu wengine wanawatazama bila kuwatenganisha ili wasiendelee kugombana? Kwa kweli, watu hao wangaliingilia kati kabla ya kupigana, wasingaliweza kuumizana.» Mmoja alikuwa amemuumiza mwenzie vibaya sana akisingizia kuwa amemwibia chupa ya pombe.

Baada ya muda, Polisi waliitwa ili kutatua tatizo hili. Ilibidi kwanza vijana hao watibiwe majeraha waliyokuwa nayo usoni na miguuni kabla ya kuwapeleka kwenye kituo cha polisi ili kuwahoji kuhusu ugomvi wao. Hapo niliendelea kumwambia ndugu yangu, «Kwa nini vijana hawa watumie nguvu zao kwa kupigana badala ya kuzitumia kwa kuzalisha mali? Wangalisoma tangazo la Daktari Mkuu wa Hospitali hii kuhusu maadili mema, wasingalishambuliana namna hii! Wao walikiuka maagizo yaliyotolewa na kuvunja kanuni za hospitali.»

Mimi na ndugu yangu tuliendelea na safari yetu ya kurudi nyumbani na kushauriana kuhusu maadili na mienendo mizuri inayofaa kumtambulisha kila mgonjwa na mtu yeyote anayetembelea mazingira ya hospitali. Tulifurahia jinsi uongozi wa hospitali yetu ulivyotilia mkazo kuwahimiza watu kuwa na maadili na mienendo mizuri. Tangu siku hiyo, niliamua kuwaonya watu wote waheshimiane na kuzingatia maagizo ya Madaktari wetu ili wasipate adhabu zisizostahili. Ndugu yangu naye aliendelea kwa kusema, «Vijana wale wasingaligombana, wasingalipelekwa kituo cha polisi kuadhibiwa.»

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Taja watu wanaozungumziwa katika kifungu hiki.
2. Watu hawa walikuwa wapi?
3. Tangazo linalozungumziwa linahusu nini?
4. Tangazo hilo lilikuwa wapi? Ni nani aliyelisoma?
5. Taja vitu angalau vitano ambavyo haviruhusiwi hospitalini.
6. Unadhani ni kwa sababu gani mtu yeyote wa nje haruhusiwi kuingia katika kungawi wala chumba cha upasuaji?
7. Ni kitu gani kilichosababisha vijana wawili kugombana?
8. Wao walivunja sheria zipi kutokana na tangazo la Daktari Mkuu?
9. Vijana hao waliamuliwa nini kutokana na ugomvi wao?
10. Ni jambo gani linalokudhihirishia kuwa Mugisha alisikitishwa na mapigano ya vijana hao?
11. Kwa nini Mugisha na nduguye walifurahia uongozi wa hospitali yao?
12. Ni maonyo gani anayoyatoa ndugu yake Mugisha ili watu wasipate adhabu zisizostahili?

## 3.2. Msamiati kuhusu Adabu Hospitalini

**ZOEZI LA 2:**

***Eleza maana ya maneno yafuatayo na baadaye uyatumie kwa kuunda sentensi zenye maana:***

1. Mwiko
2. Marufuku
3. Benchi
4. Ghafla
5. Afya
6. Mhudumu
7. Kujeruhi
8. Kugombana

**ZOEZI LA 3:**

***Jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno uliyopewa: kupiga kelele, heshima, kuvunja sheria, maadili mema, kugombana, kuheshimu.***

1. Kila mtu anapaswa kuwa na hofu ya ............................................ mahali popote alipo.
2. Mtoto huyu anafurahisha kwa sababu anaonyesha ................................ ......kwa watu wakubwa.
3. Mgonjwa alipewa ushauri kuhusu........................................ na daktari alipokuwa hospitalini.
4. Unapokuwa katika wodi unakatazwa ..................................kwa sababu kuna wagonjwa ambao wako katika hali mbaya.
5. .................................. ni kufanya matata kwa kutoa maneno makali.

**ZOEZI LA 4:**

***Jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno kutoka kifunguni :sheria, kuvuta, hawakuwatenganisha, pombe, benchi, wasingalipigana, kuhudumiwa, kutazama.***

1. Vijana wawili walipokuwa wanapigana watu .................................
2. Wagonjwa sana huhitaji ........................................................
3. Si vizuri ...................................................tu watu wanapopigana.
4. Vijana wawili waliingiza ................................................hospitalini.
5. Vijana wake wawili wangalisoma tangazo lile, ...............................
6. Nchini Rwanda hairuhusiwi ......................................sigara mahali ambapo hukutania watu wengi.
7. ...............................................................ni kifaa cha kukalia.
8. Wagonjwa waliopigana hawakujua .............................za hospitali.

## ZOEZI LA 5:

***Jaza jedwali lifuatalo kufuatana na mada zilizotolewa hapa chini:***

| Mambo manne yanayokatazwa katika tangazo | Mambo manne yanayoruhusiwa kufanywa katika tangazo |
|---|---|
| 1) ......................................... | 1) ............................................... |
| 2) ........................................ | 2) ................................................ |
| 3) ......................................... | 3) ................................................ |
| 4) ......................................... | 4) ................................................ |

### 3.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi chenye Dhana ya Masharti -ngali-

## ZOEZI LA 6:

***Jadilini kuhusu matumizi ya -ngali-katika sentensi zinazofuata:***

1. Ninyi m**ngali**kuwa na muda wa kutosha, tu**ngali**zungumzia mengine mengi kuhusu adabu.
2. Watoto wale wa**ngali**jifunza vizuri, wa**ngali**pewa zawadi nyingi.
3. Wanafunzi wa**singali**kuwa na alama za kutosha, wa**singali**fanya mtihani wa taifa.
4. Sisi tu**singali**fika mapema, tu**singali**fanya kazi nyingi.

Linganisheni maoni yenu kutoka makundi tofauti na maelezo hapa chini.

Viambishi **-nge-**, na -**ngeli**-: mzungumzaji au mwandishi anaweza kuvitumia katika nafasi ya kiambishi **-ngali-** katika nyakati tofauti. Viambishi hivi hubeba dhana ya masharti. Dhana hii inalifanya tendo fulani litegemee tendo jingine katika kutendeka kwake. Kwa mfano, kama umetumia **-ngali-** katika sehemu ya kwanza ya sentensi yako endelea kutumia pia **-ngali-** katika sehemu ya pili. Ndani ya sentensi zinazobeba hali ya masharti, ni lazima kuelewa maana ya sentensi nzima kutokana na kutegemeana kwa vitendo. Ikumbukwe kuwa viambishi vya hali ya masharti hutumiwa katika hali yakinishi na hali kanushi. Katika hali kanushi -**si**- huwekwa baada ya kiambishi nafsi cha kitenzi cha hali yakinishi.

## ZOEZI LA 7:

***Kamilisha sentensi zifuatazo ili zilete maana kamili.***

1. Raia wote wangalifuata mashauri ya usafi na kuhifadhia mazingira, magonjwa yanayosababishwa na uchafu …..............................sana.
2. ………………………………………..., tusingalipata hasara hii.
3. Ningaliepuka unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya mke wangu, ……….msiba huu.
4. Nisingaliponda mali yangu yote katika mahitaji yasiyo muhimu, ..........................
5. Serikali ya Rwanda isingalichukua mikakati thabiti kuhusu unyanyasaji wa kijinsia, ................
6. Wangalijua nia yangu katika kutetea haki za wanawake, .................. ...........................
7. Ungalionana na daktari, .................................................................... .....................................
8. Vijana wangaliepuka dawa za kulevya, bila shaka ............................. .............................
9. Barabara zote zingalikuwa za lami, kila eneo nchini Rwanda ............ ........................

## ZOEZI LA 8:

***Kanusha sentensi zifuatazo:***

1. Tungalipanda miti ya kutosha, tungalizuia mmomonyoko kupasua mlima huu.
2. Bwana yule angalijua usawa wa kijinsia, angalikuwa na maendeleo katika familia yake.
3. Ungalikuwa na moyo wa kiutu, ungalimhudumia mwanafunzi mlemavu yeyote darasani.
4. Wanafunzi wangalisoma kwa bidii, wangalishinda mitihani kwa urahisi.

### 3.4. Matumizi ya Lugha: Msamiati wa Adabu

**ZOEZI LA 9:**

***Yafuatayo ni baadhi ya maneno ya adabu yanayoweza kutumiwa nyumbani, shuleni au sokoni. Tunga sentensi moja kwa kila neno.***

1. Tafadhali
2. Asante
3. Samahani
4. Karibu!
5. Shukrani
6. Naomba
7. Pole
8. Hodi!
9. Shikamoo!
10. Marahaba

**Mienendo mizuri hospitalini humtaka kila mtu azingatie mambo yafuatayo:**

- Kuonyesha maadili mema;
- Kuwaheshimu wengine;
- Inakatazwa kugombana, kutukana, kuiba na kuwadharau wengine, kuvuta sigara;
- Kuheshimu masharti ya daktari na wafanyakazi wa hospitali,
- Kuwa na usafi;
- Kutopiga kelele katika wodi.

### 3.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

**ZOEZI LA 10:**

***Jadili mada zifuatazo:***

1. Namna watoto wanavyoweza kuimarisha adabu mbele ya wazazi nyumbani kwao.
2. Adabu ni msingi wa uhusiano mwema kati ya mtu na mtu mwingine. Eleza.

### 3.6. Kuandika: Sifa za Aya katika Uandishi

**ZOEZI LA 11:**

***Kila mwanafunzi aandike mambo muhimu matatu ya kuzingatiwa katika kukuza adabu hospitalini na kuyajadili katika aya tatu.***

## TATHMINI KUHUSU MADA YA KWANZA

***Jibu maswali yafuatayo:***

1. Taja angalau vitu vitano muhimu vinavyopatikana katika mazingira ya hospitali au zahanati.
2. Taja sehemu tatu za hospitali na kueleza shughuli zinazofanyiwa katika sehemu hizo.
3. Eleza majukumu ya wafanyakazi angalau wanne wanaopatikana hospitalini.
4. Thathmini shughuli za kuboresha usafi zinazofanywa katika moja ya hospitali ulizowahi kutembelea.
5. Jadili mwenendo unaofaa katika mazingira ya hospitali au zahanati kwa minajili ya kujilinda na magonjwa.
6. Kwa kutumia viambishi -*nge-, -ngeli-* au -*ngali-,* andika aya nne kwa kujadili hasara zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya taulo moja kwa watu zaidi ya mmoja; kisha, toa suluhisho ili kuepukana na madhara yanayoweza kujitokeza.

# MADA KUU YA 2

## MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAZINGIRA MBALIMBALI

# MADA KUU YA 2: MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MAZINGIRA MBALIMBALI

## MADA NDOGO: Msamiati katika michezo

**Uwezo Upatikanao katika Mada:** Kusikiliza kwa makini, kusoma vifungu vya habari na kutumia msamiati muhimu katika mazingira ya michezo; kutumia majina ya ngeli ya Li-Ya kwa usahihi.

**Malengo ya Ujifunzaji:**

- Kubainisha na kuainisha aina za michezo na vifaa vinavyotumiwa michezoni.
- Kutaja majina ya vifaa vya michezo mbalimbali iliyopo shuleni.
- Kueleza umuhimu wa michezo.
- Kuviweka vifaa vya michezo katika makundi na kubainisha majina yake.
- Kutunga na kujaza sentensi tofauti kwa kuzingatia matumizi ya majina ya ngeli ya LI-YA.
- Kusahihisha tungo tofauti zinazopatikana na makosa ya kisarufi kuhusu majina ya ngeli ya LI-YA.

### Kazi Tangulizi

1. Mchezo ni nini?
2. Taja aina tano za michezo unayoifahamu.
3. Ni michezo gani inayopatikana kwenye shule yako?
4. Mchezo wa mpira wa miguu unahusisha wachezaji wangapi?
5. Je, kuna makosa mbalimbali yanayojitokeza katika michezo? Eleza makosa matatu yanayopatikana katika mchezo wa miguu.

## SOMO LA 4: MICHEZO SHULENI

**Tazameni mchoro huu kisha mjibu maswali hapo chini**




**ZOEZI LA 1:**

***Zungumzia unayoyaona kwenye mchoro.***

### 4.1. Kusoma na Ufahamu: Timu Hodari

Soma kifungu hiki kuhusu "Timu hodari" kisha jibu maswali yanayofuata hapo chini.

Baada ya kumaliza masomo yangu ya sekondari kidato cha tatu, mimi na wanafunzi wenzangu tulipenda tuchaguliwe kuendelea na masomo yetu ya kidato cha nne hadi cha sita katika shule moja ya sekondari yoyote iliyopo Mkoa wa Kusini. Matokeo ya mitihani wa taifa yalipotangazwa nilijikuta nimechaguliwa kusomea wilayani Huye, Mkoa wa Kusini, kwenye Shule ya Sekondari ya Menge. Shule hii ni nzuri sana kwani ina viwanja tofauti vya michezo kama mpira wa miguu, mpira wa wavu, mpira wa kikapu na mingineyo. Mimi kama kawaida nilikuwa ninajulikana kama mchezaji hodari wa mpira wa miguu. Nilifurahi sana kwamba ndoto zangu zilikuwa zimetimia. Mpira huu unapendwa na watu wengi na umepewa majina mengi: kandanda, kabumbu, soka na majina mengine.

Tulipofika kwenye shule hiyo, mimi nilijiunga na wanafunzi wengine tukaunda timu nzuri na kali sana. Kalisa alikuwa mmoja wa wanafunzi wazuri katika lugha ya Kiswahili na alipenda kutusimulia habari tofauti za michezo. Kwenye shule tuliposomea yeye alipenda kuiga mtindo wa watangazaji habari ungedhani ameajiriwa kwenye Redio Rwanda. Katika wakati wa mapumziko, wanafunzi wengi walipenda kumzunguka na kusikiliza alivyotumia mtindo wa

lugha ya utangazaji wa mpira wa miguu. Baadhi ya maneno aliyoyarejelea katika mazungumzo yake yalikuwa pamoja na kuvisha kanzu, kutoa bomba, mpira kuwa mwingi, kukokota ngoma, kukata mbuga, mpira kuambaamba nje, kuunawa mpira, kuotea, harusi, kuunyaka mpira, refa/mpiga kipenga/ mpiga filimbi, washika vibendera na mengine tunayozoea kusikia kwenye redio mbalimbali yakitamkwa na watangazaji habari wa michezo.

Kwa hivyo, kila mara timu yetu ilipocheza yeye alikuwa karibu kuwaelezea wanafunzi wengine kuhusu matukio ya uwanjani. Viongozi wa shule yetu nao walituunga mkono na kutusaidia ipasavyo. Walitununulia jezi, viatu vya mpira, mipira, nyavu na vifaa vingine ambavyo vinahitajika katika michezo. Wakati wa kufanya mazoezi, viongozi walikuwa wanatupa ruhusa na kutupatia mahitaji yote muhimu. Timu yetu ilipendwa sana kutokana na uzoefu wake wa kushinda timu nyingine. Kila mahali tulipokwenda hatukumuacha Kalisa ambaye alizoea kutangaza sifa za kila mchezaji kwa wanafunzi na viongozi wa shule.

Wakati mmoja tulianza mashindano ya mpira wa miguu ya shule za sekondari nchini Rwanda. Timu yetu ilizishinda timu zote zilizokuwa zimechaguliwa wilayani Huye. Baada ya hapo, ilichaguliwa kama timu ambayo ingewakilisha wilaya ya Huye. Kila siku tulifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kuzishinda timu zote na kuibuka na ushindi. Hapo tulikuwa tumeshapata mashabiki wengi katika wilaya yetu na hata wilaya nyingine. Tuliendelea na michezo, tukacheza na timu zilizoteuliwa kutoka wilaya tofauti mkoani Kusini. Tulicheza na timu hizo tukapata ushindi mnono.

Timu ya mwisho ambayo tulicheza nayo ni ya Shule ya Sekondari ya Mudehe. Timu hii ilikuwa na wachezaji hodari kabisa. Lakini kama wahenga wasemavyo, “Lazima kuwe na mshindi na mshindwa.” Baada ya dakika arubaini za kipindi cha kwanza, tulikuwa tumepata mabao matatu kwa nunge na mashabiki wetu wakiendelea kushangilia ushindi wetu. Wakati huo ndipo kiongozi wa shule ya Mudehe aliposikika akisema, “Tungejua kwamba timu hii ilikuwa kali namna hii, tungefanya mazoezi ya hali ya juu.” Mashabiki wengine waliohudhuria kutazama mchezo wetu kutoka mikoa tofauti nao walishangilia huku wakisema, “tungekuwa na timu hodari kama hii ya shule ya Menge, tungefika mbali sana katika mashindano haya.” Kipindi cha pili kilianza na timu yetu iliendelea na mchezo huku ikiwa imeongoza mpaka mwisho wa mchezo. Hivyo tukafanikiwa kuingia nusu fainali. Katika mchezo wa nusu fainali, tulipaswa kucheza na timu kutoka mkoa wa Mashariki. Tulipewa wiki mbili za kujitayarisha ili tucheze mchezo wa nusu fainali.

Siku ya mchezo ilipofika tulicheza kufa na kupona ili tuweze kupata ushindi. Kwa bahati mbaya, tulitoka sare katika dakika tisini za mchezo tukiwa sifuri kwa sifuri. Ilibidi tuingie katika ngwe ya kupigiana mikwaju ya penalti. Mara hii, tulifurahi kwa sababu timu yetu ilikuwa na wachezi wengi hodari kwa

kupiga mikwaju ya penalti. Kwa hiyo, tuliweza kuingiza mikwaju mitatu katika lango la wapinzani wetu huku wao wakifanikiwa kuingiza mikwaju miwili tu. Hivyo, safari ya wapinzani wetu ikamalizikia hapo.

Siku ya fainali ilipowadia, mashabiki walikuwa wengi mno. Timu yetu ilicheza na timu moja kutoka mjini Kigali. Mashabiki wengi walikuwa wanatuunga mkono na kututia hamasa ili wachezaji wetu waweze kufunga magoli mengi. Kila mchezaji alitumia nguvu zake na mbinu nyingi ili kuweza kupata ushindi. Mchezo huo ulifurahisha wengi sana kiasi kwamba kiongozi wetu aliahidi kutupatia zawadi kubwa baada ya kumaliza mashindano hayo na kujinyakulia kombe la taifa. Wachezaji nao walifanya juu chini mpaka timu ikafunga magoli mawili kwa nunge. Kwa hiyo, wachezaji wote walianza kutambua nafasi ya kocha na kusema, “Tusingefuata mashauri ya kocha wetu, tusingefikia kiwango hiki cha kuwaridhisha wengi.”

Kutokana na uhodari tulioonyesha katika mashindano hayo, uongozi wa shule yetu uliamua kuimarisha michezo mbalimbali katika shule yetu. Kila Jumamosi, wanafunzi wengi hukutana kushiriki na michezo na hata kuzungumzia habari za michezo mbalimbali wakijadiliana kuhusu umuhimu wake. Kalisa ambaye ndiye hodari wa taarifa zote za michezo hupewa muda wa kuwasimulia wenzake jinsi ambavyo wachezaji hufaidika kwa vipawa vyao katika shughuli za michezo.

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Taja majina ya shule zinazozungumziwa katika kifungu hiki.
2. Mchezo wa mpira wa miguu una majina mengi, majina hayo ni yapi?
3. Mchango wa viongozi kwa timu hii ulikuwa upi?
4. Taja michezo mingine tuchezayo shuleni.
5. Namna gani Kalisa anajihusisha na shughuli za michezo?
6. Ni timu gani ambayo ni hodari kuliko timu nyingine? Eleza.
7. “Lazima kuwe na mshindi na mshindwa.” Eleza jinsi kauli hiyo huhusiana na kifungu cha habari ulichosoma.
8. Kwa nini kulikuwa lazima kupiga penalti katika mchezo wa nusu fainali? Matokeo yalikuwa yapi?
9. Ni timu zipi zilizowania kombe la taifa katika mchezo wa fainali?
10. Ushindi wa timu ya Menge ulitokana na nini?
11. Kwa maoni yako michezo ya riadha ni michezo gani?
12. Wanaotazama mpira wakati wa michezo huitwa .......................

## 4.2. Msamiati kuhusu Michezo Shuleni

**ZOEZI LA 2:**

***Chagua jibu katika kundi B kwa kuelezea neno kutoka kundi A.***

**MFANO:**

| Kundi A | Kundi B |
|---|---|
| 1. hodari | a) utando wa nyuzi zilizosukwa na kuacha sehemu zenye uwazi ili kufunga kwenye milingoti ya goli. |
| 2. rejesta | b) hali ya kukaa au kujishughulisha na jambo au kitu kwa muda mrefu. |
| 3. wilaya | c) mchezo wa mpira wa miguu. |
| 4. uzoefu | d) michezo ya mazoezi ya viungo vya mwili. |
| 5. mashindano | e) shindano au mashindano ya mwisho kabisa, hasa ya michezo, ili kupata mshindi. |
| 6. wavu | f) -enye kuweza kufanya kinachowashinda wengine. |
| 7. kandanda | g) -pa mtu zawadi au nishani. |
| 8. kutunukia | h) mtindo wa lugha inayotumika mahali penye shughuli fulani. |
| 9. penalti | i) mapambano baina ya pande mbili au zaidi kutafuta mshindi hususan katika michezo. |
| 10. fainali | j) adhabu itolewayo kwa timu ambayo mchezaji wake amekiuka sheria za mchezo au kipindi kinachofuata baada ya timu kutoka suluhu baada ya kucheza kila timu huteua wachezaji watano na kila mchezaji hupewa nafasi ya kupiga mpira ndani ya mita kumi na mbili akiwa amebakia yeye na kipa tu wa timu pinzani. |
| 11. riadha | k) Sehemu ndogo katika mkoa lakini kubwa kuliko tarafa. |

**ZOEZI LA 3:**

***Bainisha nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo.***

**MFANO:**

kulinda = mlinzi.

1. Kupumzika 2. Kutangaza 3. Kucheza 4. Kushinda

5. Kuzoea 6. Kuongoza 7.Kushindwa

**ZOEZI LA 4:**

***Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yanayopatikana katika kifungu cha habari:soka, timu, kabumbu, michezo, riadha, kandanda, mtangazaji.***

1. Wachezaji wa ........................................... ni kumi na moja.

2. Shule yetu ina .......................mingi sana kama vile mpira wa miguu, mpira wa kikapu, mpira wa wavu.

3. Kukimbia, kuruka, kutupa mkuki ni michezo ya ...............................

4. Majina ya mpira wa miguu: ...........................................................

5. ........................................................wa mpira huwa na lugha maalum kuelezea matukio yanayotokea uwanjani.

## 4.3. Sarufi: Matumizi ya majina ya ngeli ya LI-YA

**ZOEZI LA 5:**

***Chunguza sentensi zifuatazo na kuandika viambishi vya ngeli ya LI- YA vinavyopatikana katika vitenzi.***

**MFANO:**

***Shamba letu linaota mimea tele.***
***linaota: li- ni kiambishi ngeli ya li – ya ya nomino shamba.***

1. Mabao ya timu yetu yalikuwa matatu.

2. Somo tulilopewa na mwalimu lilitufurahisha sana.

3. Mapumziko yalimfanya apate nguvu katika kipindi cha pili cha mchezo.

4. Mazungumzo kati ya wachezaji na kocha wao yalizaa matunda.

5. Tuliyazingatia maneno yote yaliyosemwa na kiongozi wetu.

**Maelezo muhimu**

Vitenzi vilivyomo katika sentensi hapo juu, vinatumia viambishi ngeli ya Li-Ya-;

Matumizi ya viambishi hivi Li-Ya- yanategemea nomino zilizotumiwa katika sentensi hizo;

Nomino hizo zikiwa katika umoja kitenzi huchukua Li-; zikiwa katika wingi kitenzi hutumia Ya-.

## 4.4. Matumizi ya Lugha: Upambanuzi wa Maneno

**ZOEZI LA 6:**

***Chunguza maana za maneno haya ili kuyaandika katika makundi yake halisi.***

Golikipa


Ndani ya mlango

Mashabiki

Uwanjani

Washambulizi

Mlinda mlango




**ZOEZI LA 7:**

***Panga maneno yafuatayo vizuri yaunde sentensi sahihi.***

1. kucheza-ya-walianza-filimbi-kupuliza-baada-refa.
2. miguu-watu-mpira-wengi-wa-hupenda.
3. kipindi-baada-cha pili-ya-mapumziko-kilianza.
4. nyingi-ina-michezo-faida.
5. Gikondo-mashambulizi-timu-zaidi-ya-iliongeza.

## 4.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Zoezi la Kutangaza Mpira wa Miguu Redioni

**ZOEZI LA 8:**

***Soma kifungu hiki kwa kumuiga mtangazaji habari kisha uwaelezee wenzako yaliyotokea katika mchezo unaozungumziwa***

Asante sana mtangazaji mwenzangu! Mpaka sasa timu ya AMAVUBI inaongoza kwa magoli mawili kwa bila. Timu ya "LEOPARDS" ikifanikiwa kufunga mabao mawili, kutakuwa na muda wa ziada kabla ya hatua ya penalti. Iwapo matokeo yatakuwa sare. Mpira unarudishwa uwanjani. Kasereka wa "LEOPARDS" anachukua mpira. Anapiga chenga lakini anaanguka chini. Bayisenge amemfanyia kosa. Bayisenge analimwa kadi ya njano! Ameadhibiwa kwa mchezo wake usiokuwa wa kiungwana! Pedro anapata mpira. Anapiga shuti kali pale... Mpira unagonga mlingoti na kurudi uwanjani. Anaupata Hamisi. Mkwaju mkali unaolenga shabaha. Goooooooooooo! Goli rahisi kabisa! Kosa la golikipa wa Rwanda! "LEOPARDS" imepata bao la kufutia machozi! ... Mchezo unaelekea ukingoni. Refarii anapiga filimbi ya mwisho! Ni mwisho wa muda uliowekwa! "LEOPARDS" imeondolewa katika michuano. Kwa sasa, timu ya Rwanda imekuwa timu ya nne kukata tiketi ya kucheza nusu fainali.

### 4.6. Kuandika: Utungaji

**ZOEZI LA 9:**

***Timu ya mpira wa miguu ya shule yenu inacheza na timu ya shule jirani. Wewe jifanye kama mtangazaji wa redio ambaye yuko kwenye uwanja wa michezo. Tunga kifungu kifupi kwa kuwaelezea wasiohudhuria mchezo huu mambo kadhaa yanayotokea uwanjani.***

## SOMO LA 5: FAIDA ZA MICHEZO

**ZOEZI LA 1:**

***Tazama mchoro unaofuata na kujibu maswali yanayofuatia chini yake.***



## MASWALI

1. Ni michezo gani unayoiona kwenye mchoro hapo juu?
2. Michezo ina faida gani kwa binadamu?

### 5.1. Kusoma na Ufahamu: Faida za Michezo

*Soma kifungu cha habari kinachofuata ili kujibu maswali yaliyotolewa hapo chini.*

Michezo ni muhimu sana katika maisha ya binadamu. Michezo inawasaidia watu kuishi bila magonjwa hususan yale yasiyoambukiza. Unapotembelea sehemu mbalimbali ulimwenguni utaiona michezo tofauti. Lakini, michezo mikubwa inayojulikana ni mpira wa miguu, mpira wa kikapu, mpira wa wavu, kuogelea na michezo ya riadha. Michezo hii ina washiriki wengi kuliko michezo mingine.

Michezo ina faida nyingi kwa binadamu yeyote awe mdogo, mtu mzima au mzee. Michezo hujenga mwili wa binadamu na kuufanya uwe mkakamavu. Mwili unaweza kuimarishwa na chakula unachokula lakini pia michezo huimarisha mwili zaidi.

Unapochunguza vizuri, utawaona watu ambao hawafanyi mazoezi ya michezo wakiwa na miili isiyo na nguvu za kutosha. Kama mtu hana nguvu kwa kiwango hiki, mwili wake huweza kupatwa na magongwa mbalimbali kwa urahisi. Michezo ni njia moja ya kujilinda na magonjwa kama vile kisukari, shinikizo la damu, mfadhaiko, unene wa kupindukia, na kadhalika.

Michezo hufurahisha wachezaji wenyewe na hata watazamaji. Mtu anapocheza hufurahisha nafsi yake na kustarehesha roho yake mwenyewe na kuburudisha mwili wake. Hali kadhalika, michezo huwachangamsha watazamaji na kuwafurahisha kila wanapoitazama. Mashabiki wengi hupenda kuitazama michezo mbalimbali kwa kujifurahisha na kujistarehesha. Kwa hiyo, wao huweza kunufaika pia kwani kupumzika ni jambo muhimu katika maisha ya binadamu. Unapopata muda wa kupumzika na kujistarehesha unaweza kuongeza kiwango chako cha kufikiri na uwezo wako wa kutenda kazi kwa ufanisi. Aidha, unaweza hata kusuluhisha matatizo muhimu yanayojitokeza katika maisha ya kila siku.

Michezo pia hujenga uhusiano mwema kati ya mtu na mtu, wilaya na wilaya, mkoa na mkoa, na hata taifa na taifa. Kunapokuwa na mchezo wa kimataifa, wachezaji wa timu ya taifa moja hukutana na wachezaji wa timu nyingine na kujenga uhusiano wa karibu. Urafiki baina ya watu wengi huweza kuanzia michezoni. Ili kulielewa vizuri suala hili, chunguza vizuri idadi ya

watu wanaokuja kuitazama michezo katika eneo unapoishi. Mtazamaji mmoja akaapo na mtazamaji mwingine hawawezi kumaliza vipindi vyote vya mchezo bila kuambiana mambo kadhaa kuhusu mchezo huo. Watu wawili wasiofahamiana huweza kukutanishwa na mchezo wa timu yao na kuanzisha urafiki unaoweza kuwachochea kuanzisha pia miradi mingine ya kudumisha ushirikiano na mshikamano baina yao.

Michezo humletea mtu sifa nzuri na hata taifa lake huweza kujulikana na kusifiwa. Mathalani, mtu huweza kusifika katika nchi yake au kwa kiwango cha kimataifa kwa mchezaji hodari katika mchezo wa kukimbia, kucheza mpira, kuendesha baiskeli, kuogelea, ndondi, miereka na michezo mingine. Mtu akipata sifa kama hizo, hufurahia na kuridhika moyoni mwake. Aidha, sifa hizi huweza kumnufaisha anayecheza michezo hiyo kwa kumletea pato kubwa kiasi cha kuwa hata tajiri. Taifa nalo hujulikana na kupata sifa kutokana na uhodari wa raia wake ambaye ni mwanamichezo.

Kutokana na faida hizo zilizotajwa, tunapaswa kulitilia maanani suala la michezo duniani ili tuwe na maisha mema. Tujenge miili yetu kwa kucheza michezo ya aina mbalimbali hata kama hatuna uhodari wa kutosha kutokana na mchezo fulani. Tujistareheshe na kupumzisha akili zetu kwa kucheza michezo hata kama hatuna uwezo mkubwa katika michezo hiyo. Tujenge uhusiano mwema kati yetu kwa kushiriki katika michezo mbalimbali.

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Michezo ina faida gani kwa binadamu? Taja faida tatu.
2. Ni madhara gani yanayoweza kumpata mtu asiyecheza?
3. Ni namna gani urafiki kati ya mtu na mtu unavyoweza kuanzia michezoni?
4. Ni maonyo gani unayoweza kuwapa watu ambao hawachezi kwa kusingizia kwamba hawana kipawa cha michezo?
5. Taja aina tano za michezo zilizozungumziwa katika kifungu hiki.
6. Ni vipi taifa huweza kunufaika kutokana na michezo?
7. Ni namna gani urafiki ulioanzia michezoni huweza kudumishwa?
8. Kuwa na uhodari maalumu katika michezo ni njia moja ya kuongeza pato kwa mtu. Eleza.
9. Eleza jinsi ambavyo michezo hutajirisha.

### 5.2. Msamiati kuhusu Faida za Michezo

**ZOEZI LA 2:**

***Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia neno sahihi kati ya haya kutoka kifungu ulichopewa: mikakamavu, mwanamchezo, huimarisha,huwachangamua, uhusiano, magonjwa, hupumzika, kisukari, uhodari.***

1. Michezo hujenga miili ya binadamu na kuifanya iwe ................................

2. Mtu mmoja anaweza kusikika katika nchi au katika mataifa kutokana na .......................wake wa kucheza michezo tofauti.

3. Michezo....................................miili ya wachezaji na kuwaburudisha mashabiki pia.

4. Akili ya binadamu ...............................kutokana na michezo hata kama hatuna ujuzi wa kutosha.

5. Michezo hulinda mwili kupata ................................ mbalimbali kama vile shinikizo la moyo.

6. ........................................ni mojawapo wa ugonjwa unaotokana na kutoshiriki katika michezo tofauti.

7.Michezo mbalimbali .......................................................watazamaji waliohudhuria michezo.

8.Nchi na nchi nyingine zinaweza kujenga ............................................... kupitia michezo.

9. ...................................hawezi kukaa bila kucheza kama alivyozoea.

**ZOEZI LA 3:**

***Tumia maneno haya katika sentensi fupi zenye maana:***

1. binadamu
2. nafsi
3. taifa
4. mwananchi
5. kustarehesha
6. kushiriki
7. uhusiano
8. miereka
9. ukakamavu

## 5.3. Sarufi: Majina ya Ngeli ya LI-YA- pamoja na Vivumishi Vyake

### ZOEZI LA 4:

***Someni kifungu cha habari kuhusu "Faida za michezo" kisha uorodheshe vivumishi vyote vilivyotumiwa katika kifungu. Kati ya vivumishi hivyo, chagueni vivumishi vilivyomo katika ngeli ya LI-YA-.***

### ZOEZI LA 5:

***Chunguza tungo zifuatazo zenye nomino za ngeli ya LI-YA pamoja na vivumishi vyake, kisha utunge sentensi nyingine zenye kutumia nomino na vivumishi vya aina zilizotumiwa.***

1. Jiwe hili limenikata mguu vibaya.
2. Meno yenyewe yameng'olewa.
3. Shoka la Mzee Kobe halikurudishwa na Bwana Nyani.

**1. Vivumishi vya Kuonyesha**

| UMOJA | WINGI |
|---|---|
| Jahazi **hili** lilizama baharini. | Majahazi **haya** yalizama baharini. |
| Gari **hili** limeharibika. | Magari **haya** yameharibika. |
| Jina **hili** ni lake. | Majina **haya** ni yake. |
| Jahazi **hilo** lilizama baharini. | Majahazi **hayo** yalizama baharini. |
| Jahazi **lile** lilizama baharini. | Majahazi **yale** yalizama baharini. |

**2. Vivumishi vya Kumiliki**

| UMOJA | WINGI |
|---|---|
| Jicho **langu** linaniuma. | Macho **yetu** yanatuuma. |
| Jicho **lako** linakuuma. | Macho **yenu** yanawauma. |
| Jicho **lake** linamuuma. | Macho **yao** yanawauma. |

**3. Vivumishi vya Kurejesha**

| UMOJA | WINGI |
|---|---|
| Koti **lenyewe** limeibwa. | Makoti **yenyewe** yameibwa. |
| Jibu **lenyewe** limepatikana. | Majibu **yenyewe** yamepatikana. |
| Shamba **lenyewe** linalimwa. | Mashamba **yenyewe** yanalimwa. |

## ZOEZI LA 6:

***Andika sentensi zifuatazo katika umoja ama wingi:***

1. Jembe limenikata vibaya.
2. Mawe yamewekwa kando ya barabara.
3. Ondoa majani haya.
4. Meno yameng'oka.
5. Bega langu linaniuma.
6. Jengo hili kubwa ni pato la mchezaji huyo hodari.
7. Timu ya shule yetu imenunuliwa basi lenyewe kama zawadi.
8. Gari jipya litatumiwa kusafirisha wachezaji.

## ZOEZI LA 7:

***Chagua neno sahihi  na kuliandika katika nafasi iliyoachwa wazi.***

1. Dirisha………limefunguliwa (hii, hili, haya, hizi).
2. Jambazi…………lilikamatwa (huu, hilo, huyo, hiyo).
3. Tafadhali tandika jamvi………...(hiyo, hizo, hilo, hii).
4. Majani………(amekauka, zimekauka, yamekauka, imekauka).
5. Jina ..........................(la, ya, za) mwanafunzi huyu limeandikwa vibaya.
6. Mukamwezi amenunuliwa marinda ................................ (mpya, mapya, vipya).
7. Mayai ...............................(hii, hili, haya) yamekaangwa na nani?
8. Jambazi ............................ (jenyewe, lenyewe, mwenyewe) limekamatwa.
9. Dirisha hili ...............................(ndogo, kadogo, dogo) halitafunguliwa.
10. Mashindano ........................... (yao, yake, zake) yaliwanufaisha zaidi.

## ZOEZI LA 8:

***Kanusha sentensi zifuatazo*:**

**MFANO:**

- Gari kubwa litaelekea mashambani leo.
- Gari kubwa halitaelekea mashambani leo.

1. Magari makubwa yataelekea mjini Karongi leo.
2. Jino langu bovu liling'olewa jana.
3. Meno yangu mabovu yaling'olewa jana.
4. Kawa langu dogo limekifunika chungu chako kikubwa.
5. Makawa yangu madogo yamevifunika vyungu vyenu vikubwa.
6. Jitu lile baya linampiga mtoto bila sababu.
7. Majitu yale mabaya yanawapiga watoto bila sababu.
8. Shati langu limechafuka.
9. Majina yao yaliandikwa upya.
10. Hili ni jambo linalotuhusu sisi.

### 5.4. Matumizi ya Lugha: Utambuzi wa Maana za maneno

## ZOEZI LA 9:

***Andika maana za maneno haya kwa kuchagua jibu kwenye kisanduku.***

| | | |
|---|---|---|
| mazoezi | uhodari | kujenga mwili |
| riadha | kustarehe | uhusiano |

1. burudika
2. hali ya kuwa na fungamano na
3. michezo inayohusisha viungo vya mwili ikiwemo kukimbia na kurusha mshale
4. ujasiri
5. kuimarisha
6. tendo linalofanywa na mtu ili kuwa na uwezo juu ya jambo fulani

**Maelezo muhimu kuhusu faida za michezo**

- Michezo inawasaidia watu tofauti kuishi bila magonjwa;
- Michezo hujenga miili ya binadamu na kuifanya iwe mikakamavu;
- Michezo hufurahisha;
- Michezo huchangamsha;
- Huongeza kiwango cha kufikiri na uwezo wa kutenda kazi kwa ufanisi;
- Michezo hujenga uhusiano mwema;
- Michezo hujenga urafiki;
- Michezo humletea mtu sifa nzuri na hata taifa lake;
- Michezo hunufaisha anayeicheza kwa kumletea pato kubwa kiasi cha kuwa tajiri.

Magonjwa yanayosababishwa na kutofanya mazoezi ya michezo ni kama vile kisukari, shinikizo la moyo, mfadhaiko, unene wa kupindukia, na kadhalika.

## 5.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

**ZOEZI LA 10:**

***Wewe ni mwanafunzi uliyealikwa katika warsha moja mjini Kigali kuhusu michezo na faida zake. Elezea wenzako kuhusu mambo muhimu yaliyozungumziwa kwenye warsha hiyo.***

## 5.6. Kuandika: Utungaji wa Kifungu cha Habari

**ZOEZI LA 11:**

***Tunga kifungu cha habari kuhusu "Hali ya Michezo ya wanawake Nchini Rwanda."***

# SOMO LA 6: MASHINDANO KATIKA MICHEZO

**Tazama mchoro ufuatao na kujibu maswali yanayofuata hapo chini yake.**




**ZOEZI LA 1:**

***Jadili mambo unayoyaona kwenye mchoro hapo juu.***

## 6.1. Kusoma na Ufahamu: Mchezo wa Kandanda

Soma kifungu kifuatacho kuhusu mchezo wa kandanda, halafu jibu maswali uliyopewa hapo chini.

Timu ya Gikondo ni timu maarufu katika mpira wa miguu. Inajulikana kwa uwezo wake wa kufunga magoli mengi kutokana na wachezaji wake hodari. Wiki jana, timu hii ilishindana na timu ya Gicumbi. Mpira ulimalizika kwa timu ya Gikondo kushinda mabao matatu kwa sifuri.

Mpira ulipoanza, timu zote zilianza kucheza kwa tahadhari kwa dakika za mwanzo. Katika kipindi cha kwanza, wachezaji wa timu ya Gikondo walikuwa wanaonyesha uhodari wao wa kawaida wa kupiga mashuti makali na kupiga chenga tofauti na ilikuwa hivyo kwa wachezaji wa timu ya Gicumbi. Watazamaji wa mpira walikuwa wanashangilia kwa furaha wakipiga kelele, “Kalisa mpira ni wako, mvishe kanzu mtoto huyo, mpige chenga kama tatu,weee! Hamkusomea shule moja... Endelea pale!!!”

Baada ya dakika kumi tu toka mpira kuanza, wachezaji wa Timu ya Gikondo walipasiana mpira kwa pasi za haraka haraka mpaka katika lango la timu ya Gicumbi. Papo hapo sauti kali ilipigwa, vigelegele na vikengele vingi vilisikika kusherehekea goli maridadi. Timu ya Gikondo ilishangiliwa kwa kufunga goli la kwanza. "Gikondo, oye oye, oye! Magoli yako yaanze kumiminika kama maji ya mvua. Oyee, oyee shinda tu, ushindi ni wako!!!" Watazamaji walishangilia.

Mimi nilikuwa hapo uwanjani nikichunguza yaliyokuwa yakitendeka. Baada ya goli hilo la kwanza, punde si punde, nilimwona mchezaji Karake akishika mpira na kuandika goli la pili kwa kichwa maridadi. Nami nilijiunga na watazamaji tukashangilia timu ile kutokana na uhodari wa wachezaji wake. Mpira uliendelea kuwa mkali kati ya timu mbili. Wachezaji kwa upande wa Gicumbi walionekana kutumia nguvu zaidi. Wao walijaribu kupiga mashuti makubwa katika lango la timu ya Gikondo lakini mlinda mlango wa timu ya Gikondo alikuwa hodari sana. Kuna wakati aliweza kuudaka mpira ambao ulikuwa na kasi sana na hivyo kuikosesha goli la wazi kabisa timu ya Gicumbi. Mashabiki wa Gicumbi wote walikuwa wamekosa goli lililokuwa limehesabiwa na mashabiki wengi. Mchezo uliendelea mpaka ulipotoka nje.

Wakati huo wachezaji wa timu ya Gikondo walitakiwa kuurudisha kiwanjani. Mpenzi ndiye alienda kuurudisha mpira kiwanjani. Yeye aliutupia Kalisa ambaye alipiga chenga moja nzuri. Wakati alipotaka kupiga chenga nyingine mchezaji wa Gicumbi aliunawa mpira. Hivyo basi, mpira ulipelekwa mbele ya mlango wa timu ya Gicumbi. Shuti kubwa lilipigwa na Kamoso na mara hiyo sauti nyingi zilisikika zikishangilia goli la tatu la timu ya Gikondo. Ni katika dakika hizo, wachezaji walipewa dakika za mapumziko kwa kuwa kipindi cha kwanza cha mpira kilikuwa kimemalizika.

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi kwa wachezaji wa timu zote. Kila upande ulikuwa unataka kupata goli la haraka. Katika muda mfupi, ilibainika kuwa wachezaji wa timu ya Gicumbi walikuwa wameanza kuishiwa nguvu na hivyo kuonekana kuwa wadhaifu. Kocha wa timu ya Gicumbi alifanya mabadiliko ya kuwatoa wachezaji watatu waliokuwa wamechoka. Baada ya mabadiliko hayo, timu ya Gicumbi ilipata uhai tena. Ijapokuwa timu zote ziliendelea kushambuliana kwa zamu. Katika dakika za mwisho, mchezo ulikuwa upande wa timu ya Gikondo kwani wachezaji wa Gikondo walicheza pasi fupifupi za uhakika zilizowafanya waumiliki mpira.

Zaidi ya hivyo, wachezaji wa Gikondo walipata furasa ya kupiga mashuti makali katika lango la Gicumbi. Kila aliyekuwepo uwanjani alijiuliza kwa nini hawakufanya hivi toka mwanzoni? Jitihada hizi za kutafuta goli jingine hazikufanikiwa kwa kuwa muda ulikuwa umeyoyoma.

Baada ya dakika chache, mwamuzi alipiga kipenga kuashiria kumalizika kwa mchezo. Timu ya Gikondo iliibuka mshindi kwa kupata mabao matatu kwa

sifuri. Kila timu na mashabiki wake walirudi makwao. Mashabiki wa timu ya Gikondo walirudi na furaha tele ya ushindi huku wakiimba nyimbo nyingi za kuisifu timu yao kwa ushindi. Nao mashabiki wa timu ya Gicumbi walirudi makwao wakiwa na huzuni huku wakijifariji kwa kusema, "Asiyekubali kushindwa si mshindani."

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Taja majina ya wachezaji mashuhuri waliozungumziwa katika kifungu cha habari. Eleza sifa za kila mchezaji kati ya hao.
2. Timu ipi ilionyesha uhodari zaidi kati ya timu zinazozungumziwa katika kifungu hiki cha habari? Eleza jibu lako.
3. Taja makosa yaliyofanywa katika mchezo huo na wachezaji waliofanya makosa hayo.
4. Kwa nini wachezaji wa timu ya Gicumbi walionekana kuwa dhaifu katika kipindi cha pili?
5. Matokeo ya mchezo yalikuwa yapi?
6. Timu ya Gikondo ilikuwa inajulikana kwa jina lipi?
7. Eleza sababu ya timu ya Gikondo kupewa jina hilo.
8. Mabao ya timu ya Gikondo yaliingia katika kipindi cha ngapi cha mchezo?
9. Ni mchezaji yupi aliyeshinda bao kwa kutumia kichwa?
10. "Asiye kubali kushindwa si mshindani", eleza.

## 6.2. Msamiati kuhusu Mchezo wa Kandanda

### ZOEZI LA 2:

***oanisha maneno yafuatao na maana zake.***

| Maneno | Maelezo |
|---|---|
| 1. Mlinda mlango | a. Refarii |
| 2. Kudaka mpira | b. -enye kujulikana kila mahali. |
| 3. Shamrashamra | c. Kundi hodari la watu wanaohusika na mchezo fulani. |
| 4.Mwamuzi | d. Mchezaji anayezuia magoli ya timu shindani kuingia. |
| 5. Maarufu | e. Kuwa na afya mbaya kutokana na maradhi. |
| 6. Ushindi | f. Shangwe |
| 7. Kudhoofika | g. Kunyaka mpira kwa mikono. |
| 8. Timu bingwa | h. Hali ya kushinda. |

## ZOEZI LA 3:

***Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia msamiati unaofaa kati ya huu mliopewa: penalti, mlinda mlango, kocha, hodari, mwamuzi, ushindi.***

1. Mchezaji mmoja alimuumiza mchezaji wa timu pinzani ndani ya eneo lake la hatari. Hii sasa ni...................

2. Mchezo umemalizika na timu yangu imepata..............................wa magoli matatu kwa bila.

3. .........................................anaongoza timu na kutoa maelekezo kwa wachezaji wake namna ya kucheza ili wapate ushindi.

4. Mutesi ni .............................mzuri sana. Yeye analinda vizuri lango la timu yake.

5. Sasa hivi ni dakika ya tisini ya mchezo, .........................anamaliza mpira.

6. Kalisa ni mchezaji.................................................sana.

## 6.3. Sarufi: Matumizi ya Vivumishi vya Kuuliza, vya Idadi na vya Sifa

**Maelezo muhimu**

Katika matumizi ya majina ya ngeli ya Li-Ya- na vivumishi vya idadi, tarakimu **mbili** hugeuka **-wili.** Tarakimu **tatu, nne, tano, nane** huchukua kiambishi **ma-** katika wingi.Vivumishi hivyo huwa **mawili, matatu, manne, matano** na **manane.** Lakini tarakimu **sita, saba, tisa** na **kumi** hazibadiliki.

**MATUMIZI YA VIVUMISHI VYA KUULIZA, VYA IDADI NA VYA SIFA**

**1. Vivumishi vya kuuliza**

| UMOJA | WINGI |
|---|---|
| Jukwaa **lipi** tutaonyeshea mchezo? | Majukwaa **yapi** tutaonyeshea michezo? |
| Juma **lipi** tutapumzika? | Majuma **yapi** tutapumzika? |

## 2. Vivumishi vya idadi

| UMOJA | WINGI |
|---|---|
| Dirisha **moja** limefunguliwa. | Madirisha **mawili** yamefunguliwa. |
| | Madirisha **matatu** yamefunguliwa. |
| | Madirisha **manne** yamefunguliwa. |
| | Madirisha **matano** yamefunguliwa. |
| | Madirisha **sita** yamefunguliwa. |
| | Madirisha **kumi** yamefunguliwa. |
| | Madirisha **mengi** yamefunguliwa. |
| | Madirisha **machache** yamefunguliwa. |

## 3. Vivumishi vya sifa

| UMOJA | WINGI |
|---|---|
| Kabati zuri limevunjwa. | Makabati **mazuri** yamevunjwa. |
| Jengo **refu** limeanguka. | Majengo **marefu** yameanguka. |
| Kasha **kubwa** limeletwa. | Makasha **makubwa** yameletwa. |

### ZOEZI LA 4:

***Chagueni neno moja kutoka mabano na kuliandika katika nafasi tupu.***

1. Makoti……………..........yamefuliwa? (mepi, wepi, mepi, yapi)
2. Madarasa................yamesafishwa leo.(mbili, mawili, chache, tatu)
3. Daftari............................. ni la Kiswahili?(ipi,zipi,nani,lipi)
4. Wanafunzi wengi hawapendi mazoezi........................(mingi, mengi, chache, zingi)
5. Jibu .................................... linafurahisha. (lizuri, zuri, nzuri, mazuri)
6. Mabao ...................................... yaliingia katika lango lao. (tatu, vitatu, matatu, kitatu)
7. Jengo ..........................................lilianguka jana. (penyewe, kenyewe, lenyewe, mwenyewe)
8. Kabati ........................................ liliagizwa? (yapi, kapi, lipi, ipi)
9. Maswali ........................................yalikuwa mengi. (yake, lake, mwake, kake)
10. Dirisha kubwa ............................... . (yalifungwa, kufunga, wafungwa, lilifungwa)

## 6.4. Matumizi ya Lugha: Upangaji wa Maneno katika Sentensi na Miktadha ya Matumizi.

**ZOEZI LA 5:**

***Panga maneno haya katika sentensi ili yalete maana kamili.***

1. haraka haraka/wanapasiana/wachezaji/ walikuwa/mpira/wake.

2.Rubavu/kwa/ilishinda/timu/timu/Bugesera/sufuri/magoli/ya/ya/matatu.

3. linazungumziwa/hizi/michezo/suala/mno/la/siku/shuleni.

4.ngeli/ya/umoja/wanatumia/katika/majina/na/wanafunzi/li-ya-/wingi/ya.

5. mimea/haya/ni/tuliyoipanda/ya/matokeo.

**ZOEZI LA 6:**

***Tumia maneno haya ya muktadha wa mashindano kuunda sentensi zako mwenyewe.***

1. kushangiliwa
2. mashabiki
3. furaha tele
4. kipindi cha kwanza
5. kupasiana mpira
6. kuandika goli

## 6.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

**ZOEZI LA 7:**

***Zungumzia wenzako kuhusu umuhimu wa michezo kwa wanafunzi.***

## 6.6. Kuandika: Utungaji wa Kifungu kuhusu Matukio ya Mchezo

**ZOEZI LA 8:**

***Katika aya nne, andika kifungu cha habari huku ukielezea matukio yaliyojitokeza katika mmojawapo ya michezo uliyoitazama.***

## TATHMINI KUHUSU MADA YA PILI

I. Chagua neno sahihi kati ya yale yaliyotolewa katika parandesi kwa kukamilisha sentensi zifuatazo:

..........................................ya kisiasa yanaendelea kufundishwa katika jiji la Kigali kufuatana na uongozi bora (masomo, maadili, matawi, majengo).

Mwelekeo wa Rwanda hadi kufikia mwaka 2040 utaifikisha Rwanda kwenye ........................la juu la kiuchumi (madhara, maendeleo, daraja, mapengo).

Katika...........................ya ligi kuu ya soka nchini Rwanda, timu zote zilizocheza jana zilitoka sare. (mchezo, kombe, mashindano, mpira).

Mwaka jana, nilikuwa hodari wa kupiga……………………….. uwanjani lakini nimeanza kuzeeka. (chenga, masomo, daraja, mashindano)

II. Eleza faida zinazopatikana katika michezo kwa kulinganisha mchezo wa kandanda na mchezo wa kikapu.

III. Tunga kifungu cha habari kuhusu michezo ukitumia maneno yafuatayo ambayo hutumiwa katika uwanja wa michezo. Hakikisha pia kwamba umetumia maneno walau manne ya ngeli ya li-ya kwa kupiga mstari chini yake.

Kuvisha kanzu
Mpira kuwa mwingi
Kukata mbuga
Kuunawa mpira
Harusi
Refa
Kutoa bomba
Kukokota ngoma
Mpira kuambaamba nje
Kuotea
Kuunyaka mpira
Washika vibendera

# MADA KUU YA 3

## UHAKIKI WA HADITHI ZA MASIMULIZI KATIKA KISWAHILI

# MADA KUU YA 3: UHAKIKI WA HADITHI ZA MASIMULIZI KATIKA KISWAHILI

## MADA NDOGO: Muhtasari, fani na maudhui

**Uwezo Upatikanao katika Mada:** Kuelewa na kufuata mtindo wa kuandika muhtasari wa hadithi aliyoisikiliza au kuisoma; kuchambua hadithi za Kiswahili kwa kuzingatia fani na maudhui yanayojitokeza katika hadithi; kusimulia hadithi rahisi za masimulizi; kujua mabadiliko ya kisarufi katika matumizi ya majina ya ngeli ya PA-M-KU-

**Malengo ya Ujifunzaji:**

**Baada ya mafunzo ya mada hii, mwanafunzi atakuwa na uwezo wa:**

- Kuchambua hadithi mbalimbali za Kiswahili kutokana na ujuzi wa uchambuzi aliopata.
- Kutoa tathmini ya hadithi aliyochambua kulingana na mtindo maalum wa uhakiki aliofuata.
- Kusimulia tena hadithi aliyowahi kusimuliwa au kuisoma.
- Kuandika muhtasari wa hadithi aliyoisoma au kuisikiliza.
- Kutunga na kusahihisha sentensi sahihi kwa kuzingatia matumizi ya majina ya ngeli ya PA-M-KU-.

### Kazi Tangulizi

1. Unajua nini kuhusu muhtasari?
2. Nini umuhimu wa muhtasari?
3. Nini maana ya fani na maudhui?
4. Ni mambo gani muhimu yanayozingatiwa katika kufafanua fani na maudhui?

## SOMO LA 7: MUHTASARI



**ZOEZI LA 1:**

***Tazama kwa makini mchoro hapo juu, baadaye uzungumzie unayoyaona.***

### 7.1. Kusoma na Ufahamu: Mhunzi Tulia

Soma kifungu cha habari kinachofuata, kisha jibu maswali ya ufahamu uliyopewa hapo chini

Zamani za kale palikuwa na mtu ambaye jina lake ni Tulia. Tulia alikuwa mhunzi mashuhuri aliyetia fora nchini. Aidha,alikuwa pia akimtengenezea Mfalme vitu vingi vizuri.

Siku moja asubuhi, Mfalme alimwita. Tulia alienda kwenye kasri la Mfalme kwa shauku. Alipofika mahali hapo, Tulia alimwangalia Mfalme, akataka kumwuliza swali lakini akasita. Halafu Mfalme akasema, “Tulia, wewe ni mhunzi mzuri sana. Umenitengenezea vitu vingi. Hakuna mhunzi aliye bora kuliko wewe. Ninataka unitengenezee mtu mwenye uhai aliye na uwezo wa kuzungumza na kutembea. Ninakupa wiki mbili utimize kazi hiyo.”

Tulia hakuamini masikio yake. Alijibu kwa sauti ya kutetemeka na kusema, “Sultani mheshimiwa, ingawa nina maarifa mengi katika kazi yangu, siwezi kamwe kutengeneza mtu aliye na uhai.” Mfalme aliposikia hayo, alikasirika sana, macho yake makubwa yakawa mekundu. Akamwamuru Tulia aondoke mara moja na asizidi tena kuuliza maswali. Tulia aliondoka akiwa na huzuni tele kwa sababu hakujua la kufanya.

Alirudi nyumbani akalala kitandani pake na akiwaza kwa makini. Baadaye, aliamua kurudi kwa Mfalme amwarifu kwamba ilikuwa vigumu kutengeneza mtu aliye na uhai.

Asubuhi na mapema, yaani kesho yake, Tulia alirudi pahali walipokutania na Mfalme siku iliyotangulia. Mfalme aliposikia kwamba Tulia amewasili aliuliza ikiwa kazi aliyopewa ilikuwa tayari. Tulia alikariri kuwa ilikuwa vigumu kabisa kutengeneza mtu aliye na uhai. Mfalme akajibu kwa hasira, "ikiwa hutakamilisha kazi niliyokupa kwa muda wa wiki mbili utapewa adhabu kali."

Tulia, mara hii tena, aliondoka akiwa na huzuni nyingi na wasiwasi. Alipofika kwake alishikwa na kizunguzungu, akaamua kukaa chini. Aliweka kichwa chake katikati ya miguu yake na machozi yakatiririka mashavuni mwake kama mvua. Papo hapo kukatokea mwendawazimu akamwona Tulia, akasimama. "U hali gani mwenzangu mhunzi mashuhuri?" Mwendawazimu alipiga kelele. "Ala! Kwa nini huna raha? Nimekufanyia nini kibaya hata hunijibu ninapokusalimu?" Alilalamika. Tulia naye akajibu, "Hun! Ndugu yangu ninasikitika sana.... nimekwisha kufa mie ingawa sijaingia kaburini. Mfalme ameniambia nifanye kitu kisichowezekana. Alinitaka nimtengenezee mtu mzima aliye na uwezo wa kuzungumza na kutembea, ama sivyo ataniadhibu vikali."

Mwendawazimu yule alianza kucheka "Hehehe! Kwa nini watu hujifikiria kuwa na akili nyingi? Mwendawazimu ndiye anayeweza kutengeneza mtu mwenye uhai." Tulia alimsikiliza kwa makini halafu mtu yule mwenye kichaa akasema, "Tulia we! Nenda kwake Mfalme ukamwambie atoe mitungi mia moja ya machozi ya watu na magunia mia moja ya jivu la nywele za watu. Mwambie hivyo ndivyo vinavyotumiwa kwa kutengeneza mtu. Ni hayo tu, sasa nenda kwake."

Tulia kana kwamba alikuwa ametoka ndotoni alimsifu sana mwendawazimu yule na akaenda moja kwa moja hadi kwake Mfalme. Alimwarifu Mfalme juu ya mahitaji ya kutekeleza kazi yake. Mfalme akawaita watumwa wake wote na kuwaamuru waende kote nchini wakawaambie watu wakusanye machozi yao. Watu wa matabaka yote walianza vilio lakini hawakuweza kujaza hata mtungi mmoja wa machozi. Wakanyolewa nywele zao, lakini, lo! Hawakuweza kukusanya hata gunia moja la jivu la nywele hizo.

Wiki moja baadaye, Tulia alikwenda kwa Mfalme na kutaka kuchukua vifaa vya kazi aliyopewa lakini hakuweza kupata hata gunia moja la jivu lile wala mtungi mmoja wa machozi yale ya watu. Papo hapo watu wengi walikuwa wakija kumwelezea Mfalme kwamba aliloliomba halingewezekana. Walimwambia jinsi walivyofanya juhudi ya kupata machozi lakini wakashindwa kujaza hata nusu mtungi. Vilevile, waliojitahidi kupata jivu la nywele nao walikuwa

wakilalamika kwamba hilo lilikuwa jambo lisilowezekana.

Mfalme aliposikia hayo, alimhurumia Tulia kwa kumpa ombi lisilowezekana. Aliamua kumkabidhi vitu vingi vya thamani kwa heshima ya vitu vingi alivyokuwa amemtengenezea mpaka wakati huo. Tulia naye alimshukuru Mfalme kwa uamuzi mzuri alioufanya, kisha akarudi nyumbani.
Huu ndio mwisho wa hadithi.

Co-Publishing Committee, Hadithi za kwetu

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Hadithi hii ina wahusika wangapi? Wataje.
2. Tulia alikuwa anajishughulisha na kazi gani?
3. Mfalme alipomwita Tulia alimuamrisha kumfanyia nini?
4. Je, Tulia alikubali kutekeleza amri ya Mfalme?
5. Je, Tulia alijihisi vipi alipofika nyumbani kutoka kwa Mfalme?
6. Ni nani aliyemtembelea Tulia alipokuwa katika hali mbaya nyumbani kwake?
7. Tulia aliposema “Nimekwisha kufa mie ingawa sijaingia kaburini”, alikuwa anamaanisha nini?
8. Mwendawazimu alimshauri Tulia kufanya nini?
9. Je, Tulia alifuata mawaidha ya Mwendawazimu?
10. Je, tatizo lililokuwa kati ya Tulia na Mfalme lilitatuliwa? Eleza jibu lako.

## 7.2. Msamiati Kuhusu Kifungu

### ZOEZI LA 2:

***Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu, kisha uyatumie katika sentensi fupi zenye maana katika maneno yako:***

1. mhunzi
2. kutia fora
3. mfalme
4. maskani
5. kuamini
6. sultani
7. kutetemeka
8. kichaa
9. kuwasili
10. hasira
11. kizunguzungu
12. mtungi
13. jivu
14. kuabudu
15. sala

### ZOEZI LA 3:

***Oanisha maneno yaliyotumiwa katika kundi A na maelezo yake katika kundi B.***

| A | B |
|---|---|
| 1. Uhai | A. Kuwa katika hali ya utulivu. |
| 2. Zamani | B. Halafu. |
| 3. Tulia | C. Uzima. |
| 4. Kusita | D. Nyama ya juu iliyoko kwenye sehemu ya kulia na kushoto ya uso inayoanzia chini ya jicho mpaka karibu ya taya. |
| 5. Baadaye | E. Hali ya utulivu na tafakuri. |
| 6. Makini | F. Kitambo cha miaka mingi iliyopita. |
| 7.Shavu/ mashavu | G. Acha kufanya jambo baada ya kutia nia ya kulifanya au baada ya kulianza. |

## 7.3. Sarufi: Majina ya Ngeli ya Pa- na vivumishi vyake

- Alipofika pahali **papo** Tulia alimwangalia Mfalme.
- Mjini Kigali **pana** magari mengi.
- Kichwani **pangu pana** chawa.
- Mahali hapa ni **pachafu.**
- Musanze humu mna mahali **pazuri** pa kutembelea.

## ZOEZI LA 4:

***Maneno ambayo yameandikwa kwa rangi iliyokolea yanapatikana katika ngeli ipi ya majina?***

**Maelezo muhimu:**

Ngeli hii ndiyo ngeli ya kipekee ambayo ina majina mawili. Majina hayo ni *mahali* na *pahali.* Hata hivyo, ipo tofauti kati ya ***mahali*** na ***pahali.*** *Mahali* ni eneo kubwa ambalo halijulikani mipaka yake maalumu, lakini *pahali* ni eneo dogo ambalo linajulikana.

Neno **mahali** na **pahali** ni majina yanayowekwa katika ngeli ya majina iitwayo PA- M- KU. Vivumishi vya sifa ambatana huanzwa na Pa- kama ifuatavyo:

- Pahali **pakavu pa**melimwa.
- Mahali **parefu pa**mepandwa.
- Mahali **patakatifu pa**mependeza.
- Mahali **papana pa**mepandwa miti ya matunda**.**
- Mahali **pangu pa**naonekana kwa urahisi.
- Mahali **pazuri pa**mejengwa nyumba za watalii.
- Mahali **padogo pa**naingiwa na watu wachache.

**Tanbihi:** Kiswahili sanifu hakiruhusu matumizi ya pa- kwenye kivumishi cha sifa safi.

Kwa hiyo hatusemi wala hatuandiki mahali ***pasafi.*** Usanifishaji wake ni mahali **safi.**

### 1. Vivumishi vya kuonyesha

**MIFANO:**

- Pahali **hapa** palifyekwa.
- Mahali **hapo** palifyekwa.
- Pahali **pale** palifyekwa

### 2. Vivumishi vya kumiliki

| UMOJA | WINGI |
|---|---|
| Pahali **pangu** pamesafishwa. | Pahali **petu** pamesafishwa. |
| Pahali **pako** pamesafishwa. | Pahali **penu** pamesafishwa. |
| Pahali **pake** pamesafishwa. | Pahali **pao** pamesafishwa. |

**3. Vivumishi vya kuuliza**

**MFANO:**

- Mahali **papi** panapendeza?
- Pahali **papi** panaonekana?
- Mahali **papi** ni pa kutembelea?

**4. Vivumishi vya idadi**

| UMOJA | WINGI |
|---|---|
| Pahali **pamoja** panaeleweka. | Pahali **pawili** panaeleweka.<br>Pahali **patatu** panaeleweka.<br>Pahali **panne** panaeleweka.<br>Pahali **patano** panaeleweka.<br>Pahali **sita** panaeleweka.<br>Pahali **pengi** panaeleweka. |

**5. Vivumishi vya Sifa**

**MIFANO:**

- Pahali **pachafu** pamefagiliwa.
- Mahali **pazuri** panastahili kutembelewa.
- Pahali **pachafu** pamebomolewa.

**ZOEZI LA 5:**

***Sahihisha sentensi zifuatazo kwa kuzingatia matumizi bora ya vivumishi.***

1. Mahali yake inapendeza.
2. Nimetembea pahali mbaya yasipo na mazingira bora.
3. Ziwani Kivu kuna pahali kwingi ha kutembelea.
4. Nilimkuta katika baa, mahali kubaya sana.
5. Mukamana hapendi kukaa mahali mchafu.
6. Waislamu wana pahali kao kwa kusalia.

**ZOEZI LA 6:**

***Chagua jibu sahihi kati ya yale ambayo yamewekwa katika mabano.***

1. Wanafunzi walipofika Huye walisema kuwa ni pahali ……. (kuzuri, pazuri, mzuri).

2. Nilimkuta mahali ……………. ( pasafi, safi, kusafi).

3. Mateso alikuwa pahali …………… (mbaya, kubaya, habaya, pabaya).

4. Mahali …………. (mchafu, chafu, pachafu, kuchafu) panaweza kuambukiza maradhi.

5. Pahali …………… (patakatifu, takatifu, kutakatifu) hutua Wakristo wengi sana.

6. Alichezea mahali .......................... (kavu, makavu, kukavu, pakavu) akaumia kidole cha mguu.

7. Musanze ni pahali .......................... (kumoja, kamoja, pamoja, moja) pa kusafiria.

8. Si vizuri kutembelea mahali.......................... (menye, kwenye, penye, yenye) giza jingi wakati wa usiku.

## 7.4. Matumizi ya Lugha: Sifa za Muhtasari

**ZOEZI LA 7:**

***Soma kifungu cha habari "Mhunzi Tulia" hapo juu na baadaye utoe muhtasari kimazungumzo.***

**ZOEZI LA 8:**

1. Kwa maoni yako muhtasari ni nini?
2. Muhtasari mzuri unapaswa kuwa na sifa gani?

**Maelezo muhimu kuhusu muhtasari**

- Muhtasari au ufupisho wa habari ni ustadi au ufundi wa kuisoma habari, kuielewa vizuri (yaani kuifahamu) na kuweza kuieleza au kuiandika upya kwa ufupi au kwa maneno machache ukiyalinganisha na yale ya awali lakini bila kupotosha ujumbe wa habari asili au habari ya kwanza. Mbinu hii inamwezesha mtu kufikiri katika lugha husika na kupima

ufahamu wake na uwezo wake wa kujieleza kwa maneno machache yake mwenyewe lakini ujumbe wote ukatolewa kwa kutumia maneno hayo.

- Kwa upande mwingine, muhtasari ni kazi ya kuandika habari kwa ufupi. Ili kuelewa habari ni lazima kuisoma mara mbili au tatu. Baada ya kupata mawazo makuu, ndipo unapotoa muhtasari kwa theluthi moja hivi. Katika kuandika muhtasari wa habari ni lazima kutumia maneno yako mwenyewe, hakuna haja ya kuiga lugha ya mwandishi. Hivi unapaswa kueleza kwa kifupi kwa maneno yako mwenyewe. Katika kufanya hivyo kuna haja ya kutazama mambo yanayorudiwarudiwa na mwandishi na kuyafupisha.
- Ili kuweza kuielewa habari, ni lazima kuisoma habari hii zaidi ya mara moja. Mara mbili au tatu inatosha. Zingatia mawazo makuu na uyaandike. Baada ya hapo jiulize kama mambo yote ya maana yaliyokusudiwa na makala au habari ya awali yamebaki. Pia hakikisha kuwa ufupisho wako una urari au mfuatano mzuri wa mawazo.

Lugha nyingi za kibantu na nyinginezo huwa na misemo na methali. Misemo na methali ni mfano mmoja mzuri sana wa kazi ya muhtasari.

**Sifa za Muhtasari Mzuri**

1. Muhtasari unapaswa kuwa na mawazo makuu yanayoeleweka.
2. Muhtasari mzuri unapaswa kuwa theluthi moja ya kazi yote.
3. Lugha inayotumiwa ni lazima iwe lugha ya mkato (matumizi ya nahau na methali).
4. Muhtasari unaweza kuwa katika aya moja au nyingi.
5. Muhtasari mzuri unapaswa kumwezesha msikilizaji au msomaji kupanua msamiati.
6. Muhtasari mzuri lazima uwe bunifu (yaani matumizi ya maneno yako mwenyewe).

Badala ya mtu kutoa maelezo marefu kama: Bwana Mkubwa alimwamini pombe kali, mtu mlevi, amlindie mtungi wake, uliojaa pombe uliokuwa ndani ya nyumba, kwa hiyo akawa amemwacha humo."

Habari hii kwa ufupisho, mtu anaweza kuieleza kwa namna mbalimbali. Namna moja ingeweza kuwa: " Bwana mkubwa amemweka mlevi nyumbani ili amlindie pombe."

Katika mfano mwingine, mtu anaweza kutoa maelezo yafuatayo: "Watu wote ni sawa kwa maumbile lakini kila mmoja katika maisha huwa na bahati yake" au "watoto wa familia moja huweza kulelewa sawa sawa na wazazi

wao, lakini kila mmoja huweza kuwa na lengo lake tofauti na wengine." Mtu anaweza kutoa muhtasari wa maelezo hayo marefu kwa kutumia methali; " Wana huchangia sahani hawachangii bahati." Pia, " Wana huchangia titi hawachangii bahati."

### 7.5. Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

**ZOEZI LA 9:**

***Kwa njia ya mazungumzo, eleza uhusiano uliopo kati ya kichwa cha habari "Mhunzi Tulia" na mambo yaliyozungumziwa katika kifungu cha habari ulichosoma.***

### 7.6. Kuandika: Uandishi wa Muhtasari

**ZOEZI LA 10:**

***Andika muhtasari wa hadithi "Mhunzi Tulia" ukizingatia sifa za muhtasari mzuri.***

## SOMO LA 8: FANI KATIKA HADITHI SIMULIZI



**ZOEZI LA 1:**

***Zungumzia mchoro hapo juu na vitendo vinavyofanyika.***

### 8.1. Kusoma na Ufahamu: Kobe na Nyani

Soma hadithi inayofuata kuhusu Kobe na Nyani, kisha jibu maswali yaliyopo hapo chini.

Kobe na Nyani waliolewa katika kijiji kimoja. Kijijini humo mlikuwa na mashamba tele ya miti. Nyani alikuwa na shughuli ya kukata miti katika shamba lake. Alimwomba Kobe amsaidie ili shamba lisafishwe upesi kuwahi majira ya kilimo. Kobe aliitikia wito na siku waliyopatana ilipowadia, wote walikuwa katika shamba la Nyani wakiwa na mashoka yao.

Kazi ilipamba moto shambani humo. Upande aliosimama mzee Kobe, miti ilianguka kama mchezo tu. Upande wa Nyani haukuonyesha maendeleo makubwa.

Nyani alianza kulalamika, “Mzee Kobe, naona leo shoka langu linarudisha nyuma juhudi yangu. Nililinoa karibu asubuhi yote ya jana lakini bado linaonekana kuwa ni butu.”

Mzee Kobe akasema, “Kama ni hivyo, ngoja nikuazime langu, maana mimi nipo karibu kumaliza sehemu hii uliyonipimia. Nitajikokota na shoka lako butu.” Basi jamaa hao wawili walibadilishana mashoka. Nyani alikata miti kwa shoka la Kobe sasa. Miti ililazwa pasipo kifani. Nyani alilipenda shoka lile na mwisho wa kazi yao alimwambia mzee Kobe, “Mzee Kobe, shoka hili ni kali na jepesi sana katika kukata miti. Kwa sifa hizo, ninaomba uniazime ili kesho nitakapokwenda kukata miti katika shamba la mkwe wangu nilitumie. Maana bila ya hivyo nitaonekana mvivu.”

Mzee Kobe alimruhusu Nyani abaki na shoka lake, lakini kwa sharti kwamba lazima alirudishe mara akimaliza kazi yake. Baada ya hapo walikula chakula ambacho kililetwa na mke wa Nyani. Walikaa ndani nyumbani mwa Bwana Nyani, wakaagana na kila mmoja akaelekea kwake.

Baada ya siku ile, siku nyingi zilipita bila ya Nyani kuonyesha dalili yoyote ya kurudisha shoka la mzee Kobe. Siku moja, Kobe aliamua kwenda nyumbani kwake. Alipofika kule, Nyani alimkaribisha Kobe harakaharaka.

“Rafiki yangu mpenzi, karibu sana nyumbani humu, najua shida iliyokuleta hapa. Kaa kitako tulegeze makoo kwa pombe kidogo ambayo alitengeneza mke wangu.”

Mzee Kobe alihisi kwamba kulikuwa na njama ya aina fulani. Baada ya kunywa pombe hiyo kidogo, Bwana Nyani alitoa kauli ifuatayo: “Rafiki yangu Kobe, ninasikitika kukuarifu kwamba shoka lako lile hutalipata tena. Nilimwazima mjomba naye kaniarifu kuwa hivi majuzi tu mwizi aliivamia nyumba yake akaliiba. Kwa hayo yote nasema pole sana.”

Mzee Kobe hakutoa kauli yoyote. Aliondoka akarudi zake nyumbani. Siku nyingi zilipita na habari za shoka zilikwisha kusahaulika. Siku moja Kobe alimwita mkewe akamweleza: “Mke wangu, unikatekate katika vipande

vipande halafu nyama yangu iwe kitoweo kizuri kabisa. Baada ya hapo pika chakula halafu ukakiweke katika njia panda. Hakikisha unafanya hivyo wakati Nyani yumo shambani mwake."

Mkewe hakukubaliana na mawazo yake; lakini Kobe alisisitiza na alimwondoa hofu kwamba kitendo kile hakingekuwa na madhara.

Baada ya mabishano makali, mkewe Kobe alifanya kama alivyoelekezwa na mumewe. Alimkatakata mumewe vipande. Nyama yake akaikaanga vizuri sana. Akatengeneza wali. Chakula kilipokuwa tayari, alikifunika na kukipeleka njia panda karibu na shamba la Nyani. Bahati njema Nyani alikuwemo shambani mwake siku ile. Alikuwa amekwisha kufanya kazi kwa muda mrefu na sasa alihisi ana njaa. Aliamua kuweka shoka lake begani na mara akaanza safari ya kurudi nyumbani.

Alipofika njia panda alianza kuhisi riha nzuri ya chakula. Mate yalianza kumdondoka Nyani, naye hakuchukua muda kugundua aliyekiweka pale. Bila kujiuliza aliyekwenda kukiweka pale, akaanza kukishambulia.

"Uhuru ruruu! Ngururuu! Ngururuu!"

Nyani alishangaa.

"He! Mambo gani tena haya! Badala ya kuwa ninapiga mbeu ya shibe, tumbo

linanguruma!"

Akiwa katika mshangao huo alisikia sauti kutoka tumboni mwake.

"Unashangaa nini! Usishangae. Mimi ninataka unirudishie shoka langu."

Nyani aliona mambo yamekuwa makubwa. Alianza kuharakisha kwenda

nyumbani.

Hofu ilimshika. Ilikuwa shani yenye kashifa ndani yake. Alijua wazi mzee Kobe alimcheza shere. Alikuwa amenuia kumwadhiri kwa kisasi cha kudhulumiwa shoka lake. Alipofika nyumbani alionekana kuwa na wasiwasi sana. Mkewe alimtayarishia chakula lakini hakuwa na hamu ya kula. Tumbo lilinguruma tena na sauti ilisikika kutoka tumboni, "Mimi sina ugomvi nawe. Ninataka shoka langu tu basi. Nenda kalitupe pale njia panda ulipokikuta chakula ulichokula.»

Nyani kusikia hivyo alikurupuka akaenda kuchukua shoka alipolificha na wakati huo alielekea njia panda. Alilitupa shoka la mzee Kobe pale. Kitambo kidogo baada ya hapo alijihisi ameshikwa na haja kubwa. Alichepuka kando

ili ajisaidie. Katika kujikamua alijihisi kama kulikuwa na kitu kigumu katika matumbo yake. Mwishoni alijisaidia mzee Kobe badala ya mavi. Nusura apasuke msamba. Mzee Kobe alipodondoka gamba lake likapasuka likawa na nyufanyufa. Kisha akachukua shoka lake. Mzee Kobe akaenda nyumbani taratibu kwa maumivu.

Mkewe Kobe alimpaka dawa akapona. Hata hivyo mistari hiyo ya kobe ipo hata leo.

Na huo ndio mwisho wa hadithi.

(*Kitabu cha Kiswahili IV-VA, Direction des Programmes de l'Enseignement Secondaire, juillet 1986*).

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Ni wahusika gani wanaozungumziwa katika hadithi hii?
2. Nyani alimfanyia hila gani Kobe?
3. Je, ni kweli kwamba shoka la Nyani lilikuwa butu? Eleza.
4. Shoka lililoazimwa Nyani lilirudishwa?
5. Kobe alipofika nyumbani kwa Nyani alipokelewa vipi?
6. Kobe alifanya nini ili kupata shoka lake?
7. Kutokana na kauli ya Nyani, shoka lenyewe lilipotea vipi?
8. Nyani alitatua vipi tatizo alilokuwa nalo kati yake na Kobe?
9. Je, tabia ya Nyani inakubalika katika jamii?
10. Umepata funzo gani kutokana na hadithi hii.
11. Unadhani ni nini athari ya ukataji wa miti?
12. Kulipa kisasi ni jambo zuri?

## 8.2. Msamiati kuhusu Kifungu

**ZOEZI LA 2:**

***Baada ya kusoma hadithi, chunguza maana ya msamiati ufuatao katika Kamusi Sanifu kisha uyatumie katika sentensi fupi zenye maana kamili.***

1. kujikokota
2. shoka butu
3. kulalamika
4. kukaa kitako
5. epesi
6. njama
7. mvivu
8. dalili
9. kutoa kauli
10. kitoweo
11. madhara
12. kusikitika

**ZOEZI LA 3:**

***Hapa umepewa maneno tofauti. Chagua maana zake kutoka maelezo uliyopewa hapo chini.***

1. kunguruma
2. hofu
3. shani
4. kashifa
5. mabishano
6. ugomvi
7. sherere

a. jambo lisababishalo kitisho ama woga.

b. ufunuaji au udhihirisho wa siri ya jambo la aibu.

c. kutoa sauti kubwa ya kutisha.

d. mzaha wa kumfanya mtu aonekane kuwa ni mjinga.

e. hali ya kugombana.

f. tukio la kustaajabisha.

g. kuhitilafiana katika utoaji wa mawazo au wakati wa kujadiliana.

## 8.3. Sarufi: Matumizi ya Majina ya Ngeli ya M- na Vivumishi Ambatana.

**ZOEZI LA 4:**

***Tazama maneno yanayopigiwa kistari kisha utaje aina zake.***

1. Rafiki yangu mpenzi, karibu sana nyumbani **humu**.
2. Kijijini **humo** mlikuwa na mashamba tele ya miti.
3. Kazi ilipamba moto shambani **humo**.
4. Mahali **mle** mna wanafunzi wangapi?

**Maelezo muhimu**

**MIFANO:**

- Mahali **mle** mna vumbi. (mbali)
- Lala chumbani **humu,** ni pazuri. (karibu)
- Hotelini **mle** mna huduma ya hali ya juu. (mbali)

Maneno **humu**, **humo**, **mle** yaliyotumiwa katika sentensi hapo juu ni vivumishi vya kuonyesha. Vimeambatana na maneno yenye dhana ya mahali au maeneo kama vile nyumbani, kijijini, mahali. Kundi la majina haya huunda majina ya ngeli ya M-.
Matumizi ya vivumishi hivi vya kuonyesha huchukua mofimu m- mwanzoni au mwishoni mwa neno.
Mofimu hii inaweza kutumiwa kwa kuonyesha vitu vilivyo mbali au karibu.

**MATUMIZI YA MAJINA YA NGELI YA M- PAMOJA NA VIVUMISHI**

**1. Vivumishi vya kuonyesha**

**MIFANO:**

- Mahali **humu** mna jambazi.
- Mahali **humo** mna jambazi.
- Mahali **mle** mna jambazi.

**2. Vivumishi vya kumiliki**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Mahali **mwangu** mnatembelewa. | Mahali **mwetu** mnatembelewa. |
| Mahali **mwako** mnatembelewa. | Mahali **mwenu** mnatembelewa. |
| Mahali **mwake** mnatembelewa. | Mahali **mwao** mnatembelewa. |

### 3. Vivumishi vya Kuuliza

**MIFANO:**

- Mahali mupi mnapendeza?
- Darasani mupi ni safi?

### 4. Vivumishi vya kurejesha

**MIFANO:**

- Ziwani **mwenyewe** mna samaki.
- Darasani **mwenyewe** mna wanafunzi.
- Mahali **mwenyewe** mnafahamika sana.

### 5. Vivumishi vya Sifa

**MIFANO:**

- Mahali **mchafu** mmefagiliwa.
- Nyumbani **mpana** mnapendeza.

**ZOEZI LA 5:**

***Chagua jibu sahihi kati ya haya yaliyowekwa katika mabano na kuliandika katika nafasi zilizoachwa wazi.***

1. Darasani ..................... (petu, kwetu, mwetu, ketu) mnapendeza.

2. Nilikwenda kanisani mahali.........................(pazuri, mzuri, kazuri, kuzuri) palipokuwa mapadre.

3. Mahali …………..(humu, hapa, kule) mnapatikana mahitaji yote.

4. Nililazwa hospitalini, mahali.............................(ambako, ambamo, ambaye) mna vitanda vingi.

5. Nyumbani………...............(pale, mle, huku) mnaonekana uchafu.

6. Barabarani……..................(kule, humu, pale) mmewekwa debe za taka.

7. Alihukumiwa kifungo cha miaka mitano na akapelekwa gerezani, mahali ...................... (ambayo, ambako, ambamo) hataonana tena na marafiki zake.

8. Ni mahali .......................(papi, kupi, mupi) mnamopenda?

## 8.4. Matumizi ya Lugha: Fasihi

**ZOEZI LA 6:**

***Soma kifungu cha habari "Kobe na Nyani" kisha ujibu maswali yanayofuata:***

1. Wahusika katika hadithi hii ni wa aina gani?
2. Eleza tabia za kila mhusika.
3. Hadithi yenyewe ilitendeka lini na ilitokea wapi?

- Hadithi ni tanzu ya fasihi simulizi yenye fani au mtindo wa aina fulani ya kusimulia.
- Chunguza maelezo yafuatayo kuhusu fasihi:

Fasihi ni aina ya sanaa ambayo wasanii wake huonyesha ustadi wao katika kutumia maneno kisanaa ili kuwasilisha ujumbe wao kwa wasomaji/jamii iliyonuiwa. Hii ndiyo tofauti kubwa baina ya fasihi na sanaa nyingine kama uchoraji wa picha, uigizaji wa densi, utungaji au uimbaji wa ngoma au muziki, usukaji mikeka, uchongaji wa vinyango na kadhalika ambamo nguzo muhimu si lugha bali ni vifaa vitumikavyo.

Fasihi hugawanywa katika tanzu kuu mbili:

**Fasihi Simulizi:**

Fasihi simulizi ni sanaa ya maneno yenye uzuri, upya na ujumbe. Ni masimulizi ambayo kwa asili hayakuandikwa wala kunaswa katika vinasasauti. Fasihi simulizi ni masimulizi juu ya mambo ya kale na yenye misingi ya mila au tamaduni za jamii. Fasihi simulizi hutuonyesha tulikotoka na kueleza asili yetu ili tujivunie. Fasihi simulizi huwa na vipengele muhimu kama hadithi, methali, nahau, vitendawili, nyimbo na mashairi.

**Hadithi**: Ni habari za mambo yaliyotukia au habari za kubuni.

**Methali**: Ni muhtasari wa maneno ya kisanii wenye maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa.

**Nahau:** Fungu la maneno lenye maana maalum isiyotokana na maana za maneno hayo.

**Vitendawili:** Maneno yanayoficha maana ya kitu ili kisijulikane kwa urahisi; fumbo.

**Nyimbo:** Maneno yanayotamkwa kwa sauti ya muziki.

**Mashairi:** Ni tungo za kisanaa zenye mpangilio maalumu wa lugha ya mkato katika usemi.

**Fasihi Andishi:**

Fasihi andishi ni ile iliyoandikwa vitabuni, vipengele vyake vikiwa riwaya, hadithi fupi, tamthilia na ushairi. Fasihi andishi ukilinganisha na Fasihi simulizi katika jamii nyingi za Kiafrika, hii ndiyo fasihi changa, wakati fasihi simulizi ni ya kale zaidi.

Fasihi hutumia lugha kufafanua tabia za watu na athari zake huku ikituzindua ili tuone uzuri au ubaya wa jambo au tabia fulani kama vile wizi, wivu, tamaa na kadhalika.

Fasihi hushughulikia ulimwengu halisi na mambo yale yale yanayotuzunguka. Tunapoyachambua mambo hayo, tunaona kuwa yanatukia katika mazingira yetu pia yanatupa mafunzo muhimu maishani.

- **Hadithi fupi**: Hadithi Fupi ni aina ya kazi andishi ambayo huwa fupi; na huangazia wazo moja kwa kurejelea kisa kimoja. Hadithi huwa na wahusika wachache na huchukua muda mfupi. Aghalabu hadithi fupi huchapishwa katika mkusanyiko wa hadithi nyingine fupi.
- **Riwaya:** Ni hadithi ndefu ya kubuni iliyoandikwa kwa maandishi ya nathari, aghalabu inayoeleza ukweli fulani wa maisha.
- **Tamthilia / tamthiliya**: Ni utungo wa kisanaa ambao huweka wazo fulani katika matendo na mazungumzo, aghalabu huweza kuigizwa.
- **Ushairi:** Kazi au namna ya kutunga mashairi.

Fani katika Hadithi

**Fani** ni ufundi wa msanii katika kuumba umbo la kazi yake ya fasihi kutokana na ubunifu wake. Ufundi huo ndio unaoboresha njia anayoitumia msanii katika kutoa ujumbe wake kwa hadhira inayokusudiwa kwani ndimo tunapata uzuri wa sanaa na upya.

Vipengele Muhimu katika Fani

**1. Wahusika**

Wahusika ni watu au viumbe ambavyo msanii wa hadithi huwatumia ili kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Katika hadithi msanii huwagawa wahusika katika makundi mawili: wahusika wakuu na wahusika wadogo. Wahusika wakuu ni wale ambao wanajitokeza kuanzia mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Wahusika wadogo ni wale ambao wanajitokeza mara chache au katika sehemu mbalimbali za kazi za fasihi.

### Tabia za wahusika katika hadithi za fasihi simulizi

Wahusika wanaweza kuwa wanyama au binadamu. Mara nyinyi wahusika wanaweza kuonyesha tabia nzuri kama vile umoja, ushirikiano, upendo, upole, unyamavu, wema, utulivu na kadhalika. Kwa upande mwingine, wahusika huweza kuonyesha tabia mbaya kama vile uchoyo, uvivu, ukatili, wivu, ujanja, tamaa na kadhalika.

### 2. Mandhari

Ni mahali katika kazi ya fasihi yaani mahali ambapo matukio ya hadithi au masimulizi hutokea. Mahali hapo paweza kuwa halisi (kama vile chuoni, sokoni, mgahawani, kijijini, msituni, majini, angani na kadhalika) au pa kufikirika (kama vile mbinguni, kuzimuni, ahera na kadhalika).

### 3. Muundo

Ni mtiririko wa visa au namna matukio katika kazi ya fasihi yalivyopangwa na kuleta mtiririko wa kazi husika wa fasihi. Muundo unaweza kuwa wa moja kwa moja, wa mwanzo-upeo-mwisho au kinyume chake yaani mwisho-upeo-mwanzo.

### 4. Mtindo

Ni mbinu ya kipekee inayohusu uundaji wa kazi ya fasihi na kutofautisha msanii mmoja na mwingine kulingana na hisia zake. Tofauti hii inaweza kujitokeza kwa namna mbalimbali kama vile kuingiza kipengele cha wimbo katika hadithi, matumizi ya nafsi, matumizi ya majibizano, matumizi ya nahau na misemo au methali au tamathali za usemi, miundo ya sentensi na kadhalika. Kwa ufupi mtindo ni matumizi ya lugha.

**ZOEZI LA 7:**

***Oanisha misemo ifuatayo iliyotumiwa katika hadithi na maana zake:***

| Misemo | Maana |
|---|---|
| 1. Kazi kupamba moto | A. Kuketi |
| 2. Kujikokota na shoka | B. Kunywa |
| 3. Kukaa kitako | C. Kufanyia mzaha. |
| 4. Kulegeza makoo | D. Kuendelea kwa kutumia nguvu nyingi zaidi. |
| 5. Kupiga mbeu ya shibe | E. Kata miti pole pole. |
| 6. Kuchezea mtu shere | F. Kutosheka na chakula baada ya kukila. |

### 8.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

**ZOEZI LA 8:**


***Soma hadithi "Kobe na Nyani" kisha uzungumzie kwa marefu mawazo makuu uliyoyapata kutoka hadithi.***

### 8.6. Kuandika: Utungaji wa Hadithi

**ZOEZI LA 9:**

***Andika katika Kiswahili hadithi simulizi moja ya Kinyarwanda unayoijua.***

## SOMO LA 9: MAUDHUI KATIKA HADITHI SIMULIZI



**ZOEZI LA 1:**

***Zungumzia mchoro hapo juu na vitendo vinavyofanyika.***

### 9.1. Kusoma na Ufahamu: Wafalme Wawili

*Soma hadithi hii inayofuata kuhusu* "Wafalme Wawili"*, kisha jibu maswali ya ufahamu yaliyotolewa hapo chini.*

Hapo zamani za kale, kulikuwa na wanyama waliokuwa wanaishi msituni. Kila mnyama alikuwa anaishi na mke wake na watoto wake tu, bila kujali kuhusu wanyama wengine. Msituni huko hakukuwa na mfalme wala kiongozi yeyote wa wanyama hao. Walikuwa na uhuru wa kuishi na kutembea mahali huku na kule.

Siku moja, walipotazama namna wanyama wa misitu mingine walivyoishi, walidhani kuwa wanyama hao walikuwa na furaha zaidi kuliko wao, kwa sababu wanyama wa misitu mingine walikuwa na mfalme. Walisema,

“Jameni, acheni tujichagulie mfalme kama wanyama wa misitu mingine.” Siku ya kuchagua mfalme ilipofika, walikutania kwa Bwana Nungunungu. Wote walikuwa mahali huko: Simba, Tembo, Chui, Twiga, Ngiri, Sungura, Nguchiro, Fisi, Nyoka, Mbogo, Ndege na Samaki. Wagombea uchaguzi walikuwa watatu tu: Tembo, Simba na Sungura. Kabla ya uchaguzi, kila mmoja alijaribu kuomba kura huku akijaribu kuwashawishi wanyama wengine kuhusu namna anavyofaa kuchaguliwa kuwa mfalme kuliko wagombea wengine. Kila mgombea alijinadi kuwa yeye ana tabia nzuri zaidi kuliko washindani wake.

Ilipofika zamu ya Tembo kusema, alifungua domo lake na kusema: “........ msituni hapa na misitu mingine yote hakuna mnyama aliyekuwa na nguvu kama mimi. Nikichaguliwa kuwa mfalme wenu, nitalinda usalama wenu, mabibi zenu na watoto wenu. Hakutakuwa na mnyama kutoka misitu mingine atakayewashambulia. Hata binadamu hataingia hapa tena.” Papo hapo akateuliwa kuwa mfalme wa wanyama wote msituni humo.

Siku chache baadaye, Mfalme Tembo aliita mkutano wa wanyama wote. Wote waliitikia wito, wakafika mbele ya Mfalme. Hapo Mfalme Tembo alisema: “Tegeni masikio nyote kwa sababu jambo ninalotaka kuzungumzia ni zito na litaathiri kila mmoja wenu wakati wote...... Kazi ya kulinda usalama wenu ni kazi ngumu sana na inanilazimisha kula chakula kizuri kila siku. Mimi sitaendelea kula nyasi kuanzia leo. Hivyo inamaanisha kwamba kila siku ninahitaji wanyama watakaoniletea chakula ili nile vizuri!”

Siku iliyofuata, Bwana Ngiri alitayarisha chakula. Siku nyingine, Nguciro akakiandaa chakula kizuri. Mambo yaliendelea namna hiyo mpaka wanyama wote majike kwa madume walipomaliza zamu zao. Ilipofika zamu ya Sungura, kutayarisha chakula hicho, Sungura alikimbia haraka kwa Mfalme Tembo kumuuliza swali moja. Alipofika hapo, Mfalme Tembo ndiye alikuwa wa kwanza kumuuliza Sungura: “We raia mbaya unayedharau Mfalme, mbona hujaleta chakula? Unataka nife leo? Ama unataka wewe mwenyewe uwe chakula changu sasa hivi!”

Sungura aliogopa sana na kuanza kutetemeka, lakini alijaribu na kumuuliza Mfalme swali moja lililobadilisha mambo msituni hapo. “Kuna wafalme wangapi msituni humu? Sijui ni yupi atakaye kuwa analetewa chakula kila siku kati yenu wawili” Sungura akasema. Mfalme Tembo kwa kusikia hayo, ghafla alifoka na kumuuliza Bwana Sungura, “Nani huyo mwendawazimu anayejidai kuwa Mfalme hapa? Twende kanionyeshe haraka nikamfundishe somo moja ambalo hatalisahau maishani mwake!” Sungura alimwelekeza wakatembea kwa haraka sana kama kilomita tatu mpaka walipofika kwenye mto wenye kina kirefu.

Sungura alimwonyesha Mfalme Tembo kwa kutumia kidole: “Tazama pale majini. Mfalme huyo anajificha ndani ya maji. Nenda kaongee naye. Lakini ujue kwamba yeye haogopi mnyama yeyote.” Sasa ndipo Mfalme Tembo alielekea kwenye mto kumtafuta mfalme huyo mwingine. Kwa kutazama ndani ya maji, aliona Tembo wa kiume mnono kama yeye na kumwambia, “We raia mbaya sana, mjinga na mshenzi! Toka hapo nikuonyeshe mfalme ni nani kati yetu!” Ghafla, Mfalme Tembo alijitupa ndani ya mto ili apigane na mfalme huyo. Lo! Alianza kupiga kelele kuomba msaada. Mungu weee nisaidie.....nisaidie jameni ..... nisaidie .....! Papo hapo, Sungura alishikwa na huruma sana na mara moja akaanza kupiga kelele kuomba wanyama wenzake kuja kumwokoa mfalme wao. Hivyo basi, karibu nao kulikuwa na wanyama wenye nguvu kama vile Simba, Vifaru, Nyati na wengine wengi walikuja wakaogelea majini na kumwokoa mfalme wao.

Baada ya tukio hilo, Tembo alihudumiwa kwa wiki tatu akapona. Siku tatu baadaye, Sungura alimsogelea mfalme wao na kuanza kumwelezea sababu iliyomfanya amdanganye mpaka ajitose majini. Mfalme wao alijutia kosa lake la kuwanyonya wenzake na kula mali zao mpaka akaamua kuwaita wanyama wote ili awaombe msamaha. Wanyama walipofika walifurahia kwamba mfalme wao ameweza kukiri kosa lake. Wao waliamua kumchagua Simba awe kiongozi wao naye akaahidi kwamba angekomesha tabia zote mbaya na mienendo mingine isiyofaa miongoni mwa wanajamii wote. Aliagiza sheria iwekwe na kila mwanajamii aheshimu wengine. Tangu siku hiyo, ndiye mfalme wa pori na wanyama wote huheshimu uamuzi wake. Huu ndio mwisho wa hadithi.

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Ni sababu gani iliyowafanya wanyama msituni wajichagulie mfalme?
2. Taja angalau majina matano ya wanyama waliohudhuria mkutano wa kuchagua mfalme.
3. Kila mgombea kati ya wale watatu alipewa fursa ya kufanya nini?
4. Ni juu ya kigezo kipi Bwana Tembo alichaguliwa kuwa mfalme wa wanyama?
5. Alipoita mkutano wa wanyama wote baada ya kuchaguliwa, Mfalme Tembo aliwaambia nini?
6. Je, unadhani wanyama wengine walifurahia utawala wa Mfalme Tembo? Eleza jibu lako.
7. Sungura alipofika nyumbani kwa mfalme Tembo alipokelewa vipi?
8. Mfalme Tembo aliposema: “Nitamfundisha somo moja ambalo hatasahau maishani mwake” alikuwa anamaanisha nini?

9. i) Mfalme Tembo alichokiona ndani ya maji kilikuwa nini?

   ii) Tembo alifanya nini papo hapo? Mambo yalikuwaje baadaye?

10. Kwa nini Mfalme Tembo alijuta na kuomba msamaha wanyama wengine?

11. Ni nani aliyeteuliwa kuwa mfalme? Mtazamo wake ulikuwa upi katika uongozi wake?

12. Ni fundisho lipi linalopatikana katika hadithi hii?

## 9.2. Msamiati kuhusu Wafalme Wawili.

### ZOEZI LA 2:

***Eleza maana ya maneno yaliyopigiwa kistari katika sentensi zifuatazo:***

1. Wanyama walimchagua Simba kuwa **mfalme** wao.
2. Walikuwa na **uhuru** wa kuishi kokote.
3. Kila mgombea uchaguzi alijaribu **kuwashawishi** wanyama wengine.
4. **Tegeni masikio** nyote nitakayowaelezea.
5. Nitakalozungumzia **litaathiri** kila mmoja wenu.

### ZOEZI LA 3:

***Jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno haya kutoka hadithi: mwendawazimu, raia, msituni, haogopi, akili, kutetemeka, mtoni, ilipofika, amemdharau, alimfokea.***

1. Alipofika mbele ya Mfalme Tembo, Sungura alianza ..............................
2. Mfalme Tembo alisema kwamba mnyama yule mwingine aliyejidai kuwa mfalme ni........................................
3. Zamu ya Sungura kumpikia mfalme ......................................, yeye hakumpikia chakula.
4. Katika hadithi simulizi, Sungura huonekana kama mhusika mwenye ..............................nyingi.
5. ..............................................mnaishi viumbe kama samaki na ngwena.
6. Simba ..................................................mnyama yeyote.
7. Mfalme Tembo alifikiri kwamba Sungura .......................................
8. Wanyama walikuwa wanaishi ........................................ bila shida yoyote.
9. Mfalme Tembo................................................ "mfalme" yule mwingine.
10. ..................................wote walikuwa wametarajiwa kumtayarishia chakula Mfalme.

## 9.3. Sarufi: Matumizi ya Majina ya Ngeli ya Ku- na Viumishi Ambatana.

**ZOEZI LA 4:**

***Tazama maneno yaliyopigiwa kistari kama yalivyotumiwa katika hadithi kisha utaje aina zake.***

1. Uhuru wa kutembea mahali **huku** na **kule**.
2. Msituni **huko** hakukuwa na mfalme yeyote.
3. Wanyama wote walikuwa mahali **huko**.
4. Msituni **huku** na misituni mingine **kule** hakuna mnyama mwenye nguvu kama mimi.

**Maelezo muhimu**

- Maneno **huku**, **huko**, **kule** yaliyotumiwa katika sentensi hapo juu ni vivumishi. Vimeambatana na maneno yenye dhana ya mahali au maeneo kama vile mahali, msituni. Kundi la majina haya huunda majina ya ngeli ya **Ku-**.
- Matumizi ya vivumishi hivi huchukua mofimu Ku- mwanzoni au mwishoni mwa neno.
- Mofimu hii inaweza kutumiwa kwa kuonyesha vitu vilivyo mbali au karibu.

**MIFANO:**

- Mahali **kule** kuna nyasi nyingi. (mbali)
- Chuoni **huku** kuna wanafunzi wengi. (karibu)

**1. Vivumishi vya kuonyesha**

- Mahali **huku** kunaonekana vizuri.
- Mahali **huko** kunajulikana.
- Mahali **kule** kunajulikana.


**1. Vivumishi vya kuonyesha**

**MIFANO:**

- Mahali **huku** kunaonekana vizuri.
- Mahali **huko** kunajulikana.
- Mahali **kule** kunajulikana.

2. **Vivumishi vya kumiliki**

**MIFANO:**

| UMOJA | WINGI |
|---|---|
| Mahali **kwangu** kunanifurahisha. | Mahali **kwetu** kunatufurahisha. |
| Mahali **kwako** kunanifurahisha. | Mahali **kwenu** kunatufurahisha. |
| Msituni **kwake** kunamfurahisha. | Msituni **kwao** kunawafurahisha. |

**3.Vivumishi vya kuuliza**

**MIFANO:**

- Mahali kupi kunapendeza?
- Sokoni kupi hakuna wateja?

**4. Vivumishi vya idadi**

**Tanbihi:** Ngeli hii haiambatani na vivumishi vya idadi.

**5. Vivumishi vya kurejesha**

**MIFANO:**

Shuleni **kwenyewe** kuna wanafunzi na walimu.
Musanze **kwenyewe** kuna baridi.
Mahali **kwenyewe** kunanyesha mvua.

**6. Vivumishi vya sifa**

**MIFANO:**

- Mahali **kuchafu** kumefagiliwa.
- Mnyama mmoja alikimbia mahali **kurefu**.

**ZOEZI LA 5:**

***Sahihisha sentensi zifuatazo kwa kuzingatia matumizi bora ya vivumishi vya majina ya ngeli ya ku-***

1. Sokoni wapi kunapatikana bidhaa zenye bei nafuu?
2. Mahali refu kunafurahisha.
3. Darasani hangu kunavutia.
4. Msituni huku wana Simba mkali.
5. Mguuni wapi pamezungumziwa kuwa na kidonda?

## 9.4. Matumizi ya Lugha: Maudhui katika Fasihi

**ZOEZI LA 6:**

***Soma hadithi uliyopewa kuhusu "Wafalme wawili" kisha ujibu maswali yafuatayo:***

1. Soma tena hadithi uliyopewa kuhusu "Wafalme Wawili, kisha eleza sifa za wahusika wakuu waliozungumziwa.
2. Ni mgogoro upi uliojitokeza baina ya Mfame Tembo na wanyama wengine?
3. Taja mambo muhimu angalau manne yaliyozungumziwa katika hadithi.

- **Maelezo muhimu kuhusu maudhui**

Maudhui ni mawazo na mafunzo yote yanayozungumziwa yaani mambo yote yanayosemwa au yanayokusudiwa kusemwa. Kwa ufupi, ni yaliyomo katika kazi yoyote ya fasihi.

**Vipengele vya maudhui**

Vipengele vinavyoshughulikiwa katika maudhui ni kama hivi vifuatavyo: kichwa cha habari, dhamira, migogoro, ujumbe, falsafa, muhtasari.

Hebu tutoe maelezo kuhusu vipengele hivyo.

**Maelezo kuhusu vipengele vya maudhui**

Maudhui katika kazi yoyote ya fasihi huweza kuchunguzwa kupitia vipengele vifuatavyo:

- **Kichwa cha hadithi**

Mhakiki anachunguza kama kichwa kinasadifu yanayozungumziwa katika hadithi. Ila, katika kazi nyingi za fasihi simulizi, kichwa anachokitumia msanii ni majina ya wahusika wake (kama vile "Hadithi ya mbuzi, kondoo na mbwa, ...").

- **Dhamira**

Dhamira ni wazo kuu na mawazo mengine yanayosaidia katika kulijenga wazo kuu. Jambo kuu hilo lililomfanya msanii atunge kazi yake ndilo liitwalo "**dhamira kuu**"; yale madogo madogo yanayosaidia wazo kuu ni "**dhamira ndogo ndogo.**"

- **Mgogoro**

Mgogoro ni hali ya kutoafikiana baina ya pande mbili au zaidi yaani mivutano na misuguano mbalimbali ipatikanayo katika kazi ya fasihi. Migogoro hiyo yaweza kuwa kati ya: wahusika, familia zao na matabaka yao. Migogoro ndiyo inayoifikisha hadithi kwenye kilele chake.

- **Falsafa**

Ni msimamo au mtazamo wa msanii kuhusu maisha au masuala mbalimbali ya kijamii kwani msanii anapotunga kazi yake huwa na imani na mwelekeo. Falsafa yake ni ile hali ya kuamua kufuata na kushikilia jambo fulani linaloweza kupingwa na wengi lakini akalishikilia tu. Falsafa inaweza kuwatofautisha wasanii wawili wanaoandika kuhusu mazingira yanayofanana. Kwa mfano, msanii anaweza kuwa na msimamo wa kimapinduzi kwani amejaribu kutunga kazi yake kuhusu tatizo linalochangia kukwama kwa ujenzi wa jamii mpya (kama vile wivu, magendo, usaliti, uhujumu, uchumi, na kadhalika) na kuonyesha suluhisho. Msanii anaweza pia kuwa na msimamo wa kimapokeo na kutotaka kubadilika kwa mambo.

- **Ujumbe**

Ni mafunzo au maadili yaliyokusudiwa na msanii yaifikie jamii aliyoilenga kufikisha kazi yake ya kifasihi. Msanii anapoitunga kazi yake huwa na taarifa ambayo hutaka iifikie jamii aliyoikusudia. Taarifa hiyo hupatikana baada ya kuisoma kazi hiyo. Dhamira kuu hubeba taarifa ya msingi na dhamira ndogo ndogo hubeba taarifa ambayo husaidia kujenga ile ya msingi. Hapa ndipo mhakiki anajiuliza maswali kadha kama:

1. Hadithi hii inafundisha nini?
2. Inaonya?
3. Tunakubaliana na ujumbe wa hadithi au la?
4. Na kadhalika .....

- **Muhtasari**

Ndicho kipengele cha sita katika maudhui kinachoshughulikiwa na mhakiki. Hapa ndipo anatoa ufupisho wa hadithi anayoichambua.

## 9.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

**ZOEZI LA 7:**

***Kwa maneno yako mwenyewe eleza ikiwa kichwa cha hadithi "Wafalme wawili" kinasadifu yanayozungumziwa katika hadithi yenyewe.***

## 9.6. Kuandika: Utungaji wa Hadithi

**ZOEZI LA 8:**

***Baada ya kusoma hadithi "Wafalme Wawili", tunga hadithi yako yenye maneno yasiyopungua 200.***

## TATHMINI KUHUSU MADA YA TATU

***I. Soma kifungu cha habari ulichopewa hapo chini kisha ujibu maswali yaliyopendekezwa mwishoni mwa kifungu.***

**Hadithi: Wivu Haufai**

Hapo zamani mamba alikuwa na meno mazuri sana. Wanyama wengi waliyapenda meno yake. Baadhi yao walisikika wakitia chumvi kuwa meno ya mamba yalikuwa na thamani sawa na dhahabu.

Mamba huyo alipotangaza nia yake ya kujipatia jiko karibu kila mnyama aliyekuwa na binti mzuri alitaka binti yake aolewe naye. Hivyo mabinti wengi walionekana wakijipitisha mbele ya mamba huku mmoja akiwa amejipamba vizuri ili kuweza kuliteka penzi lake.

Hali hiyo haikumpendeza kabisa Sungura kwani miongoni mwa wasichana hao waliojitokeza, alikuwepo mmoja aliyependwa sana na Sungura. Hivyo, Sungura wakati wote alikuwa akiwaza la kufanya ili kumwangusha Mamba.

Siku moja Sungura alipita nyumbani kwa Mamba na kumkuta amelala fofofo chini ya kivuli cha mti huku meno yake mazuri yakionekana waziwazi. Hapo Sungura aliweza kuyaona maganda mengi ya karanga na akagundua kuwa Mamba alikuwa akitafuna karanga.

Siku nyingine Sungura alikuja tena nyumbani kwa Mamba. Akamwambia, “Rafiki yangu nimekuchukulia zawadi nzuri uipendayo.’’ Zawadi gani?” “karanga”, alijibu Sungura huku akimwonyesha mamba mfuko uliojaa karanga. Mamba alipouona mfuko huo, aliurukia mfuko akaliingiza domo lake refu ndani na kuanza kutafuna kwa pupa. “Mama wee !’’ Mamba alisikika akilia huku mikono yake ikishikilia mdomo wake ambao sasa umejaa damu. Meno yake mengi yaling’oka pia. Kumbe ndani ya mfuko ule Sungura aliweka mawe mengi na njugu nyasa chache tu. Mamba alipojaribu kutafuna alichofikiria kuwa ni karanga, meno yake mengi yaling’oka.

Sungura alipoona mbinu yake imefaulu, aliondoka na kuelekea kwake kwa furaha. Siku hiyo jioni, wanyama wengi walishangaa kumuona Sungura alikuwa amevaa miwani na kupepesuka ovyo. Kumbe alikuwa akisherekea ushindi wake dhidi ya mamba.

Habari za Mamba kung’olewa meno yake zilienea kwa haraka sana. Wasichana wote walipopata habari hizo, walibadilisha mawazo yao ya kutaka kuolewa na Mamba ambaye sasa alikuwa kibogoyo na kuchukiza sana.

(Hadithi hii msingi wake ni kutoka *NIYOMUGABO C. (2013). Mafunzo ya Kiswahili. Kitabu cha Mwanafunzi kidato cha Tano*).

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Mamba alikuwa akijulikana kwa sifa gani?
2. Uzuri wa Mamba ulipotea namna gani?
3. Eleza jinsi ujanja wa Sungura na mpango wake dhidi ya Mamba ulivyofaulu.
4. Husisha kichwa "WIVU HAUFAI" na yaliyoelezwa katika hadithi.
5. Ni ujumbe gani unaojitokeza katika hadithi hii?
6. Chuki ya Sungura na Mamba ilitoka wapi?
7. Kwa maoni yako, ni shida gani alizopata mamba baada ya kung'oka kwa meno yake.

**II. Oanisha nahau katika kundi A na maana zake katika kundi B.**

| A | B |
|---|---|
| 1. kutia chumvi | A. kujifanya kuwa mrembo. |
| 2. kujipatia jiko | B. kulewa. |
| 3. kujikwatua | C. kusinzia sana. |
| 4. kutia fora | D. kufanya achukiwe na wengine. |
| 5. kuangusha mtu | E. kuongeza maneno zaidi ya jambo lilivyo. |
| 6. kulala fofofo | F. kupita/kuzidi. |
| 7. kuvaa miwani | G. kuoa. |

**III. Tunga sentensi moja kwa kila nahau zilizoelezwa hapo juu.**

**IV. Jaza sentensi hizi kwa kutumia maneno katika mabano:**

1. Mahali ................................. (hii, haya, hapa) pametuchosha.
2. Mahali .................................. (huku, hiyi, kuno) kunapendeza.
3. Mahali ................................... (haya, hii, humu) mna nyoka.
4. Hakuna mahali ........................ (mwa, pa, ya) kukaa.
5. Amejificha chumbani ........................... (huku, humu, kile).
6. Pahali ............................. (pengi, kwingi, nyingi) pana wanyama.

# MADA KUU YA 4

## UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO

# MADA KUU YA 4: UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO

## MADA NDOGO: MIDAHALO NA MIJADALA

**Uwezo Upatikanao katika Mada:**

Kuweza kuelewa mwongozo wa midahalo na mijadala na kushiriki katika kazi za majadiliano kwa kuzingatia mada zilizotolewa kujadiliwa; kujiandaa na mdahalo kwa kutafiti na kuandika hoja atakazotumia, kujua jinsi ya kutoa amri kwa vitenzi.

**Malengo ya Ujifunzaji:**

- Kuonyesha uwezo wa kufanya mjadala kutokana na maandalizi ya awali yaliyoegemea katika utafiti;
- Kukumbuka taratibu za kufuata wakati wa kutoa hoja katika makundi;
- Kutafsiri mazingira ya mada na kuijadili bila upotovu wowote;
- Kutambua lugha inayofaa katika majadiliano;
- Kuelezea mtiririko wa hoja au majadiliano ili kujiepusha na marudio ya wazo au fikra;
- Kuelezea jinsi ya kutoa amri kwa kutumia hali ya kushurutisha kwa vitenzi.


### Kazi Tangulizi

1. Nini maana ya mdahalo?
2. Unaelewa nini kuhusu mjadala?
3. Ni tofauti gani iliopo kati ya mdahalo na mjadala?
4. Ni uhusiano gani uliyopo kati ya mdahalo na mjadala?
5. Una ujuzi gani kuhusu andalio la mdahalo na mjadala?

## SOMO LA 10: MDAHALO

**ZOEZI LA 1:**

***Chunguza mchoro hapo chini kisha, eleza shughuli zinazoendelea kwenye mchoro huo.***



### 10.1. Kusoma na Ufahamu: Mazungumzo Baina ya Wanafunzi

*(Mwanafunzi mmoja anaingia katika kidato cha nne. Kiranja wa darasa anamtambulisha)*

**Kiranja wa darasa:** Wanafunzi wenzangu, huyu anayesimama mbele yenu anaitwa Shupavu na anasoma katika kidato cha sita, mchepuo wa lugha. Kumbukeni kuwa jana, mwalimu wetu alituambia kuwauliza wanafunzi wa kidato hicho kuhusu midahalo. Hilo ndilo jambo linalomleta hapa dada yetu Shupavu. Karibu sana darasani kwetu!

**Shupavu:** Ahsante sana wanafunzi wenzangu kwa mwaliko wenu ili nije niwaelimishe kuhusu midahalo. Midahalo si mambo mageni kwenu ila wanafunzi wengi huchanganya midahalo, mijadala, kongamano na mazungumzo. Sababu muhimu ya kuchanganya mambo haya ni kwamba wanafunzi hao hufikiria kwamba shughuli hizo zote hulenga majadiliano na mazungumzo baina ya watu wengi juu ya mada maalum.

**Mwanafunzi wa 1:** Nami sielewi kabisa tofauti iliyopo kati ya mambo hayo. Labda ninalofahamu ni kwamba kongamano ni mjadala juu ya jambo fulani unaofanywa na mkusanyiko wa watu baada ya wazungumzaji maalumu kuuanzisha. Na mjadala huhusu mada fulani inayojadiliwa na kufafanuliwa na watu waliopo. Je, midahalo ni nini?

**Shupavu:** Mdahalo ni majadiliano ya watu wengi juu ya jambo moja maalum. Kwa maneno mengine mdahalo ni namna ile ya mazungumzo yanayofanywa na watu wengi mahali pamoja kuhusu jambo moja maalum. Majadiliano hayo yanafanywa kwa kutolea hoja kuhusu jambo hilo ili kushindana kwa hoja. Kwa hiyo, ni lazima kuwe na:

kiongozi (au mwenyekiti) wa kuyaongoza,

wasemaji wa pande mbili; yaani watetezi wanaoiunga mkono mada hiyo na wapinzani wanaoipinga mada yenyewe,

wasikilizaji-washiriki nao husikiliza mazungumzo yanayofanywa na pande hizo mbili; yaani utetezi na upinzani ili baadaye waweze kutoa hoja zao kuhusu yaliyozungumziwa.

**Mwanafunzi wa 2:** Samahani kwa kukukata kauli mwanafunzi mwenzetu. Unamaanisha kuwa watu wanaozungumza hawana msimamo sawa? Je, kuna faida zipi za kutetea na kupinga mada iliyopo?

**Shupavu:**Kwa kweli mazungumzo haya ni kama mashindano ya hoja, kwani mwishowe ni lazima tupate mshindi. Watetezi hutafuta hoja zao kuitetea mada na wapinzani hutafuta mawazo ya kuwapinga na baadaye wanafikia wakati wa kupiga kura ili kujua mshindi kati ya pande zote mbili. Kwa hiyo, kiongozi wa mdahalo huwa na kazi muhimu ya kuongoza mazungumzo hayo kwa kuhakikisha kuwa kila msemaji anatumia muda uliopangwa na kuimarisha nidhamu katika mazungumzo yao. Wahusika wengine kama katibu huandika hoja zinazotolewa na kuzisomea hadhira. Kwa upande wa wasikilizaji-washiriki, wao hufuata mazungumzo na kusaidia kuchagua mshindi.

**Mwanafunzi wa 3:** Ni vizuri ndugu yetu. Naona tumeelewa mengi kuhusu mdahalo. Lakini, kwa upande wangu, ningependa utuelezee pia umuhimu wa midahalo.

**Shupavu:** Midahalo ni muhimu katika maisha ya binadamu, hasa kwa wanafunzi wanaojifunza lugha yoyote. Katika njia hii, midahalo hukuza uwezo wa kufikiri, hali ya udadisi wa mtu na ustadi wake wa kutumia lugha husika. Midahalo humfanya pia mwanadamu aweze:

kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri; kuzoea kusikiliza na kupima hoja za wenzake; kuzoea kutoa maoni na maelezo kuhusu mada iliyopo kwa kuzingatia muda uliowekwa.

**Kiranja wa darasa:** Asante sana ndugu yetu kwa maelezo yako mazuri. Mimi ningependa utuelezee jinsi upande fulani (watetezi au wapinzani) unavyoweza kufanya ili uweze kupata ushindi katika mdahalo.

**Shupavu:** Wanafunzi wenzangu, ili upande fulani ufaulu katika mdahalo, ni lazima kujiandaa ipasavyo; yaani kufanya utafiti na kuzipanga hoja vizuri kabla ya mdahalo kuanza. Kuzipanga hoja kunazifanya fikra zisije zikarudiwarudiwa.

Wakati wa kuzungumza unapofika, ni lazima kila mzungumzaji ajitahidi:

kutumia lugha sahihi ya kuvutia na ishara za mwili zinazolingana na hoja husika,

kuonyesha heshima na adabu; kutokasirika ovyo au kutokata tamaa; kujiamini ili wasikilizaji-washiriki wakuunge mkono na kuonyesha urafiki na ushirikiano kwani kushindana kwa hoja si wakati wa kupigana au kugombana.

**Mwanafunzi wa 4:** Unataka kusema kuwa inakatazwa kukasirika ovyo katika mashindano haya?

**Shupavu:** Ndiyo! Kila upande unapaswa kuyaheshimu mawazo ya upande mwingine na hata yale ya wasikilizaji-washiriki na kukubali kushindwa, kwani "asiyekubali kushindwa si mshindani." Hata hivyo, ili muweze kufanikiwa katika mazungumzo ya aina hii, ni vyema mfanye mazoezi mengi ili kuimudu lugha ya Kiswahili.

Asanteni nyote! Ninamalizia hapa, mkihitaji maelezo mengine zaidi msisite kunialika tena.

*(Wanafunzi wote wanampigia makofi).*

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Shupavu ni nani?
2. Nani aliwaambia wanafunzi wamwalike Shupavu?
3. Mwaliko wake ulikuwa na madhumini gani?
4. Taja watu wanaohusika katika mdahalo na kazi zao.
5. Eleza mambo yanayoweza kuzingatiwa ili upande fulani uweze kufaulu katika mdahalo.
6. Kwa nini mdahalo huchukuliwa kama mashindano?
7. Onyesha faida za mdahalo kwa wanafunzi.
8. Taja mambo ya kuzingatiwa wakati wa kujiandaa kwa mazungumzo ya mdahalo.
9. Taja na kueleza aina nyingine za mazungumzo zilizozungumziwa katika kifungu hiki.
10. Ni zipi tabia zinazotarajiwa kwa kila mshiriki wa mdahalo?

### 10.2. Msamiati kuhusu Maana ya Mdahalo

**ZOEZI LA 2:**

***Andika maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika mazungumzo:***

1. Hoja
2. Majadiliano
3. Watetezi
4. Wapinzani

**ZOEZI LA 3:**

***Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:***

1. Taratibu
2. Kusikiliza
3. Mada
4. Mashindano

## ZOEZI LA 4:

***Tumia maneno yafuatayo kwa kujaza sentensi zifuatazo: huchanganya, mazungumzo, yaheshimiwe, kiongozi, upekee, maalumu, wapinzani, ustadi, mawazo, hoja.***

1. Mawazo ya kila upande ................................................
2. Ni lazima kuwe na mfuatano mzuri wa ...............................
3. Kazi ya .......................... wa mjadala si rahisi.
4. Midahalo ni mojawapo ya ...............................................
5. Midahalo ina .............................. wake ukiihusisha na mazungumzo mengine.
6. Wanafunzi wengi .............................. midahalo na mijadala.
7. Mada moja ............................hujadiliwa katika mdahalo.
8. Kazi ya Katibu ni kuziandika ................................ zitolewazo.
9. ................................... ni wale wasiokubaliana na hoja zilizotolewa.
10. Midahalo hukuza ...................... wa kutumia lugha.

### 10.3. Sarufi: Matumizi ya Hali ya Kushurutisha kwa Vitenzi

## ZOEZI LA 5:

***Viandike vitenzi vya umoja kwa wingi na vya wingi kwa umoja.***

**MIFANO:**

kumbukeni → kumbuka

eleza→ elezeni

1. zungumzieni→
2. tetea →
3. pangeni →
4. angalia →
5. simameni →
6. changanua →
7. zingatieni →
8. hakikisha →
9. ongoza→
10. changieni→

## ZOEZI LA 6:

***Viandike vitenzi ulivyoviandika kwenye zoezi hapo juu (umoja na wingi) katika hali kanushi.***

**MIFANO:**

msikumbuke → usikumbuke

usieleze → msieleze

**Maelezo muhimu kuhusu Matumizi ya Hali Shurutishi ya Vitenzi.**

Katika umoja, ukanushaji wa hali ya kushurutisha huhusisha matumizi ya kikanushi **"-si-"** ambacho huwekwa baada ya kiambishi cha nafsi, kiishio **"-e"** huwekwa mwishoni mwa kitenzi. **Mfano**: Changieni mada hii.▯ Msichangie mada hii.

**MIFANO:**

**Tafuta maana ya neno hili kwenye kamusi.**

**Jibu:Usitafute** maana ya neno hili kwenye kamusi.

Katika wingi, ukanushaji wa hali ya kushurutisha huhusisha matumizi ya kikanushi "-**si**-" ambacho huwekwa baada ya kiambishi cha nafsi cha wingi na kiishio"**-e**" huwekwa mwishoni mwa kitenzi.

Mfano: Changieni mada hii.▯ Msichangie mada hii.

**ZOEZI LA 7:**

***Ziandike sentensi za umoja kwa wingi, na za wingi kwa umoja.***

1. Jitayarisheni kujadili mada mliyopewa na mwalimu.
2. Chagua kundi moja kati ya lile la kuunga ama la kupinga kauli iliyotolewa.
3. Ongoza mdahalo huu kama mwenyekiti aliyechaguliwa darasani.
4. Toa oni lako kuhusu jambo linalozungumziwa sasa.
5. Tangaza upande ulioshinda baada ya hoja kutoka pande zote mbili kusomwa.
6. Someni vizuri hoja zote kama zilivyotolewa na kila upande.
7. Jiepusheni na tabia mbaya ya kukasirika ovyo.
8. Wekeni mikono juu ili mruhusiwe kusema kitu.

**ZOEZI LA 8:**

***Ziandike sentensi zote hizo (za umoja na wingi) katika hali kanushi.***

## ZOEZI LA 9:

***Jaza jedwali lifuatalo kwa kutumia vitenzi vyenye hali shurutishi:***

| Kawaida (umoja) | Kukanusha (umoja) | Kawaida (wingi) | Kukanusha (wingi) |
|---|---|---|---|
| 1. kimbia | ……………… | ……………….. | ……………… |
| 2. …………….. | Usiseme | ……………… | ……………….. |
| 3. …………….. | ……………… | Chungeni | ……………… |
| 4. …………….. | ……………… | ……………… | Msilete |
| 5. cheza | ……………… | ……………… | ……………… |
| 6. …………… | Usichome | ……………… | ……………… |
| 7. …………… | ……………….. | Pateni | ……………… |

## 10.4. Matumizi ya Lugha: Maana ya Mdahalo

## ZOEZI LA 10:

***Pigia mstari neno lililo tofauti.***

**MIFANO:**

***sarufi, mpakuzi, kanuni, lugha.***

1. hoja, mada, maoni, kiungulia.
2. taratibu, maana, mpango, orodha.
3. kinywaji, mahojiano, mazungumzo, majadiliano, mdahalo.
4. kutega sikio, kuwa makini, kuangalia, kutukana.
5. mwenyekiti, msimamizi, daktari, kinara.
6. mwanasheria, istilahi, sarufi, lugha, msamiati.
7. mjadala, mdahalo, mwanya, kongamano.
8. watetezi, wafugaji, wapinzani, wasemaji.
9. kupiga kura, kupinga hoja, kuandika hoja, kufanya mtihani.
10. kupanga mawazo, kufanya utafiti, kuomba Mungu, kutangaza mshindi.

**Maelezo Muhimu kuhusu “Maana ya Mdahalo”**

Katika mdahalo mtu hutathmini jambo kwa kuangazia manufaa na hasara au ubora na udhaifu wa jambo hilo. Watu wa pande mbili wanahusika katika kujadili. Kila upande unatoa maoni yake, huku ukionyesha ubora au udhaifu wa jambo husika. Upande wa kuunga mkono na ule wa kupinga wote wanatoa hoja zao. Mfano wa mada ya mdahalo: “Shule ya Mseto ni Bora Kuliko ya Wasichana au Wavulana Pekee.” Maelezo zaidi kuhusu utaratibu unaofuatwa katika kuandaa mdahalo yatazungumziwa katika somo la 11.

## ZOEZI LA 11:

***Ukifuata maelezo ya hapo juu na mfano wa mada ya mdahalo uliotolewa, sema ikiwa kila kauli ni kweli au si kweli.***

1. Kila mara kwenye mdahalo, kuna pande mbili ambazo zina maoni tofauti kuhusu jambo moja.

2. Katika mdahalo, si lazima kila upande utoe maoni yake.

3. Katika mdahalo, jambo linalozungumziwa huonyeshewa manufaa na udhaifu wake.

4. Kujadili ni kupingana.

## ZOEZI LA 12:

***Jaza matini ifuatayo kwa kutumia maneno mwafaka: (hadhira, upande, muhtasari, maalumu, matokeo, katibu, wajibu, wawili, hoja, nidhamu)***

Mdahalo ni majadiliano baina ya watu wengi juu ya jambo moja …………………. Katika mdahalo, aghalabu wazungumzaji …………….. kwa kila …………………., mwenyekiti wa mdahalo huwa na …………….. mkubwa kwa kufungua na kuendesha mdahalo, kuangalia ………………….., kuwachagua wazungumzaji kutoka katika …………………ili kutoa hoja zao, kupigisha kura na kufunga mdahalo.

Pia huwepo …………………wa mdahalo, ambaye kazi yake kubwa huwa ni kuandika ……………..zinazotolewa na wazungumzaji mbalimbali, na mwishoni kusoma ……………wa hoja hizo zilizotolewa katika mjadala kwa pande zote mbili, pamoja na kutangaza ……………ya kura zilizopigwa.

### 10.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**ZOEZI LA 13:**

***Elezea wenzako (kimazungumzo) upande wako mwenyewe kuhusu mada ifuatayo:***

"Jua ni muhimu kuliko mvua."

### 10.6. Utungaji

**ZOEZI LA 14:**

***Andika aya tatu ukieleza sababu zinazoweza kuufanya upande mmoja kutofaulu/kushindwa katika mdahalo.***

## SOMO LA 11: MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA MDAHALO

**Tazama kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yanayofuata hapo chini.**



**ZOEZI LA 1:**

***Jibu maswali yafuatayo:***

1. Unaona nini kwenye mchoro huu?
2. Unafikiri mchoro huu unazungumzia nini?
3. Mchoro huu unakukumbusha nini katika maisha yako?

## 11.1. Mdahalo: Dawa za Kulevya Ndilo Tatizo Linaloathiri Maendeleo ya Vijana

**Mwenyekiti (anasimama):** Waheshimiwa mabibi na mabwana mliokusanyika hapa leo, kwanza ningependa niwakaribishe katika mdahalo huu. Hapa mbele yenu, mimi ni mwenyekiti. Pembeni mwangu upande wa kushoto mnamuona katibu wa mdahalo wetu.

**Mdahalo wetu unazihusisha pande mbili**: upande wa utetezi na upande wa upinzani. Mada yetu ya mdahalo kama mnavyoiona pale mbele, inahusu: "**Dawa za kulevya ndilo tatizo kuu linaloathiri maendeleo ya vijana.**" Kila msemaji atakayepewa fursa ya kuzungumza asizidi dakika tano na ni sharti ya mdhibiti-muda kumkataza kuendelea kutoa hoja anapozidisha fursa yake ya kusema. Bila kupoteza muda, ningependa nimkaribishe msemaji mkuu wa kwanza upande wa utetezi ili atoe hoja zake.

**Msemaji Mkuu wa 1 (Utetezi):**

Mheshimiwa mwenyekiti, wasikilizaji washiriki, ni kweli kabisa kwamba dawa za kulevya ni tatizo kubwa linalojitokeza miongoni mwa vijana wa leo kiasi kwamba huathiri sana tabia zao na mwenendo wao mwema. Sisi sote tunajua kwamba Mwenyezi Mungu amemkirimu mwanadamu kwa kumpa akili na fahamu ili aweze kufikiri, kuongoza viumbe wengine na kutunza mazingira yake. Kwa hivyo, akili na fahamu ni johari zenye thamani na ni neema kubwa inayomtofautisha na wanyama. Hakika ni kwamba wanadamu wamefadhilishwa kwa fadhila kubwa kuliko viumbe wengine wote. Akili ni kipawa alichotunukiwa ili aweze kutekeleza vizuri wajibu aliopewa na Mungu kwa madhumuni ya kuboresha maisha yake.

Matumizi ya dawa za kulevya hujitokeza kama janga kubwa kwa jamii zetu. Vijana wengi wakiwemo wanafunzi wamezama katika janga hilo kwa kutumia uraibu huu mbaya unaowaangamiza kwa kuwafanya wapoteze afya au kutumbukia katika mienendo mibaya. Wanaotumia dawa hujikuta katika hali ya uvivu unaokuwa kikwazo muhimu katika maandalizi na utekelezaji wa miradi ya kujiendeleza. Badala ya kujielimisha, vijana hao hujiingiza katika mambo mabaya kama vile ugomvi, ujambazi, umalaya, ukatili, n.k. Mtu anapotumia dawa za kulevya huanza kukosa akili timamu inayomwezesha kuwa na mipango mizuri kuhusu maisha yake.

Kwa yote hayo na mengineyo yatakayotolewa na wenzangu, ninaona kwamba wasikilizaji washiriki hamtasita kuniunga mkono kwamba dawa za kulevya ndilo tatizo kubwa miongoni mwa vijana wa leo. Lazima tupambane na dawa hizi ili tuweze kubadilisha maisha ya watoto wetu. Asante sana kwa kunitega sikio.

**Mwenyekiti:**

Naam, waheshimiwa wasikilizaji washiriki, baada ya kusikiliza hoja za msemaji mkuu wa upande wa utetezi, sasa ningependa kumkaribisha msemaji mkuu wa upande wa upinzani ili naye atoe hoja zake.

**Msemaji mkuu wa 1**

**(Upinzani):** Asante sana mwenyekiti. Mimi sikubaliani kabisa na mtetezi wa mada hii. Msemaji huyo alisema kwamba dawa za kulevya ndiyo madhara makubwa kwa maendeleo ya vijana wa leo, lakini mimi ninaona kwamba kuna mambo mengine mengi yanayokwamisha maendeleo ya vijana na ya jamii kwa ujumla.

Kwa maoni yangu, ninafikiria kwamba matumizi mabaya ya teknolojia mpya na mitandao ndilo janga kubwa kwa vijana wetu. Siku hizi vijana wengi hupoteza muda mrefu kwa kuangalia mitandao ambayo huwafanya waige tabia mbovu za watu wasio na adabu na mienendo mizuri. Kijana anamaliza muda wake kwa kuangalia mitandao isiyomnufaisha kwa chochote. Ni dhahiri kwamba hataweza kujiendeleza na hataweza kuwa na mipango mizuri ya kuendeleza jamii yake. Kama yeye ni mwanafunzi atakosa kujifunza kwa bidii ili aweze kuelimika na hata kama yeye ameisha bahatika kumaliza masomo yake na kupata kazi, hataweza kuifanya vizuri kwani muda mrefu ataumaliza kwa kuangalia mitandao hiyo, jambo ambalo litaathiri pato litakalotokana na kazi hiyo.

Aidha, ili kuthibitisha haya, hebu tuchukue mfano wa kijana ambaye kazi yake ni udaktari. Yeye anapofika kazini, jambo la kwanza ni kuchunguza kwa mitandao mambo kadhaa yaliyotukia hapa na pale, kisha kuzungumza na marafiki zake kwa kutumia mitandao ya kijamii, ya fesibuku na mitandao mingine ya kijamii. Kijana huyu hataweza kuleta matunda kwa kazi anayoifanya na jamii huweza kuangamia kutokana na mienendo yake kwani badala ya kuokoa maisha ya watu, yeye amezama katika mambo yasiyo na maana na faida yoyote kwa jamii.

Zaidi ya hayo, matumizi mabaya ya mitandao huendeleza tabia mbaya katika jamii pale ambapo vijana wengi wameanza kuonekana kama wakosefu wa nidhamu, wenye kiburi cha kupindukia baada ya kujitoma katika kutazama baadhi ya vijana wengine kutoka nchi mbalimbali. Ni mara ngapi tunasikia wazazi wakilalamika kwamba watoto wao huwaiga wahusika tofauti ambao wanawatazama katika filamu zisizo na maadili mema? Kumbukeni kwamba mambo haya hutukia wakati ambapo wazazi wameenda kazini na kuacha tarakilishi sebuleni ambapo watumishi wa nyumbani huziwasha na kuwaonyesha watoto hao filamu zenyewe. Wakati mwingine vijana wa leo hupata mienendo mibaya wanapowatembelea ndugu au jamaa zao ambao

wana mazoea ya mienendo isiyo mizuri. Kwa kweli, filamu hizi huchochea tabia mbaya mno kama vile uasherati, uzinzi na nyingine miongoni mwa vijana wetu. Kwa hivyo, ni wazi kwamba vijana wetu hukumbwa na matatizo mengine mengi na mazito zaidi kuliko matumizi ya dawa za kulevya. Ni vyema tuelewe kwamba matatizo haya yote yanapaswa kuchunguzwa na kukomeshwa ili kuwajenga vijana wetu badala ya kufikiri kuwa dawa za kulevya ndilo tatizo kubwa linalohitaji suluhisho kuliko yale mengine. Asante sana Mwenyekiti.

**Mwenyekiti:**

Waheshimiwa wasikilizaji washiriki, tumekwisha kuyasikiliza maoni ya wasemaji wakuu wa pande zote. Sasa ningependa niwakaribishe wasemaji wa pili wa pande hizi mbili watoe hoja zao. Atakayeanza ni yule wa upande wa utetezi.

**Msemaji wa 2**

**(Utetezi):** Asante sana Bwana mwenyekiti, Bwana katibu na waheshimiwa wasikilizaji washiriki. Nimeishaelewa hoja za msemaji anayemaliza kutoa hoja zake kwa kupinga mada yetu na kwa hakika aliyoyasema hayatofautiani na msimamo wetu kama watetezi. Mimi ningependa kumkumbusha tu kwamba matatizo mengi aliyoyazungumzia hutokana na matumizi ya dawa za kulevya au pengine nayo huweza kuchukuliwa kama dawa za kulevya. Kitu chochote kinachoweza kufanywa kwa kipimo kinachozidi kiasi nacho huwa kama dawa za kulevya. Filamu hizo zinazomfanya mtu asahau wajibu wake, matumizi mabaya ya mitandao au simu inayokufanya ubadilishe mwenendo wa kawaida unaotakiwa katika jamii nazo huchukuliwa kama dawa hizo za kulevya.

Dawa za kulevya maana yake msingi ni dawa zinazoweza kumezwa, kujichoma ndani ya sindano, kutafuna au kunusa ili anayezitumia abadili hali na mienendo yake. Katika hali nyingine, wanaotumia dawa hizi hulenga kujiepusha na woga kwani wanapokula na wanapokunywa dawa hizo hufikiria kwamba wamejitia nguvu zinazowawezesha kufanya jambo lolote lile. Kwa hivyo, ni wazi kwamba matokeo ya kitendo cha kutumia dawa za kulevya humbadili mtu kwa kila kitu anachofanya kuanzia fikira zake, mipango na utekelezaji wa shughuli zake. Mtu huyu hatafaa tena kwa chochote kwani ameishageuka mtu mwingine ambaye hawezi kuwa na mpango imara wa kile anachokifanya kwani dawa hizo ndizo humwelekeza katika matendo yake. Hivyo basi, maana hiyo ya dawa za kulevya hupanuliwa kwa vitu vyote vinavyomfanya mtu abadilishe tabia zake, na mienendo yake na akaonekana kama mtu asiye na akili timamu yenye kumwelekeza kutekeleza mambo kwa ufanisi.

Mbali na ukweli huo, tukichunguza dawa zenyewe katika uhalisi wa mambo, tutaona kwamba vijana wanaotumia dawa za kulevya huathirika sana kiafya pale ambapo dawa hizi huingia mwilini na kuua kinga za mwili wake hadi unapoanza kuwa dhaifu kiasi cha kupatwa na magonjwa ya aina mbalimbali. Chunguza kwa mfano hali ya mtu anayetumia dawa kama kokeni, heroini, bangi na miraa. Mtu huyu huathirika kwanza katika ubongo kama alivyozungumzia mwenzangu aliyenitangulia na kisha mwili wake hudhoofika. Madhara huzidi kuongezeka mpaka wakati anapoanza kukosa nguvu za kufanya kazi yoyote katika kulijenga taifa lake na yeye kugeuka mzigo mkubwa kwa taifa zima na wanajamii wengine.

Watu wengi ambao hutumia dawa za kulevya hawawezi kuaminika na mtu yeyote kiasi cha kupewa kazi ya kujiendeleza. Vilevile anapopewa kazi hiyo, matokeo ni kwamba yeye huzembea kufanya kazi hiyo mpaka anapofutwa kazini. Ama wakati mmoja ameenda kunywa pombe kali kiasi kwamba yeye husahau kwamba anatakiwa kwenda kazini, au yeye kubainisha mienendo mibaya mbele ya mkuu wa kazi yake kiasi cha kufukuzwa. Hali hii inapotokea mtu hukosa kazi na kuanza kushirikiana na makundi ya uhalifu kama vile wezi, makahaba, na watu wengine hatari.

Kwa hiyo, ni vyema tuelewe kwamba matumizi ya dawa za kulevya ndilo tatizo kuu ambalo linatakiwa kutafutiwa ufumbuzi kwani ndicho chanzo cha matatizo yote yanayojitokeza miongoni mwa vijana wa leo. Ahsante sana mwenyekiti.

**Mwenyekiti:**

Naam! Waheshimiwa wasikilizaji washiriki! Maoni ya wasemaji wakuu upande wa utetezi yamekwisha kusikilizwa. Sasa ningependa kumkaribisha msemaji mkuu upande wa upinzani ili naye atoe hoja zake.

**Msemaji Mkuu wa 2 (Upinzani):**

Asante sana Mheshimiwa Mwenyekiti! Waheshimiwa wasikilizaji washiriki! Msemaji ambaye ametoa maoni yake amebainisha kwamba matumizi ya dawa za kulevya husababisha matatizo yote yanayowakumba vijana na kwamba likitatuliwa tatizo hilo, matatizo mengine yote yatapata ufumbuzi. Je, ni vijana wangapi ambao wanakosa namna ya kuendeleza miradi yao ya kujiendeleza kwa sababu wao hawana uwezo wa kifedha? Hata kama vijana hawa hawajiingizi katika tabia za kutumia dawa za kulevya wao hukutana na tatizo la umaskini na ambalo halihitaji kukomeshwa kwa kuondosha tatizo la dawa za kulevya ili nalo litatuliwe. Jambo muhimu kwa vijana hawa ni kusaidiwa kupata mitaji inayowawezesha kuanzisha miradi ya maendeleo na kuendeleza taifa kwa ujumla. Ni vyema kwamba serikali yetu imefanya mengi kwa ajili ya kusaidia vijana hao kupata uwezo wa kuanzisha miradi yao, lakini

tatizo lingali linajitokeza na ni muhimu zaidi lishughulikiwe ili kuyaboresha maisha ya vijana wetu.

Tatizo la ukosefu wa uwezo wa kutosha wa kuanzisha miradi ya maendeleo huambatana na lile la ukosefu wa kazi miongoni mwa vijana wanaohitimu masomo yao katika viwango mbalimbali vya elimu. Ieleweke hapa kwamba watu wengi wanaojiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya huwa ni wale ambao hawana kazi. Kwa hivyo, ni lazima watu hawa wasaidiwe kupata kazi ili kupunguza au kumaliza tatizo la wanaotumia dawa za kulevya. Mtu akiwa na kazi hawezi kupata muda wa kwenda kunywa pombe hizo kali au kutamani kitu kingine kinachoweza kuharibu afya yake kwani atakuwa na wajibu wa kutekeleza. Kwa hivyo, wasikilizaji washiriki hamtakosa kuniunga mkono kwamba tatizo la matumizi ya dawa za kulevya ni sehemu ndogo ya matatizo mengine mazito kwani hujitokeza kama mojawapo ya athari au matokeo ya kuendelezwa kwa matatizo mengine makubwa kama vile ukosefu wa kazi na uwezo mdogo wa kuanzisha miradi ya kimaendeleo. Mara tu haya yatakapotatuliwa ndipo tatizo la matumizi ya dawa za kulevya litakapokomeshwa au kupunguzwa. Tufikirie namna ya kusaidia vijana wetu kupata kazi na shughuli nyingine za kuzalisha mali ili waweze kuwa watu muhimu katika jamii nzima. Asante sana mwenyekiti.

**Mwenyekiti:**

Asante sana Wasikilizaji washiriki, watetezi na wapinzani kwa hoja zote zilizotolewa. Mengi yamekwisha semwa na nina imani kwamba wasikilizaji washiriki mmeisha kuyasikiliza maoni ya pande hizi mbili. Sasa ningependa kuzikaribisha hoja zenu kabla ya kumaliza majadiliano. Fursa mwafaka ya kukaribisha hoja zenu. (Mwenyekiti humchagua anaenyoosha mkono kati ya hadhira). Karibu msikilizaji mshiriki pale nyuma.

**Msikilizaji Mshiriki:**

Asante sana Bwana Mwenyekiti. Katika siku hizi, vijana wengi wamejiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya, badala ya kujifunza na kuwasaidia wazazi katika kazi mbalimbali. Vijana hujitumbukiza katika vitendo potovu kama vile unyanyasaji, ukatili, ujambazi na ugomvi kutokana na matumizi ya dawa za kulevya. Vitendo hivi viovu hutokana na ukosefu wa maadili na tabia njema ambazo zingeweza kuwatambulisha vijana waliolelewa vizuri. Pengine, athari za dawa hizi zinapozidi, vijana hugeuka majambazi ya kutisha ambayo hayaogopi kuzibomoa nyumba za watu waliotoa jasho lao kwa kufanya shughuli mbalimbali za kutafuta mali zao. Kwa hivyo, vijana kama hawa, hawawezi kujiendeleza kila wanapozitumia dawa za kulevya. Asante sana mwenyekiti

**Mwenyekiti:**

Asante sana msikilizaji kwa kutoa hoja hizo. Sasa ningependa kukaribisha msikilizaji ambaye ana hoja tofauti ya hizi zilizokwishasemwa. (Mwenyekiti humchagua anayenyoosha mkono kati ya hadhira). Karibu sana msikilizaji mshiriki.

**Msikilizaji wa 5:**

Asante sana Bwana Mwenyekiti. Mawazo yaliyotolewa kutoka upande wa upinzani, yamenikidhi vya kutosha. Ninachoweza kusema kwa kusisitiza yaliyosemwa na upande huo ni kwamba malezi ndiyo msingi wa maendeleo ya vijana wetu. Tukishughulikia sote malezi ya vijana wetu, tutafanikisha maisha yao mema. Kama walivyosema wapinzani wa mada hii, suluhisho tunaloweza kupendekeza ni kuwafundisha vijana wote ili tuwajengee uwezo wa kuboresha maisha yao.

**Mwenyekiti:**

Asante sana wasemaji na ninyi nyote wasikilizaji washiriki. Baada ya kusikiliza mawazo yote muhimu kutoka pande zote mbili, ningependa kumkaribisha katibu wa mdahalo huu ili atusomee muhtasari wa hoja zilizotolewa. Karibu sana katibu wetu.

**Katibu:**

Asante sana Bwana mwenyekiti, wasemaji kutoka pande zote mbili na wasikilizaji washiriki! Huu ni muda mwafaka wa kuwasomea hoja zilizotolewa na pande zote za mdahalo wetu. Upande wa utetezi ulitoa hoja zifuatazo:

- Dawa za kulevya huathiri sana tabia za vijana kimaendeleo na kimwenendo,
- Dawa za kulevya zina madhara hata katika maendeleo ya vijana wa jamii ya leo,
- Wanaotumia dawa za kulevya hujikuta katika hali ya uvivu unaokuwa kikwazo cha maandalizi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo,
- Badala ya kujielimisha na kujiendeleza, vijana wanaotumia dawa za kulevya hujiingiza katika mambo mabaya kama vile ugomvi, ujambazi, umalaya, ukatili, na wizi au udokozi.
- Mtu anapotumia dawa za kulevya hukosa akili timamu inayomwezesha kuwa na mipango mizuri kuhusu maisha yake,
- Mtu anapotumia dawa za kulevya hukosa nguvu za kufanya kazi yoyote katika kulijenga taifa lake,

- Vijana wanaotumia dawa za kulevya huathirika sana kiafya pale ambapo dawa hizi huingia mwilini na kuua kinga ya mwili wake.

Upande wa upinzani umeelezea kwamba badala ya dawa za kulevya, vijana wa leo hukumbwa na matatizo mengine mengi na mazito zaidi kuliko matumizi ya dawa za kulevya. Mawazo yao ni kama haya yafuatayo:

- Matumizi ya teknolojia mpya na mitandao ndilo janga kubwa kwa vijana wetu,
- Umaskini huchochea tabia mbaya mno kama vile uasherati, uzinzi,
- Tabia za uvivu, ukatili, uzinifu, ulevi, ujinga, umaskini, umalaya na uraibu mbaya hutokana na:
    - Ukosefu wa mwenendo mwema na uhaba wa wajibu wa wazazi kuwashauri vijana,
    - Hali ya kutosikilizana kwa wazazi katika familia,
    - Ukosefu wa malezi mema,
    - Hali ya kushirikiana na makundi ya vijana waovu, na kadhalika.

**Mwenyekiti:**

Naam! Baada ya kusikia hoja zote tuko tayari kutangaza upande ulioishawishi hadhira kuliko mwingine. Hivyo basi, ni wakati wa kupiga kura ili tuonyeshe upande ulioshinda. Wanaounga mkono upande wa utetezi nyosheni mikono juu. Bwana katibu, nakuomba uchukue idadi yao. Wasiounga mkono upande wa upinzani nanyi nyosheni mikono. Wasiounga mkono upande wowote nanyi nyosheni mikono juu. Katibu! Tusomee matokeo ya kura.

**Katibu:**

Waliounga mkono upande wa utetezi ni kumi na watatu. Wasiounga mkono upande wa upinzani ni kumi na sita. Wasio na msimamo wowote ni watano.

**Mwenyekiti:**

Mabibi na mabwana kama mlivyoona upande ulioshinda ni ule wa upinzani. (Wasikilizaji washiriki wanawapigia makofi). Na huu ndio mwisho wa mdahalo wetu tukutane siku nyingine kwa mada nyingine. Asanteni. (Hadhira inampigia makofi).

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Ni watu gani wanaotajwa katika mdahalo huu?
2. Ni madhara gani yanayosababishwa na dawa za kulevya.
3. Toa majukumu ya wazazi kuhusu malezi ya watoto wao.
4. Katika sentensi mbili, eleza maoni ya watetezi kuhusu dawa za kulevya.
5. Ni ushauri gani unaowapa watoto wale wanaotumia dawa za kulevya?
6. Ni kitu gani kinachoweza kufanywa ili vijana wajiepushe na matumizi ya dawa za kulevya?
7. Elezea jinsi matumizi ya dawa za kulevya huweza kusababisha umaskini na kutojiendeleza kwa vijana wa leo?
8. Eleza jinsi ambavyo dawa za kulevya huweza kuathiri vijana kiafya?
9. Eleza jinsi ambavyo teknolojia huweza kuwa tatizo miongoni mwa vijana wa leo.
10. Eleza aina ya dawa za kulevya zilizozungumziwa katika mdahalo huu.

### 11.2 Msamiati kuhusu "Mdahalo"

**ZOEZI LA 2:**

***Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo:***

1. Utetezi
2. Upinzani
3. Wajibu
4. Janga
5. Kuhofu
6. Uzinzi
7. Kuzama
8. Johari
9. Kutunukiwa
10. Mdhibiti-muda

## ZOEZI LA 3:

***Jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yafuatayo: kutambulisha, kukukataza,mwafaka, kumbusha, madhara, mitandao, fursa, uliridhika.***

1. Adhabu ninayokupatia ni onyo la kwanza la………………………... kujitoma katika matumizi ya dawa za kulevya.
2. Katika mdahalo ni wajibu wa mwenyekiti ……………………….. makundi yanayoshiriki yaani upande wa utetezi na ule wa upinzani.
3. Ni wajibu wa mwenyekiti tena kuwapa ……………… ya kutoa maoni yao kuhusu mada husika.
4. …………………………..hadhira mada itakayozungumziwa katika midahalo ili wahusika wasiende nje ya mada husika.
5. Kila upande …………………..na kutia saini makubaliano ya amani.
6. Mara nyingi viongozi hupenda kutumia ……………………..ya kijamii wanapotaka kuwajulisha wenzao tukio muhimu.

## ZOEZI LA 4:

***Oanisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B***

| Sehemu ya A | Sehemu ya B |
|---|---|
| 1. Mtaji | a. Kuingia ndani ya maji na kwenda chini baharini au mtoni |
| 2. Kufadhili | b. Hali ya kutokuwa na huruma |
| 3. Uzinifu | c. Mali inayotumika kuanzishia biashara |
| 4. Ukatili | d. Kufanya wema |
| 5. Kuzama | e. zidi mno |
| 6. Pato | f. Kuleta manufaa |
| 7. Uzinzi | g. Kuteketeza |
| 8. Kupindukia | h. Kitu kinachopatikana baada ya kazi fulani |
| 9. Kuangamiza | i. Hali ya ukware |
| 10. Kunufaisha | j. Uasherati |

## 11.3. Sarufi: Matumizi ya Vitenzi vya Silabi Moja

**ZOEZI LA 5:**

***Soma sentensi zifuatazo kisha ubainishe vitenzi jina vilivyoandikwa kwa rangi iliyokolea:***

**MIFANO:**

**Mpe msomaji mkuu fursa ya kutoa hoja zake.**

**Jibu:**Mpe → Kupa

1. **Atakayekula** chakula bila kunawa mikono atakumbwa na magonjwa.
2. Tulipofika baharini, maji yalikuwa **yamekupwa**.
3. Zaidi ya nusu kwa mia **wamekula** ugali na kunywa chai ya rangi.
4. Ningependa kuwaelezea ukweli kwamba mchomea juani **hulia** kivulini.
5. Wewe **umekunywa** chai glasini au kikombeni?
6. Aliamka mapema,akamuamsha dada yake na kumuambia kwamba **kumekucha**.

**ZOEZI LA 6:**

***Eleza sifa kuu ya vitenzi ulivyovibainisha katika zoezi la 5.***

Vitenzi vyenye silabi moja kama vile *(ku)-la, (ku)-fa, (ku)-ja* na vingine huambatanishwa kiambisha ku- katika hali mbalimbali ili sentensi zikubalike kuwa ni sentensi sahihi. Mifano zaidi ya vitenzi vyenye sifa hii ni kama hivi vifuatavyo:

1. **-cha** -: kucha - jua linapochomoza asubuhi k.m kumekucha.
2. **-fa** -: kufa - kuacha kupumua, kupoteza uhai k.m amekufa.
3. **-ja**-: kuja - fika mahali hapa k.m nimekuja.
4. **-la**-: kula - kutia chakula mdomoni k.m anakula.
5. **-nya**-: kunya - kutoa mabaki ya chakula toka tumboni k.m mtoto amekunya.
6. **-nywa**-: kunywa - kutia kinywaji kama vile maji au maziwa mdomoni k.m ninakunywa uji.
7. **-pa**-: kupa - kumkabidhi/kumpatia mtu kitu k.m amenipa pesa.

8. **-pwa-:** kupwa – Kujaa mpaka maji yanatoka ufukoni na kufika sehemu ya mbali ya bahari - k.m maji yamekupwa.

9. **-wa-**: kuwa - kutokea katika hali au mahali fulani k.m alikuwa.

## ZOEZI LA 7:

***Andika hali kanushi ya vitenzi vilivyotumiwa, kisha ueleze tofauti iliyopo kati ya miundo ya vitenzi hivyo katika wakati uliopo na wakati ujao:***

| Hali yakinishi | Hali kanushi |
|---|---|
| 1. Nita**ku**ja kesho | ------------- |
| 2. Nina**ku**nywa chai | -------------- |
| 3. Mimi **hula** mkate | -------------- |
| 4. Nime**ku**nywa maji | ------------- |
| 5. Mama **anakuja** leo | ------------ |

## ZOEZI LA 8:

***Andika vitenzi hivyo katika zoezi la 8 kwa kutumia hali shurutishi.***

**MFANO:**

Mutoni atakula mkate mmoja.

Jibu: Mutoni, kula mkate mmoja

## ZOEZI LA 9:

***Andika mifano mitano ya vitenzi vya silabi moja katika hali shurutishi.***

**MFANO:**

Kunywa chai haraka!

## ZOEZI LA 10:

***Kamilisha sentensi hizi kwa kutumia maneno haya yafuatayo: walikufa, nipe, nile, zijae, walikuja, nilipokuwa, kula, kimeliwa, tuliokuwa, kunywa.***

1. Ninataka ……… mapema ili nitembezwe katika mbuga za wanyama.
2. Gari la Bwana Gatabazi lilipopata ajali, waliokuwa ndani wote …….
3. Wanafunzi wa upwa wa ziwa la Kivu hupenda ……………. samaki.
4. Alishindwa kupata uji akachagua ………….. maziwa bila sukari.
5. …………....kitabu hicho ili niangalie kama kuna mfano wa mdahalo.
6. Unatakiwa kuchota hadi pipa zile …………………maji.
7. Juzi ……..kazini, nilimsaidia mwenzangu Kamali kutunga mdahalo.
8. Chakula kingine ……………………..na wageni.
9. Hawa ndio wageni ………………………..tukiwangojea kwa hamu.
10. Wageni wale .................... jana ili kushiriki mkutano wetu.

## ZOEZI LA 11:

***Tumia vitenzi katika mabano kwa kukamilisha sentensi zifuatazo:***

1. Tume…………chakula chetu baada ya shughuli zetu za kufanya biashara (kula).
2. Mpenzi wangu ………………………kutokana na kidonda moyoni mwake (kufa).
3. Kalisa hupenda …………chai katika kikombe cha udongo kila asubuhi(Kunywa).
4. Kila kukiwa……… huianza siku yangu kwa kumuomba Mwenyezi Mungu anisaidie na kunilinda siku nzima. (kucha)
5. Mtoto alipoongea na mamaye hakuamini alivyoelezwa kuhusu……………..nyumbani likizoni (kuja).

### 11.4. Matumizi ya lugha: Maandalizi na Utekelezaji wa Mdahalo

## ZOEZI LA 12:

***Soma maelezo yafuatayo kuhusu maandalizi na utekelezaji wa mdahalo kisha ujibu maswali yanayofuata:***

Mdahalo ni majadiliano kati ya watu wengi wenye misimamo tofauti. Yafuatayo ni mambo muhimu ya kuzingatia katika maandalizi na utekelezaji wake:

**Maandalizi:**

a. Kuchagua mada ya kuzungumzia katika mdahalo: uchaguzi huu hufanyika kwa kupiga kura.
b. Kumchagua mwenyekiti wa mdahalo: mwenyekiti huchaguliwa kwa kupiga kura na atakayechaguliwa ni yule mwenye uwezo wa kuongoza na kuendesha mdahalo.
c. Kumchagua katibu wa mdahalo: mhusika huyu pia huchaguliwa. Yeye ana wajibu wa kuandika na kuwasomea hadhira matokeo ya mdahalo.
d. Kumchagua mdhibiti-muda: huyu ana jukumu la kuchunguza kwamba kila mhusika anatumia muda wake wa kutoa hoja zake ipasavyo.
e. Kupanga wahusika kwa upande wa utetezi na upande wa upinzani kama wasemaji wakuu wa pande hizo.
f. Kupanga namna ya kukaa kwa wahusika wa mdahalo upande wa utetezi na upande wa upinzani. Kitendo hiki huwafanya wahusika wakae pande mbili (upande wa kulia na upande wa kushoto) ambapo watabadilishana mawazo kwa urahisi.
g. Kupanga muda utakaotumiwa na wahusika wa pande hizo mbili.

**Utekelezaji wa mdahalo**

a. Mwenyekiti hufungua mdahalo kwa kuwatambulisha wahusika wa mdahalo akianzia kwake kama kiongozi wa mdahalo kisha katibu na washiriki wa pande mbili zitakazojadiliana yaani upande wa utetezi na upande wa upinzani.
b. Kabla ya kuanza kutoa hoja za pande mbili husika mwenyekiti huwakumbusha mada mahsusi itakayozungumziwa.
c. Mwenyekiti huwapatia wahusika wasikilizaji muda wa kutoa maoni yao kuhusu mada iliyokuwa inazungumziwa.
d. Kila mhusika hutakiwa kuheshimu muda wake wa kutetea au kupinga mada husika na muda wa kunyamaza kwa kusikiliza hoja za wengine.
e. Mwenyekiti huwapatia wasikilizaji washiriki muda wa kutoa maoni kuhusu mada inayojadiliwa.
f. Wahusika hupaswa kuheshimu amri ya mwenyekiti na kupata uamuzi maalum.
g. Mwenyekiti humpatia katibu fursa ya kuwasomea alivyoandika kama

matokeo ya mdahalo.

h. Mwenyekiti huongoza zoezi la kupiga kura na kumuomba katibu aandike idadi ya kura kwa kila upande ili kuonyesha upande ulioibuka na ushindi na ule ulioshindwa.

i. Mwenyekiti hutangaza matokeo ya kura na kuwapongeza waliohudhuria na kufunga mdahalo.

**Maswali**

1. Toa kanuni zinazoongoza maandalizi ya mdahalo.
2. Ni njia gani zinazotumiwa katika utekelezaji wa mdahalo.
3. Taja mifano mitatu ya mada zinazoweza kujadiliwa katika mdahalo.
4. Mdahalo ni zoezi zuri kwa anayetaka kukuza uwezo wake wa lugha. Jadili.

## ZOEZI LA 13:

***Panga maneno yafuatayo kwa sentensi sahihi:***

1. Watu/ni/mdahalo/juu/baina/jambo/ya/wengi/ya/maalum/majadiliano/moja.
2. Kazi/mdahalo/kutoa/wakuu/na/za/wazungumzaji/mada/katika/maoni/huwa/yao/fulani/kuhusu.
3. Huzingatia/wapinzani/mdahalo/utekelezaji/mwenyekiti/makao/ya/na/katibu/watetezi/wa/wake/tena/na.
4. Hukimbia/bongo/gongo/likiingia.
5. Ulevi/penye/ndipo/matata/penye.
6. Hatari/penye/ndipo/mvinyo/penye.
7. Mlevi/cha/na/huliwa/mgema.

## ZOEZI LA 14:

***Tafuta maneno kumi na mawili yenye maana kamili katika mraba wa hapo chini.***

**MIFANO:**

1. Jibu.

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | A | W | A | Z | O | X | T | K | U | I |
| I | N | A | M | R | I | R | T | U | T | O |
| N | A | **J** | I | B | U | K | E | H | U | T |
| A | S | **I** | K | M | D | A | H | A | L | O |
| J | Y | **B** | C | M | B | M | A | K | A | O |
| I | T | **U** | H | R | U | M | Y | I | O | E |
| L | Z | W | K | H | A | K | I | K | A | J |
| I | T | I | K | A | D | I | W | I | S | O |
| A | H | K | Y | K | U | H | U | S | U | I |
| E | T | N | M | H | O | J | A | H | G | T |
| M | A | J | A | D | I | L | I | A | N | O |

## 11.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Mdahalo

**ZOEZI LA 15:**

***Andaa mdahalo wenye moja ya mada zinazofuata:***

1. Utalii ni nguzo muhimu katika ujenzi wa nchi yetu.
2. Mali bila daftari hupotea bila habari.

## 11.6. Kuandika: Uandishi wa Mdahalo

**ZOEZI LA 16:**

***chagua mada moja kati ya hizi hapa chini kisha utayarishe mdahalo:***

1. Matumizi ya teknolojia mpya ndiyo nguzo muhimu ya kurahisisha maendeleo ya jamii.
2. Kujiunga pamoja katika vyama vya kuzalisha mali hutajirisha.

# SOMO LA 12: MJADALA

## ZOEZI LA 1:

***Jibu maswali haya yanayofuata:***

1. Nini maana ya mjadala?
2. Ni watu wangapi wanaoongoza mjadala?
3. Kwa kuzingatia mambo uliyojifunza katika kidato cha tatu kuhusu mjadala, eleza tofauti iliyopo kati ya mjadala na mdahalo.

## 12.1. Kusoma na Ufahamu: Maana ya Mjadala

*Soma kifungu kuhusu* «Maana ya Mjadala» *ili ujibu maswali yaliyotolewa hapo chini.*

Kuna mazungumzo ambayo hufanywa kuhusu suala fulani linalohitaji kujadiliwa na kutafutiwa ufumbuzi. Mazungumzo ya aina hii ndiyo hujulikana kwa jina la mijadala. Kwa kawaida, mjadala ni mazungumzo juu ya jambo maalum ambayo hufanywa na watu kwa kutoa hoja zao kwa jambo fulani linalotakiwa ufafanuzi au ufumbuzi wa suala lililopo.

Mjadala ni aina ya majadiliano ambayo huhusisha watu wengi wanaotoa hoja kuhusu mada fulani. Miongoni mwa watu wanaohusika katika mjadala huwa kuna kiongozi ambaye jukumu lake ni kuongoza majadiliano kwa kupanga muda wa kuzungumza kwa kila msemaji anayeshiriki katika mazungumzo hayo. Katika mjadala, hakuna msemaji ambaye anaruhusiwa kutoa hoja bila kumuomba fursa kiongozi wa majadiliano.

Mjadala huwa na mada ambayo humulika hoja zote zinazotolewa wakati wa mazungumzo. Kama kuna wasemaji ambao wanataka kukiuka mada katika hoja zao, kiongozi wa mjadala huwarekebisha kwa kuwakumbusha mada inayotolewa hoja.

Mjadala huwa na malengo ya kukuza uwezo wa kitaaluma na hali ya udadisi kwa washiriki wa majadiliano. Mjadala hukuza uwezo wa kushawishi watu hadharani ili wakubaliane na mawazo ya msemaji kuhusu jambo fulani. Aidha, humwezesha mtu kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri wakati anapoandika insha au habari. Mjadala pia humsaidia mtu kutambua kipaji alicho nacho cha kuzungumza bila aibu mbele ya hadhira na kukuza stadi ya utumiaji wa lugha kwa kutumia msamiati na matamshi bora ya lugha. Humzoeza pia mtu kusikiliza maoni ya watu wengine, kupinga au kutetea maoni na hoja zao. Jambo muhimu ni kwamba majadiliano haya humpa fursa ya kuelewana na watu anaotofautiana nao kimawazo.

Wazungumzaji wanapofanya mjadala hukuza uwezo wao wa mazungumzo kuhusu suala fulani na hupanua kiwango chao cha msamiati na hupunguza uoga wa kuongea hadharani. Vilevile, mjadala hutumiwa kama wenzo bora wa kutatua migogoro inayoweza kuzuka miongoni mwa wanajamii. Katika mjadala, watu wenye mawazo yaliyo kinyume na mada, hupata nafasi ya kujadiliana juu ya jambo fulani kwa madhumuni ya kutatua tatizo linalowakumba. Mjadala hutumiwa kwa kutatua tatizo na kuondoa migogoro miongoni mwa watu kwa njia ya amani.

Katika mjadala, kama tulivyokwisha kusema, kunajitokeza wahusika ambao ni kiongozi wa mjadala na hadhira. Kiongozi ndiye ambaye ana jukumu la kuongoza mjadala. Kiongozi anaweza kuwa mtu mmoja au wawili kulingana na mada iliyochaguliwa au malengo ya majadiliano yenyewe. Ukichaguliwa kama kiongozi ni lazima uongoze mjadala ipasavyo na usikose kumpangia kila msemaji muda atakaotumia ili aweze kuchangia mawazo yake.

Kwa upande wa mjadala, kiongozi humruhusu yeyote atakaye kutoa mchango kwani hakuna makundi ya watetezi na wapinzani wa mjadala. Kiongozi huyu huwa na majukumu tofauti kwani ndiye anayetoa muhtasari wa mawazo yaliyotolewa.

Katika mjadala, kuna hadhira pia ambayo hushiriki katika mazungumzo kwa kusikiliza na kutoa mchango wao kuhusu suala linalojadiliwa. Kila mtu aliye na hoja hunyosha mkono kuomba fursa ya kuzungumza. Lengo la kwanza la kila msemaji katika mjadala si kupata ushindi, kwani si mashindano bali lengo la kila msemaji ni kutoa mawazo kwa nia ya kutatua tatizo fulani linalofafanuliwa na kujadiliwa kwa pamoja. Hivyo, katika mjadala hakuna kushindania ushindi; kila mtu ambaye ana la kusema huruhusiwa na hutoa hoja kama apendavyo kuhusu mada ile inayohusika bila kukiuka taratibu zilizowekwa.

Watu wanaoshiriki katika mijadala huhakikisha kuwa mjadala ni njia ya kukuza uwezo wa kufikiri na kutafuta masuluhisho kwa masuala yanayoikumba jamii fulani. Katika mazungumzo haya, kiongozi ndiye anaongoza majadiliano ili wazungumzaji watoe mchango wao kuhusu suala lililopo. Kiongozi humpa fursa mzungumzaji kwa kusema, "Simama utoe mchango wako." Mzungumzaji huweza kutoa hoja zake kulingana na jinsi anavyofikiria kuhusu suala husika. Mara nyingi, mjadala huweza kufanyika katika makundi madogo madogo au makubwa. Kiongozi hubainisha mada ya mjadala na kuhakikisha kuwa wakati wote wa mjadala kuna mwenendo mwema unaowaongoza washiriki wa mjadala husika. Mzungumzaji katika mjadala ni lazima awe na uwezo wa kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri. Yeye anakuza ustadi wa utumiaji wa lugha kwa kuwa anaweza kuutumia msamiati na kujizoeza kutumia matamshi mazuri ya lugha.

Jambo muhimu pia katika mijadala inayofanywa ni kwamba mazungumzo yanayofanywa huwazoeza wengi kusikiliza na kupima maoni na hoja za wenzao, kuelewana na wengine kutoka sehemu mbalimbali, kuheshimiana

kulingana na mawazo tofauti yanayotolewa na kila mzungumzaji.

Kwa hiyo, mjadala ni zoezi zuri kwa yeyote anayetaka kukuza uwezo wa mawasiliano, majadiliano, mahojiano, ujuzi wa kutoa maoni yake na kujitambua katika jamii yake.

Mwisho, mjadala ni mazungumzo yanayoendeshwa na kushirikisha watu tofauti kwa kukidhi haja na malengo yanayotofautiana na kuingiliana kwa upande mwingine. Ni lazima kuelewa kuwa mjadala ni nyenzo timamu za kuimarisha ustadi wa maongezi kuhusu mada fulani.

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Eleza kwa ufupi maana ya mjadala.
2. Katika mjadala, kiongozi ana kazi gani?
3. Toa hoja tatu kuhusu umuhimu wa mjadala.
4. Washiriki katika mjadala ni wa aina ngapi? Wataje.
5. Ni ipi kazi ya hadhira katika mjadala?
6. Lengo la kila msemaji katika mjadala ni lipi?
7. Toa angalau mifano mitatu ya mambo yanayoweza kujadiliwa katika mjadala.
8. Mjadala husaidiaje kujua lugha?
9. Ni maadili yapi yanayojengeka kupitia mijadala?
10. Mjadala ni zoezi zuri kwa anayetaka kukuza uwezo wa mawasiliano, majadiliano na mahojiano. Jadili.

### 12.2. Msamiati kuhusu Maana ya Mjadala

## ZOEZI LA 2:

***Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo:***

1. ufumbuzi
2. migogoro
3. suala
4. kiongozi
5. hoja
6. jukumu
7. mchango
8. majadiliano
9. hadhira

## ZOEZI LA 3:

***Ambatanisha maneno katika kundi A na maelezo yake katika kundi B:***

| Kundi A | Kundi B |
|---|---|
| **1. mazungumzo** | a. Nafasi ya kuweza kufanya jambo. |
| **2. mijadala** | b. Kusimamia mtu ili kumkinga na mambo, aghalabu mabaya, yaliyomfikia. |
| **3. ufafanuzi** | c. Mtu aliye hodari wa kusema. |
| **4. kuongoza** | d. Kusawazisha, kusahihisha. |
| **5. msemaji** | e. Mapambano baina ya pande mbili au zaidi k.v. katika michezo, ngoma au maneno. |
| **6. fursa** | f. Mkusanyiko wa watu kadhaa. |
| **7. kurekebisha** | g. Kuwa mkuu au msimamizi wa kazi au shughuli nyingine yoyote. |
| **8. uwezo** | h. Jambo linalojadiliwa na watu au kikundi cha watu kwa lengo fulani. |
| **9. hadharani** | i. Maneno yaonyeshayo fikira za mtu juu ya jambo fulani. |
| **10. maoni** | j. Maelezo yanayotolewa ili kuweka jambo wazi. |
| **11. kutetea** | k. Hali ya kuweza kufanya jambo. |
| **12. mashindano** | l. Mazungumzo juu ya jambo maalumu yanayofanywa kwa kutolea hoja kuhusu jambo hilo. |

## ZOEZI LA 4:

***Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yanayofaa kati ya haya yafuatayo: kuwashirikisha, mjadala, kupanga, mazungumzo, hoja, kiongozi, fursa, mada, kipaji, mahojiano, hadhira.***

1. Mjadala humsaidia mtu kutambua …………alichonacho cha kuzungumza bila woga mbele ya wengine.
2. Aliyechaguliwa kuongoza majadiliano kwa kupanga muda wa kuzungumza kwa kila msemaji huitwa ………………..
3. . ……………..ni jumla ya wasikilizaji au wasomaji wa kazi maalumu.
4. Katika mazungumzo lazima …………………mawazo kwa mfuatano mzuri.
5. Uulizaji maswali ili kufahamu maarifa anayojua mtu hujulikana kama………………………..
6. . ………………… unahitajika kwa wanaohitaji ufafanuzi zaidi.
7. Mjadala huchukuliwa kama …………………juu ya jambo maalumu.
8. Watu wengi wanapojadiliana kuhusu mada fulani hutoa ………….. ambazo husaidia wengine kuelewa ukweli fulani.
9. Mtu yeyote aliyehudhuria mkutano alipewa …………………ya kufanya jambo fulani.
10. Mwalimu anaweza ……….wanafunzi katika uchaguzi wa mada.
11. Kitu muhimu kinachojitokeza katika mjadala ni ................. ya kuzugumzia.

### 12.3. Sarufi: Hali Shurutishi ya Vitenzi

## ZOEZI LA 5 :

***Orodhesha vitenzi vyote ambavyo huishia na kiambishi tamati kisichokuwa -a katika kifungu «Maana ya Mjadala.» Vitenzi ulivyoorodhesha unadhani ni vya aina gani? Eleza jibu lako.***

Vitenzi vyenye asili kutoka kwa lugha nyingine badala ya kibantu hujulikana kama **vitenzi vya kigeni**. Baadhi ya lugha hizo ni Kiarabu, Kizungu, Kireno, Kihispania, n.k. Vitenzi hivi havifuatilii muundo wa kawaida wa vitenzi vya Kiswahili ambavyo huishia kwa kiambishi tamati **-a**. Badala yake, vitenzi hivi huishia kwa sauti nyingine kama vile **-e**, -**i**, **-o** na **u.**

**MIFANO:**

***haribu, tubu, shukuru, salimu, thamini, amini, samehe, baleghe (balehe).***

- Katika hali ya kushurutisha au ya kuamrisha, vitenzi vya aina hii huondolewa kiambishi awali cha kitenzi **ku-**. Katika wingi, vitenzi hivi huondolewa kiambishi **ku-** pamoja na kiambishi tamati, halafu vikachukua kiambishi -ni badala ya kiambishi tamati -a.

| Umoja | Wingi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|---|
| Rudi | Rudini | Ahidi | Ahidini |
| Hisi | Hisini | Dharau | Dharauni |
| Sifu | Sifuni | Furahi | Furahini |
| Abudu | Abuduni | Kubali | Kubalini |
| Afiki | Afikini | Sali | Salini |

- Vilevile katika hali kanushi, hupachika kiambishi cha kukanusha -si- baada ya kiambishi awali.

**Tanbihi: Kiambishi tamati -ni cha wingi hakitumiki katika hali kanushi wingi.**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Usiharibu | Msiharibu |
| Usitubu | Msitubu |
| Usishukuru | Msishukuru |
| Usithamini | Msithamini |
| Usiamini | Msiamini |
| Usisamahe | Msisamehe |

**ZOEZI LA 6 :**

***Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia hali ya kushurutisha ya vitenzi ulivyopewa mabanoni.***

**MIFANO:**

Mzazi aliwashauri watoto wake: "……………….mmoja kwa mwingine." (kupenda)

**Jibu:** Mzazi aliwashauri watoto wake: "**pendaneni** mmoja kwa mwingine."

1. ……………………….mijadala kwa sababu hoja za kila mtu zinahitajika. (kuheshimu)

2. Kiongozi wa mjadala aliwaomba washiriki: "…………kutoa mawazo kuhusu mada husika." (kusaidia)

3. Mwalimu alimuomba mwanafunzi akisema: "……………ratiba ya masomo yenu."(kupanga)

4. "……………….na wengine kwani tuna uhaba wa vitabu shuleni" Mwalimu alisema. (kusoma)

5. Katika majadiliano unganisha mawazo ipasavyo. ………………… katika kutoa hoja. (kutetea)

6. Mlitoa maoni mazuri kuhusu mada yenyewe. …………………….. makofi msaidiane.(kupigia)

7. Kiongozi wa shule aliwaambia: "………….barua za kirafiki kwa kukuza uhusiano." (andika)

8. ……………………...tabia ya kujifanya unajua kila kitu. (kudharau)

9. …………………………..na wanaotenda mema kwa hiari. (kushiriki)

## 12.4. Matumizi ya Lugha: Maana ya Mjadala

**ZOEZI LA 7 :**

***Soma maelezo yanayofuata ili kujibu maswali hapo chini.***

**"Maana ya mjadala"**

- Mjadala ni mazugumzo juu ya jambo fulani. Yanaweza kufanyika katika makundi madogo madogo au makubwa.
- Mjadala unaongozwa na mtu mmoja au watu wawili ambao wanazusha mawazo na kuhakikisha ikiwa kuna mwenendo mwema kati ya washiriki wa mjadala huo.

- Kiongozi wa mjadala ndiye anayetoa muhtasari wa mawazo yaliyotolewa. Mada zinazojadiliwa katika mjadala ni zile ambazo zinahitaji ufafanuzi kutokana na mchango wa mawazo ya wengi.
- Anayetoa hoja yake, anaweza kuunga mkono maoni ya mwenzake au kuyapinga kwa minajili ya kutoa mchango wake wa kutatua tatizo linalojadiliwa.
- Katika mjadala, mada hutolewa mawazo na ndiyo inayomulikia mjadala. Kiongozi wa mjadala hulazimika kuwasaidia wasemaji kutokiuka mada.
- Mdahalo huwa na malengo yafuatayo:
    - Kukuza uwezo wa kitaaluma na hali ya udadisi kwa washiriki wa mjadala.
    - Kukuza uwezo wa kushawishi watu hadharani ili wakubaliane na mawazo ya msemaji kuhusu jambo fulani.
    - Kumwezesha mtu kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri wakati anapoandika insha au habari.
    - Kumwezesha mtu kutambua kipaji alichonacho cha kuzungumza bila aibu mbele ya hadhira.
    - Kukuza stadi ya utumiaji wa lugha kwa kutumia msamiati na matamshi bora ya lugha.
    - Kumzoeza mtu kusikiliza na kupinga au kutetea maoni na hoja za wengine.
    - Kuwapa watu wasaa wa kuelewana na wengine kutoka maeneo mbalimbali.
- Wahusika katika mdahalo ni kiongozi na hadhira.
- Katika mjadala kila yeyote anayetaka kutoa hoja anaruhusiwa kutoa hoja yake na kiongozi.
- Katika mjadala hakuna washindi. Kiongozi anatoa suluhisho kutokana na mawazo yaliyotolewa. Mjadala si mashindano.

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Mjadala unaweza kuongozwa na watu watano. Ni kweli au si kweli? Eleza.
2. Ni ipi kazi ya kiongozi katika mjadala?
3. Jadili malengo matatu ya mjadala mzuri.
4. Kwa sababu gani katika mjadala hakuna mshindi?
5. Jadili wahusika katika mjadala.

## ZOEZI LA 8 :

***Unda sentensi sahihi kwa kutumia maneno uliyopewa hapo chini.***

1. wa/hukuza/hadhira/watu/mjadala/katika/uwezo/kushawishi.
2. kuelewana/mbalimbali/ya/hutupa/sehemu/na/mawasiliano/wenzetu/kutoka/fursa.
3. utakiwapo/kupanga/hoja/mawazo/ni/kutoa/lazima.
4. yake/maoni/msemaji/anaporuhusiwa/hutoa.
5. hajielimishi/wakati/mtu/ambapo/kujiendeleza/hawezi.

## 12.5. Kusikiliza na Kuzungumza

## ZOEZI LA 9:

***Jadili mada zifuatazo:***

1. Maendeleo nchini huyafanya maisha ya Wanyarwanda yabadilike kwa kiwango cha juu.
2. Mikakati ya kuepuka maambukizi na kujikinga na ugonjwa wa malaria.

## 12.6. Utungaji

## ZOEZI LA 10:

***Tayarisha mjadala kuhusu mada zifuatazo:***

1. Ubaya wa dawa za kulevya katika maisha ya binadamu.
2. Mtu ambaye hasikii ushauri mwema wa wakubwa, hupata hasara kubwa.

## SOMO LA 13: MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA MJADALA



**ZOEZI LA 1:**

***Tazama mchoro hapo juu kisha ujadili unayoyaona yanatendeka kwenye mchoro husika.***

### 13.1. Mjadala kuhusu: "Mchango wa Wazazi katika Malezi ya Watoto Wao"

**Kiongozi:**

Waheshimiwa mabibi na mabwana mliokusanyika hapa, kwanza ninataka niwakaribishe katika mjadala huu. Kama mnavyotuona hapa mbele yenu, mimi ninayewakaribisha ni kiongozi wa mjadala huu. Pembeni mwangu mnayemwona ni kiongozi msaidizi. Mada ya mjadala wetu wa leo ni kama mnavyoisoma mbele yenu "**MCHANGO WA WAZAZI KATIKA MALEZI YA WATOTO WAO.**" Karibuni sana nyote na bila kupoteza muda, ningetaka kumkaribisha mshiriki aliye tayari atoe mchango wake.

**Mshiriki wa kwanza:**

Ninawashukuru sana viongozi na wasikilizaji washiriki wenzangu. Ni kweli kabisa wazazi ndio wenye jukumu la kwanza katika malezi ya watoto wao. Kama inavyojulikana malezi ya kwanza kwa mtoto huanzia nyumbani. Nyumbani ndipo mtoto anapopata malezi ya msingi ambayo humulikia maisha yake. Malezi haya ya kwanza yapatikanayo nyumbani humsaidia mtoto kufanikiwa katika maisha yake. Malezi haya yanatolewa na wazazi ambao ndio walezi muhimu wa watoto wao. Bila mchango wa wazazi, watoto hawawezi kupata elimu. Kwa hiyo, wazazi wana jukumu la kwanza katika

malezi ya watoto wao. Ahsanteni kwa kunitega sikio.

**Kiongozi:**

Asante sana kwa hoja yako. Kama mlivyosikia, msemaji huyu ameeleza kwamba wazazi ndio wanaowapatia watoto wao malezi ya msingi ambayo yanawasaidia kufanikiwa maishani mwao. Tafadhali, naomba mjaribu kutoa maoni mengine kuhusu suala hilo. Karibu bibi!

**Mshiriki wa pili:**

Asante sana kiongozi kwa fursa hii ya kuniruhusu kutoa mchango wangu. Kwa maoni yangu, ni kweli wazazi wana nafasi kubwa katika malezi ya watoto wao. Lakini, kuna matatizo makuu ambayo wazazi hawatilii mkazo katika malezi hayo. Chunguza jinsi watoto na vijana wengine wanavyotumia dawa za kulevya. Siku hizi, idadi ya wanaokumbwa na matumizi ya dawa za kulevya huzidi kuongezeka. Wazazi wenzangu, mjue kwamba dawa za kulevya ni hatari sana kwa binadamu. Dawa hizi husababisha magonjwa mengi na huharibu ubongo wa watoto. Kwa upande wangu, kila mzazi lazima ashiriki katika malezi ya watoto wote anaokutana nao badala ya kufikiria watoto wake tu. Wazazi wote wakilititilia maanani suala hili, tatizo hili lingemalizika haraka sana na watoto wetu wakawa na maisha mazuri.

**Kiongozi:**

Ninamshukuru sana mshiriki kwa maoni yake. Anaeleza kwamba wazazi hawazingatii wajibu wao kwa kutoa mchango wao kukomesha matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana. Anaeleza pia kwamba malezi ya mtoto ni jukumu la kila mtu. Tunamshukuru sana. Hebu, tumsikilize pia mshiriki yule anayenyosha mkono pale ili naye atoe hoja zake.

**Mshiriki wa tatu:**

Mheshimiwa kiongozi na wasikilizaji washiriki wenzangu, watu ambao wako karibu sana na watoto ni wazazi wao ambao wana mchango wa kwanza katika malezi ya watoto hao. Wao huwatunza watoto wao, tangu wanapozaliwa na wakati wa kwenda shule unapofika, wao ndio wanapiga hatua ya kwanza kuwapeleka shuleni.

Wajibu wa kila mzazi ni kupeleka mtoto wake shuleni kwani anapata mwenendo mwema utakaomsaidia maishani mwake. Watoto wanapofika shuleni, ni vyema wazazi wao wawajibike kufuatilia malezi ya watoto wao kwa kuwashauri, kuwafundisha kuwa na mienendo mizuri, kuwanunulia vifaa vya shule na kuwalipia karo. Waheshimiwa wasikilizaji, kama mnavyoelewa, bila mchango wa wazazi, watoto hawawezi kupata elimu inayotolewa shuleni kwani wao ndio wanarahisisha kila jambo linalotendewa mtoto, awe shuleni,

nyumbani na mahali pengine. Asante sana kwa kunitega sikio. Hayo ndiyo maoni yangu.

**Kiongozi:**

Waheshimiwa wasikilizaji washiriki, mawazo hayo ya mwenzetu mmeyasikia. Sasa ninataka kumkaribisha msemaji mwingine yeyote ambaye ana la kusema ili naye atoe mchango wake kwa ufumbuzi wa suala letu. Karibu sana bibi.

**Mshiriki wa nne:**

Asante sana kiongozi na wasikilizaji washiriki kwa kunipa fursa hii. Wapendwa wasikilizaji washiriki, taifa letu hufanya mengi ili iweze kukomesha matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa wananchi. Kwa nini wazazi tusiwasaidie viongozi wetu kupambana na tatizo hili ili tupige marufuku dawa za kulevya ambazo huangamiza maisha ya watoto wetu? Serikali yetu imechukua uamuzi mzuri wa kuanzisha mradi wa elimu kwa wote ambapo kila mtoto anapelekwa shuleni akaendelea na masomo yake mpaka anapomaliza shule za sekondari.

Kwa hivyo, ni lazima walimu na viongozi wa shule waelewe kwamba wanahitaji kushirikiana na wazazi ili waweze kutimiza wajibu wao mkubwa wa kubadilisha mienendo ya vijana wanaowalea hasa vijana wale wanaopatikana wakitumia dawa za kulevya. Bila mchango wa wazazi kwa vijana hao, shule zetu haziwezi kufanikiwa kuwapatia watoto hao maadili yanayotakiwa. Kwa mfano, utamkuta kijana mmoja akikosekana shuleni kwa siku moja au mbili na akifika huwadanganya viongozi kwamba alikuwa ameenda nyumbani na viongozi hawa hukubali bila kuuliza wazazi wa mtoto huyo kuhusu ukweli wa yale aliyosingizia. Kwa kumaliza, ni vyema kila mtu anayehusika na malezi ya watoto awe mwalimu, kiongozi wa shule na hata majirani waelewe kwamba wazazi wana nafasi kubwa katika urekebishaji wa mienendo mibaya ya watoto wetu.  Asante sana kwa kunitega sikio.

**Kiongozi:**

Ninamshukuru mshiriki mwenzetu kwa maelezo yake ambayo yamewagusa wengi. Yeye amesema kwamba ni lazima kuisaidia serikali katika kulinda watoto wetu dawa za kulevya. Ameeleza pia kwamba kila mtu anayehusika na malezi ya watoto aitambue kwanza nafasi ya wazazi kwa kujaribu kuwashirikisha kwa kila uamuzi kuhusu mienendo na tabia za watoto wao. Kwa hivyo, tunamshukuru sana kwa mawazo yake.

Kama mnavyoona, mengi yamekwishaelezwa na muda unazidi kuyoyoma.

Hebu nichukue fursa hii kuwakaribisha washiriki wengine wawili kabla ya kutamatisha mjadala wetu. Karibu sana.

**Mshiriki wa tano:**

Asante sana kiongozi kwa kunipa muda huu ili nami nitoe maoni yangu. Washiriki wenzangu, mawazo yaliyotolewa na waliotangulia ni mazuri sana na yanaeleweka waziwazi. Ni ukweli mtupu kwamba wazazi ndio wenye jukumu la kwanza katika malezi ya watoto wao na ndiyo maana wahenga walisema, "Mtoto hutazama kisogo cha mama yake." Mzazi ni mfano unaoigwa na mtoto wake. Kama mzazi ana tabia nzuri mtoto naye bila shaka ataathiriwa vizuri na itakuwa kinyume kama mzazi ana tabia zisizopendeza. Kwa hivyo, mimi ningependa kuhimiza wazazi wote kukuza na kuendeleza tabia nzuri mbele ya watoto wao ili waweze kuigwa na kutumiwa kama mifano mizuri kwa malezi ya watoto wao kwani mtu hutoa kile alichonacho na pia huvuna kile alichopanda. Asanteni.

**Kiongozi:**

Asante sana mshiriki kwa mawazo yako mazuri. Naona kuna wengine wanaonyosha mikono yao ili kutoa michango yao kuhusu suala letu. Lakini, hebu tumsikilize mzazi yule ili tukamilishe mazungumzo yetu. Karibu sana.

**Mshiriki wa sita:**

Kiongozi na wasikilizaji washiriki wenzangu! Ni lazima tuelewe kwamba mtoto hulelewa na watu wote wanaomzunguka kwani hawa nao wana nafasi kubwa kwa kumwathiri vizuri au vibaya kulingana na mienendo na tabia zao. Mtoto afikapo shuleni, malezi yake huwa zaidi mikononi mwa walimu na viongozi wa shule ambao hufanya kazi kubwa ya kuwalea watoto na kuwaelimisha. Watoto humaliza muda mrefu mikononi mwa walimu na viongozi wa shule wanaomsaidia kurekebisha tabia mbaya na kuendeleza tabia nzuri huku wakimpa elimu itakayomfaa katika maisha yake. Mbali na hayo, mtoto akitembea barabarani, njiani na akienda kwingine anakotumwa na wazazi wake hukutana na watu ambao si wazazi wake. Mtoto akipewa ruhusa ya kwenda kuangalia familia yake pana hukutana na watoto wengine katika familia hizo na hata watu wengine ambao si wazazi wake.

Kwa hivyo, mimi naona kuwa watu wote wanamzunguka mtoto kuanzia wale wanaokaa naye nyumbani kama vile wazazi wake, ndugu zake na watumishi wa nyumbani, majirani na wengine ambao hukutana naye nao wanaweza kuathiri sana malezi ya mtoto na hata kuliko wazazi wake wanavyoweza kufanya. Ni mara ngapi tunasikia habari kwamba watoto wameathiriwa na watumishi wa nyumbani kwa kujiingiza katika vitendo na mienendo mibaya kama vile uzinzi, ulevi, matumizi ya maneno yasiyo na maadili, na kadhalika!

Haya yote yanathibitisha kwamba malezi ya watato yanahusu watu wote wanaomzunguka mtoto huyo na kwamba wito unapaswa kutolewa kwao ili watambue wajibu wao kumlea mtoto.

Wazazi humwelekeza mtoto wakati angali mchanga lakini aanzapo kwenda shuleni na kukutana na watu wengine, nafasi ya wazazi katika malezi yao huendelea lakini wanaomwathiri zaidi huwa ni watu wote anaokutana nao katika shughuli zake mbalimbali. Asante sana kwa kunitega sikio; hayo ndiyo yamekuwa maoni yangu.

**Kiongozi:**

Ninakushukuru sana kwa maelezo yako. Nasikia kwamba wewe unatilia mkazo kwamba watu wote wanapaswa kutoa mchango wao kwa kumlea mtoto badala ya kufikiria kwamba wazazi ndio wenye nafasi kubwa. Asante sana kwa mawazo hayo. Inaonekana kwamba watu wengi wangependa kutoa mchango wao lakini muda wetu hauturuhusu kuendelea kusikiliza hoja nyingine. Mjadala wetu unakaribia kufikia mwisho na ningependa kuwapongeza ninyi nyote kwa maoni na mawazo mazuri ambayo mmeyatoa katika mjadala huu. Asante sana kwa wote mlioshiriki katika mjadala huu. Kichwa cha mjadala wa leo kimekuwa **"MCHANGO WA WAZAZI KATIKA MALEZI YA WATOTO WAO."**

Miongoni mwa hoja mlizozitoa ni kwamba ni wajibu wa wazazi kuwalinda watoto kutumia dawa za kulevya, kuwapeleka watoto shuleni na kufuatilia masomo na mienendo yao kokote wanakoenda, viongozi wa shule na walimu kushirikisha wazazi katika malezi ya watoto wao na watu wengine wanaokutana na mtoto kuelewa kwamba nao wanaweza kumwathiri mtoto huyo vizuri au vibaya. Waheshimiwa mabibi na mabwana hoja zote mlizozitoa zimezingatiwa na zimeeleweka vizuri. Asante sana kwa mchango wenu katika kupigania malezi bora kwa watoto wetu. Mjadala wa leo unaishia hapa. Njooni tena wakati mwingine kwa mada nyingine. Ahsanteni sana kwa kushiriki.

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Nani ambaye anawaruhusu washiriki kutoa hoja zao katika mjadala?
2. Malezi ya msingi mtoto huyapata wapi?
3. Dawa za kulevya zina madhara gani kwa maisha ya vijana?
4. Kwa nini mzazi ana wajibu wa kuwapeleka watoto shuleni?
5. Eleza nafasi ya Serikali katika malezi ya watoto kama ilivyozungumziwa katika mjadala huu.
6. Viongozi na walimu hutakiwa kufanya nini kwa kuzingatia nafasi ya wazazi katika malezi ya watoto wao?
7. «Mtoto hutazama kisogo cha mama yake.» Msemo huu unahusianaje na kifungu ulichosoma?
8. Mtu hutoa kile alicho nacho na pia mtu huvuna alichopanda." Eleza msemo huo kwa kuzingatia uliyoyasoma katika mjadala huu.
9. Zaidi ya wazazi, ni watu gani tena ambao huweza kuwaathiri watoto?
10. Ni masomo gani unayoyapata kutoka mjadala huu?

### 13.2. Msamiati kuhusu "Andalio la Mjadala"

## ZOEZI LA 2:

***Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo yanayotumika katika mjadala:***

1. mchango
2. elimu
3. dawa za kulevya
4. kisogo
5. kulea
6. kukaribisha
7. kiongozi
8. uzinzi
9. ulevi
10. serikali

## ZOEZI LA 3:

***Oanisha maneno yaliyoko katika orodha A na maelezo yaliyopo katika orodha B.***

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| 1. kutia motisha | a. jambo linalomlazimu mtu kulitimiza. |
| 2. jukumu | b. matendo ya mtu yanayojirudiarudia/tabia. |
| 3. mshiriki | c. kukataza jambo kufanyika. |
| 4. malezi | d. ada ya shule inayotolewa na mwanafunzi. |
| 5. ubongo | e. mpango fulani wa maendeleo k.v. ya nchi unaotarajiwa kutimizwa au uliokwisha anzwa. |
| 6. kuathiri | f. mtu anayeshiriki kufanya jambo fulani k.v. michezo maandamano au semina. |
| 7. mwenendo | g. bonge laini la nyamanyama lenye mishipa ya fahamu lililomo kichwani. |
| 8. kukiuka | h. kufanya isivyostahili. |
| 9. karo | i. kushawishi mtu kufanya jambo. |
| 10. kupinga marufuku | j. njia ya ukuzaji wa mtoto kwa kutarajiwa kufuata tabia na mwenendo unaostahiki. |
| 11. mradi | k. kumtia mtu mwingine hamu zaidi ya kufanya jambo. |

**ZOEZI LA 4:**

***Soma sentensi zifuatazo kisha ujadili hali zake:***

1. Kiongozi alisema katika mjadala: «Sikilizeni watakaotoa hoja zao.»
2. Tafadhali, mtoe michango yenu kuhusu mada.
3. Wanafunzi walikuwa wanapiga kelele, mwalimu akasema: «Nyamazeni mgeni anakuja.»
4. Usiwe na hofu! Mwelezee Mungu unayoyapitia kama matatizo, naye atakusaidia.

## 13.3. Sarufi: Matumizi ya Hali ya Vitenzi

Katika hali ya kuomba tunatumia maneno yafuatayo: tafadhali, samahani, kumradhi. Neno la kwanza ni neno la heshima la kumwomba mtu afanye jambo kwa hisani yake; neno la pili ni tamko linalotumika kuomba radhi au kumtafadhalisha mtu; wakati neno la tatu hufasiliwa kama tamko la kumwomba mtu haja au msamaha.

**MIFANO:**

- Tafadhali, nipe maji ya kunywa!
- Samahani, nionyeshe njia!
- Kumradhi, tamka neno ipasavyo.
- Tuelezee maana ya mjadala!
- Mletee kinywaji mzee yule!

Vitenzi katika hali ya kuomba, vinaweza kutumiwa katika umoja na vilevile katika wingi.

**MIFANO:**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Nisomee kifungu hiki kwa sauti. | 1. Nisomeeni vifungu hivi kwa sauti. |
| 2. Nisindikize hospitalini. | 2. Nisindikizeni hospitalini. |
| 3. Tuimbie wimbo wa furaha. | 3. Tuimbieni nyimbo za furaha. |
| 4. Washirikishe katika makundi. | 4. Washirikisheni katika makundi. |
| 5. Tafadhali, msaidie kuandika barua. | 5. Tafadhali, msaidieni kuandika barua. |

**Tanbihi:** Vitenzi hivi vinavyowekwa katika wingi, kiambishi -ni huongezwa kwenye vitenzi vya umoja.

**ZOEZI LA 5:**

***Ziweke sentensi hizi katika hali ya wingi:***

1. Sahau uliyoyaona yaliyokuhuzunisha.
2. Boresha maisha ya wanaoishi duniani.
3. Taarifu wenzako wasiohudhuria masomo ya leo.
4. Ruhusu mwanafunzi yule aende zake.
5. Samahani, tunga kifungu chenye maelezo kamili.

## ZOEZI LA 6:

***Tungo hizi zipo katika hali yakinishi, ziandike katika hali kanushi kushurutisha.***

1. Soma kitabu vizuri.
2. Kimbiza Simba asimshambulie mtoto.
3. Endelea na utafiti kuhusu maendeleo.
4. Penda anayekupenda tu.
5. Chanja watoto wachanga.
6. Wasili haraka kwenye majadiliano.
7. Jaribu kueleza mawazo yako waziwazi.
8. Jibu maswali yote unayoulizwa kwenye mjadala.
9. Samehe wanaosababisha kutopata ushindi wa kujinyakulia kombe.
10. Fikiri takribani mara mbili kabla ya kutoa hoja yako.

## 13.4. Matumizi ya lugha: Maandalizi na Utekelezaji wa Mjadala

## ZOEZI LA 7:

***Soma maelezo muhimu hapo chini kisha ujibu maswali yanayofuata:***

**Maelezo muhimu kuhusu "Andalio la mjadala"**

- **Mjadala** ni mazugumzo juu ya jambo fulani. Unaweza kufanyika katika makundi madogo madogo au makubwa.
- Mjadala unaongozwa na mtu mmoja au watu wawili ambao wanazusha mawazo na kuhakikisha ikiwa kuna mwenendo mwema kati ya washiriki wa mjadala huo.
- Kiongozi wa mjadala ndiye anayetoa muhtasari wa mawazo yaliyotolewa katika mjadala.
- Anayetoa hoja yake, anaweza kuunga mkono maoni ya mwenzake au kuyapinga kwa minajili ya kutoa mchango wake wa kutatua tatizo linalojadiliwa.

- Mjadala unapomalizika, kiongozi huwapongeza waliohudhuria mjadala na kuwaalika katika mjadala mwingine.

**Mambo ya kuzingatia katika utekelezaji wa mjadala:**

- Kutumia vizuri muda uliopangwa,
- Kuepuka fujo na kelele,
- Kupaza sauti unapotoa hoja kuhusu mada,
- Kutoa maoni kwa madhumuni ya kutimiza lengo la mjadala,
- Kutumia lugha isiyo ya matusi,
- Kuwaheshimu wengine,
- Kupanga mawazo yako kabla ya kupata fursa.

**MIFANO:**

1. Eleza maana ya mjadala.
2. Ni watu gani wanaoshiriki katika mjadala? Eleza.
3. Jadili mambo mawili ya kuzingatia katika uandalizi wa mjadala.

**ZOEZI LA 8:**

***Toa maana nyingine iliyo sawa na maneno haya kutoka mjadala:***

1. kudanganya
2. tia doa au dosari
3. wasaa
4. sharti
5. muadhamu
6. mvyele
7. dola
8. mazungumzo juu ya jambo maalumu
9. utaratibu wa kufanya jambo kwa hatua ili kufikia lengo linalokusudiwa
10. funzo
11. mtu aliye hodari wa kusema

**ZOEZI LA 9:**

***Chagua na uandike jina lifaalo baina ya yaliyomo katika mabano:***

1. Kiumbe kinachozaliwa hasa na mtu. (mtego, mtoto, moto).
2. Mtu anayesimamia na kuelekeza watu au kikundi cha watu wafanyao kazi au shughuli fulani (fundi, mkufunzi, kiongozi).
3. Mtu anayemtunza, kumhudumia na kumfundisha mtoto mpaka akue (mlezi, kiongozi, baharia).
4. Mtu aliye karibu na mahali unapoishi. (jinsia, jirani, jivu).
5. Mtu aliyezaliwa nawe kwa baba, kwa mama au kwa wazazi wote wawili (nduma, ndama, ndugu).
6. Kiongozi wa shughuli za shirika au taasisi fulani (mkufunzi, mkurufunzi, mkurugenzi).
7. Mahali ambapo wanafunzi hufundishwa elimu k.v. kusoma, kuandika, hesabu na masomo mengine (shuli, shule, shume).
8. Mtu anayefanya kazi za kuandika kumbukumbu na kuhifadhi maandishi ya shirika, kampuni au chama (katibu, katiba, katekista).
9. Mazoea yanayotokana na kurudiarudia hali, mwenendo au matendo. (tabibu, tabia, tabasamu).

## 13.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**ZOEZI LA 10:**

***Chagua mada moja kati ya hizi, kisha ujaribu kuijadili.***

1. Dawa za kienyeji zinasaidiaje katika uboreshaji wa afya nchini Rwanda?
2. Faida au hasara za kuishi katika miji mikubwa.
3. Mafanikio ya elimu ya wasichana kwa kulinganisha na nyakati zilizopita nchi mwetu.

## 13.6. Utungaji

**ZOEZI LA 11:**

***Ulisikia kuwa kila kukicha taifa letu linashuhudia ongezeko la idadi ya watoto wanaozurura na kuishi mitaani. Andika kifungu chenye aya sita ukitoa maoni yako kuhusu namna serikali na taifa zima linavyoweza kuwasaidia watoto hao.***

### TATHMINI YA MADA YA NNE

**A.**

1. Eleza uhusiano uliopo kati ya mdahalo na mjadala.
2. Jadili tofauti iliyopo kati ya mjadala na mdahalo.
3. Eleza mambo ya kuzingatia katika utekelezaji wa mjadala.
4. Eleza mambo ya kujiepusha katika mdahalo.

**B. Chagua mada moja kati ya hizi zifuatazo, kisha uandae mdahalo (kumbuka kutumia vitenzi katika hali shurutishi pale panapohitajika):**

1. Wakoloni walileta mabaya mengi kuliko mazuri.
2. Shule za bweni ni bora kuliko shule za kutwa.
3. Uzuri wa mtu si urembo bali ni tabia.
4. Kutoa si utajiri bali ni moyo.

**C. Kwa kuzingatia matumizi ya vitenzi katika hali shurutishi, andaa mjadala kuhusu moja ya mada zinazofuata:**

1. Manufaa ya michezo kwa mtu binafsi na kwa taifa.
2. Madhara ya kutumia dawa za kulevya na kushiriki ulevi.

# MADA KUU YA 5

## UTUNGAJI

# MADA KUU: UTUNGAJI

## MADA NDOGO: INSHA ZA MASIMULIZI AU ZA KUBUNI

**Uwezo Upatikanao katika Mada:**

Kumwezesha mwanafunzi kuzingatia mwongozo wa kutunga insha za masimulizi kulingana na mada iliyotolewa na kuzitolea muhtasari darasani kwa njia ya mazungumzo; kuelewa jinsi ya kumnukuu mtu mwingine.

## Malengo ya Ujifunzaji:

- Kueleza tofauti iliyopo kati ya insha ya kubuni na hadithi ya masimulizi;
- Kukumbuka sehemu kuu za kuzingatia katika utungaji wa insha za masimulizi;
- Kutafsiri mazingira ya mada na kuijadili bila upotovu wowote;
- Kutambua taratibu za kutoa ripoti ya taarifa kwa kuzingatia usemi wa asili na usemi wa taarifa;
- Kubainisha mabadiliko yaliyopo toka usemi wa asili kwenda usemi wa taarifa.

### Kazi Tangulizi

1. Kutokana na ujuzi wako, insha ni nini?
2. Unaelewa nini kuhusu insha za masimulizi?
3. Ni tofauti gani iliyopo kati ya insha za kubuni na hadithi za kubuni?
4. Orodhesha aina za insha unazozijua na ujaribu kutoa maelezo mafupi kuhusu kila aina.
5. Ni taratibu zipi zinazozingatiwa katika utungaji wa insha?

## SOMO LA 14: MAANA YA INSHA

### ZOEZI LA 1:

***Jibu maswali haya:***

1. Unaelewa nini kuhusu insha ?
2. Eleza aina za Insha unazozielewa.
3. Ni maadili yapi uliyoyapata kutokana na insha hiyo?

## 14.1. Kusoma na Ufahamu: Tarakilishi

Tarakilishi au kompyuta ni mashine au chombo muhimu cha kisayansi chenye uwezo wa kupokea na kukusanya taarifa, na kisha huzishughulikia taarifa hizo kulingana na kanuni za programu iliyopo kwenye tarakilishi. Hivyo tarakilishi hufuata hatua za kimantiki katika ufanyaji kazi wake. Uwezo wake unafanana na akili ya binadamu. Hapo, hutoa matokeo ya kazi na namna kazi hiyo ilivyoendeshwa, pamoja na kutoa matokeo ya kitu kilichofanyika. Chombo hiki ni kama rafiki katika jamii ya leo.

Tarakilishi huwawezesha binadamu kufanya mambo mengi muhimu kwa muda mfupi na kwa uhakika. Watu wengi huihitaji ili kurahisisha kazi zao mbalimbali. Mtu aitumiapo, hufanya kazi kwa wepesi wa hali ya juu, kiasi yeye hufanikisha kazi hiyo kwa muda wa sekunde chache tu. Mathalani watu wanapofanya hesabu ngumu na takwimu changamani, wao hupata matokeo au majibu kwa muda mfupi sana kuliko mtu yule asiyetumia tarakilishi. Hali hii ndiyo imewafanya watafiti wengi watimize kazi zao kwa kiwango cha juu ambapo tarakilishi imewasadia kutumia mitandao na intaneti inayowawezesha kupakua masomo mbalimbali na maandishi mengine muhimu yanayohitajika katika tafiti zao.

Tarakilishi hufanya kazi kwa ubora zaidi. Mtu anapoitumia hujiepusha na makosa yanayoweza kujitokeza katika hali ya kawaida. Hata kama itabainika ya kwamba kuna makosa ambayo yametendeka kwenye kazi fulani, usahihishaji wake huwa rahisi kama maandalizi yake yalifanyiwa kwa tarakilishi na kuhifadhiwa vizuri. Kompyuta ina uwezo mkubwa wa kusahihisha makosa yote yanayoweza kujitokeza katika kazi na mengi yanapofanywa, huwa inataarifu kwamba makosa hayo yapo na mtumiaji wake huyarekebisha kabla ya kuendelea na kazi yake.

Mara nyingine, ikiwa mtumiaji hana udhaifu wa kuitumia vizuri huwasiliana na kompyuta yake kwa kusoma na kutafakari kuhusu habari zinazotolewa na kompyuta yake kila inapomwelekeza katika kazi yake. Wakati mwingine, yeye hulazimika kuchagua, ama kuendelea na kazi yake baada ya kufanya marekebisho yanayohitajika.

Kompyuta humwezesha binadamu kufanikisha kazi nyingi sana katika nyanja mbalimbali za maisha yake. Shughuli za elimu, udaktari, uchapishaji wa vitabu, kilimo, ufugaji, urubani, biashara za aina mbalimbali, unahodha, utafiti wa aina mbalimbali, na nyingine nyingi huhitaji matumizi ya tarakilishi. Chunguza kwa mfano daktari akiwa katika operesheni ya upasuaji wa viungo fulani vya mwili wa mtu, kompyuta hufanya kazi kubwa ya kumwelekeza kwenye sehemu zilizoathiriwa na ugonjwa na kazi huwa rahisi. Vilevile, utabibu wa magonjwa kwenye hospitali kama vile kupima mishipa ya damu

na kupimia kiwango cha chumvi au sukari kwenye damu zote hutumia kompyuta ili kupata matokeo.

Shughuli nyingi zilizoweza kuwashangaza watu na ambazo zilitokana na uvumbuzi wa binadamu, msingi wake ni kompyuta. Kuendesha ndege angani ni mojawapo na shughuli hizo muhimu ambapo matumizi ya kompyuta huchukua nafasi kubwa. Rubani anapofanya kazi yake huitumia kompyuta kuwasiliana na wasafiri na wafanyakazi wengine wanaomwelekeza kuhusu sehemu za kupitia, hali ya hewa na mambo mengine muhimu yanayohitajika. Zaidi ya hayo, yeye huhitaji kompyuta kumjulisha usalama wa ndege na hitilafu zote zinazoweza kujitokeza katika safari yake. Tarakilishi hiyo ndiyo husaidia pia kwa kuhifadhi taarifa zote zinazohusiana na safari ya ndege kupitia kisanduku cheusi kiasi kwamba jambo fulani kama vile ajali au maafa yakitokea, wachunguzi na watafiti huitumia kujua sababu za ajali iliyotokea. Matokeo ya uchunguzi huo ndio huwaelekeza kuchukua uamuzi unaofaa kulinda usalama wa ndege nyingine na hata kuchochea urekebishaji na uendelezaji wa teknolojia na ufundi wa vyombo vya usafiri.

Hivyo basi, tarakilishi ni miongoni mwa nyenzo zilizotokana na mabadiliko ya teknolojia ya hali ya juu na huweza kuchukuliwa kama chombo muhimu kilichowahi kuvumbuliwa na mwanadamu. Tarakilishi ni msingi imara wa kuonyesha kiwango cha maendeleo ya kisayansi na nguzo muhimu katika mawasiliano na maendeleo ya kijamii ulimwenguni kote. Ni vyema watu wote wajue kuitumia kwani mambo mengi inayoyafanya huelekezwa na kuongozwa na binadamu.

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Ni nini maana ya tarakilishi?
2. Chombo hiki kina uwezo gani?
3. Kwa nini chombo hiki huchukuliwa kama rafiki katika jamii ya leo?
4. Toa mifano miwili inayoonyesha jinsi tarakilishi hutumia muda mfupi kwa kufanya kazi.
5. Tarakilishi ina mchango gani katika kuboresha afya ya watu?
6. Jinsi gani tarakilishi hutumiwa katika mawasiliano?
7. Kisanduku cheusi kinachopatikana katika ndege huwa na umuhimu gani?
8. Toa mifano saba ya kazi ambazo hufanywa na tarakilishi.
9. Kwa maoni yako tarakilishi ina umuhimu gani kwa mwanafunzi?

## 14.2. Msamiati kuhusu Kifungu cha Habari

**ZOEZI LA 2:**

***Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo kulingana na matumizi yake katika kifungu hapo juu:***

1. Tarakilishi
2. Mantiki
3. Intaneti
4. Utabibu
5. Utafiti
6. Nguzo
7. Kuchochea
8. Uchapishaji

**ZOEZI LA 3:**

***Jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yafuatayo: huchochea, mantiki, mishipa, Utabibu, hitilafu, unahodha, tarakilishi, kuhifadhi, urubani, nguzo.***

1. Shule yetu imepewa zawadi ya ……………………………zitakazotumiwa na wanafunzi.
2. Kazi za umuganda ni ……………..……….muhimu katika uboreshaji wa uchumi.
3. Kompyuta hutumiwa katika kufanya………………….. wa magonjwa mbalimbali kwa wagonjwa.
4. Alitumia…………….. …. Kueleza suluhisho la mgogoro uliojitokeza.
5. ................na ..........................ni shughuli zinazohitaji sana matumizi ya tarakilishi kwa madhumuni ya kuendesha ndege na meli.
6. Lugha ni chombo kinachowasaidia binadamu ...................................taarifa zote zinazohusiana na utekelezaji wa jambo fulani.
7. Teknolojia mpya ......................... kuandaa miradi mbalimbali ya kujiendeleza.
8. Tarakilishi husaidia wahandisi kuangalia mwenendo wa hali ya hewa na hivyo kuweza kupanga namna ya kuepuka ………………… zinazoweza kutukia wakati wa safari za ndege.
9. Ugonjwa wa…………inayosafirisha damu miguuni huweza kusababisha kukatwa mguu.
10. …………………wa kuku kibiashara ni nyenzo muhimu zinazomwezesha mtu kupambana na umaskini.

## ZOEZI LA 4:

***Oanisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B.***

| Sehemu ya A | Sehemu ya B |
|---|---|
| 1. Tarakilishi | a. Ustadi wa kazi ya kutibu, hasa hospitalini. |
| 2. Uchapishaji | b. Kifaa cha kielektroniki cha kuhifadhi na kuchanganua taarifa zilizoingizwa pamoja na kuongoza mitambo mbalimbali. |
| 3. Kuchochea | c. Mtandao wa mawasiliano ya kimataifa wa kikompyuta. |
| 4. Nguzo | d. Mtiririko wa fikra zilizopangwa ili kujenga hoja yenye kukubalika. |
| 5. Utafiti | e. Uchunguzi wa kitaaluma wenye lengo la kugundua au kutafuta habari. |
| 6. Intaneti | f. Kutia hamu, kuamsha, kuchangamsha. |
| 7. Utabibu | g. kazi au shughuli za kutoa vitabu au magazeti. |
| 8. Mantiki | h. Jambo la msingi. |

### 14.3. Sarufi: Usemi Halisi na Usemi wa Taarifa

## ZOEZI LA 5:

***Soma maelezo kuhusu usemi halisi kisha ujibu maswali hapo chini.***

Usemi halisi huitwa pia usemi wa asili. Haya ni maneno yanayosemwa na mtu yakiwa katika hali yake ya kwanza bila kugeuza kitu kimuundo na kimatamshi. Katika usemi halisi mzungumzaji hutoa hotuba juu ya jambo fulani yeye mwenyewe. Hivi ni kusema kwamba maneno yanayotamkwa ni ya mtu yule mwenyewe bila kuripotiwa, yaani ni usemi wa moja kwa moja.

**MIFANO:**

a. Kitindamimba akamuuliza babake Yakobo “Babangu, Kwa nini ungali shuleni wakati wenzako wao wameisha maliza masomo?”

b. Akaendelea “Wengi mwa walimu wetu hapo shuleni mlijifunza pamoja.”

c. “Una fanya kazi gani?” Wazazi wangu waliniuliza.

d. Kalisa anasema “Nina kazi nyingi ofisini.”

e. “Ninampenda mke wangu” Yohana anasema.

**Matumizi ya alama za mtajo**

Katika usemi halisi alama za mtajo (“”) hutumiwa kumaanisha kwamba maneno yanayonukuliwa ni yale ya yule aliyeyasema bila kuongeza au kubadili kitu. Pia katika usemi halisi alama ya kuuliza (?) na alama ya kushangaa (!) nazo ni lazima zitumiwe.

**MIFANO:**

a. “Una nini mikononi mwako?” Baba anamuuliza mtoto wake.

b. “Aah! Hujui kwamba nitakuja kesho kuongea nawe!” Bwana yake alisema.

c. “Unanihitaji leo jioni?” Keti anamuuliza rafiki yake.

d. “Unanihitaji?” Anamuuliza Keti.

**Weka alama zinazohitajika kwa kukamilsha sentensi hizi:**

1. Ninakwenda nyumbani Alisema mwanafunzi
2. Huyu ni ng’ombe mnene kabisa Muhire alisema kwa mshangao
3. Utatoka hapa saa ngapi Baba aliniuliza
4. Ninampenda sana Mungu Maombi anaeleza
5. Rafiki yangu ana ulemavu wa mguu Kampire alituambia

**ZOEZI LA 6:**

***Kufuatia mifano iliyotolewa hapo juu, tunga sentensi tano katika usemi halisi.***

## 14.4. Matumizi ya Lugha: Maana ya Insha na Sifa Zake

**ZOEZI LA 7:**

***Soma maelezo haya yafuatayo ili ujibu maswali yaliyotolewa hapo chini:***

**Insha** ni mtungo wa kinathari unaozungumzia suala au kusimulia kisa fulani. Utungo huu huwa na urefu wa wastani. Kisa hicho au suala hilo ndilo mada ya utungo huo. Insha hutumiwa kuelezea maoni ya mwandishi kuhusu masuala au mambo tofauti.

**Sifa za Insha**

- Insha nzuri inapaswa kuwa sahihi kisarufi. Usafi huu huhusisha muundo wa sentensi na mpangilio wa aya ufaao.
- Lazima suala linalozungumziwa au yaliyomo katika insha yahusishwe na kichwa cha insha.
- Insha inapaswa kuepuka utata. Yaani kuwepo kwa maana nyingi. Pasiwepo na kauli au sentensi ambazo hazionyeshi uhusiano wazi na sentensi nyingine.
- Lazima insha iwe na utangulizi mzuri unaojitokeza wazi pamoja na mwisho ambao unadhihirika waziwazi.
- Insha inapaswa kuwa na urefu wa kutosha. Isiwe ndefu sana na fupi kupita kiasi. Aghalabu urefu wa insha unafungamana na mada yenyewe au kinachozungumziwa katika insha hiyo.
- Insha haipaswi kuwa mkusanyo wa nukuu au maneno ya wandishi wengine isipokuwa pale ambapo mwandishi ameweka wazi kuwa anatumia maneno ya wengine.
- Mwisho, insha ni sharti iwe na mvuto. Yaani uwezo wa kumvutia msomaji.

**Muundo wa Insha**

**Insha yoyote huwa na muundo. Muundo huo huwa na:**

a. **Kichwa:** Hii ndiyo mada ya insha au kinachozungumziwa. Kichwa hakipaswi kuwa na maneno mengi.

b. **Utangulizi:** Sehemu hii hutanguliza insha. Sehemu hii huwa na aya moja ambayo haina mistari mingi (labda minane). Hupaswa kuwa na mvuto kwa msomaji na kutoa mwelekezo wa insha yenyewe.

c. **Mwili au sehemu kuu:** Hii huwa ndiyo hasa insha yenyewe. Mwili wa insha huundwa na aya zinazoendeleza mada ya insha. Kila aya lazima ichangie katika kuliendeleza wazo kuu. Ni vyema kuhakikisha kuwa pana muunganiko ulio wazi kutoka aya moja hadi nyingine.

d. **Hitimisho:** Ni sehemu ya mwisho wa insha. Katika sehemu hii mwandishi hurudia kwa ufupi yale aliyoyaelezea katika insha yenyewe.

**Jibu maswali yafuatayo kuhusu maelezo muhimu uliyoyasoma hapo juu:**

1. Ni nini maana ya insha?
2. Insha nzuri inapaswa kuzingatia mambo gani?
3. Taja sehemu nne muhimu za insha.
4. Ni katika sehemu gani ya insha ambapo mwandishi hulifafanua kwa mapana swali linaloshughulikiwa?

**ZOEZI LA 8:**

***Dokeza mambo muhimu yanayoweza kuzingatiwa kwenye kichwa, mwili na hitimisho la insha zenye mada zifuatazo:***

1. Utawala Bora
2. Umoja wa Jamii
3. Afya ya Watoto

## 14.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

**ZOEZI LA 9:**

***Jadili kuhusu mada zifuatazo:***

1. Nafasi ya Teknolojia Mpya katika Maendeleo ya Kilimo na Ufugaji.
2. Umuhimu wa Kompyuta katika Biashara Mbalimbali.
3. Umuhimu wa Kompyuta katika Michezo na Burudani.

## 14.6. Utungaji: Uandishi wa Insha

**ZOEZI LA 10:**

***Kutokana na mfano wa insha uliotolewa hapo juu, andika insha kuhusu mada***

"Umoja wa Afrika ni Msingi Muhimu kwa Maendeleo ya Afrika"

# SOMO LA 15: AINA ZA INSHA

## ZOEZI LA 1:

***Jibu maswali haya:***

1. Unaelewa nini kuhusu insha?
2. Eleza aina za insha unazozielewa.
3. Ni maadili yapi uliyoyapata kutokana na insha hiyo?

## 15.1. Kusoma na Ufahamu: Nchi Yetu

Soma kifungu kifuatacho kwa makini, kisha jibu maswali yaliyopo hapo chini yake.

Tazama unavyopendeza! Tazama ulivyopambwa na Mungu. Ewe fahari yetu, Rwanda nchi ya amani. Wewe ni nchi ya neema. Usafi umejipamba, ewee Rwanda kujulikana ulimwenguni kote. Jina lako umejijengea, we nchi ya usalama iliyo mfano wa kuigwa na majirani na hata wengi kutoka Ughaibuni.

Nani asiyeona uzuri wako, ewee nchi mashuhuri? Maelfu ya milima yako mirefu, ya kuvutia kwa kila mtu, awe mgeni au mwenyeji! Wengi wakupenda kwa hali isiyokadirika. Milima yenye mabonde huwavutia wote, kwa miti mirefu na midogo, nyasi na mimea ya aina nyingi huchangia kuonyesha mvuto wako. Maua mazuri umejipamba ewee nchi yetu, mandhari yako yapendeza kwa mbuga za wanyama zinazowaleta watu wengi kutalii.

Ni nani ambaye hatakusifu kwa sababu ya usafi wa miji na vijiji vyako? Miji yako ni safi, inamulika kila sehemu, kokote unakoenda wewe utajivunia. Ukifika jiji kuu Kigali, moyo wako unatekwa na hali ya usafi inayokaribisha, ewee nchi yangu umejipamba ukapambika.

Barabara zote lami imewekwa, pembezoni alama nyeusi na nyeupe huonekana, wafikiria kama pundamilia anayetulia kwa shibe. Miti tofauti imepandwa kiasi kuneemesha jiji hili kwa harufu nzuri ya maua yake ungedhani manukato ya mwali aliye tayari kuolewa. Jiji hili laonekana kijani kibichi kutokana na miti hiyo, usiku kutwa watembea bila wasiwasi kwa kuvuta hewa nyororo. Usiku taa huwashwa jijini pote, ewee nchi yangu wametameta kama nyota mbinguni!

Ukiingia mikoani, huwezi kutofautisha vijiji na miji kwa sababu pote ni safi. Popote uendapo usafi ndio desturi yao, usichafue mazingira, hata pasipotarajiwa, pengine kutema mate barabarani, hilo ni mwiko kwa kila anayepita! Mabango mengi husema, chunguza vizuri na ufikiri usijiingize hatarini kwa kuyachafua mazingira yaliyopambwa kwa jasho la wananchi. Ukifanya matendo yaliyo kinyume, utatozwa faini. Hivyo hupaswi kuchafua

mazingira, jitahadhari unakoenda usiwe na kiburi, fuata sheria na kanuni.

Kila mwishoni mwa mwezi, shughuli za “Umuganda” hufanywa kwa ajili ya kustawisha maendeleo yetu. Aidha, mazingira pia husafishwa. Ewee mama yetu mpedwa Rwanda, tunajivunia wewe. Katika usafi wa mazingira, huwa tunafyeka vichaka, tunafagia, tunapanda miti, tunasafisha mitaro,tunaziba vidimbwi vya maji, taka zote huzolewa na kutupwa jalalani ili tujilinde dhidi ya maradhi ya kuambukiza, hasa yale yanayochochewa na uchafu. Kwa hakika tumejikinga na magonjwa haya yote. Zaidi ya hivyo, hata malaria yapigwa vita, wananchi wote waneemeka na kuishi kwa utulivu nchini Rwanda.

Ewee fahari yetu Rwanda, nitakusifu daima! Nitakutangaza ujulikane! Usafi wako ni desturi, wananchi wako wamelijua. Kulia barabarani si tabia yao, utamaduni unatukataza, kila mmoja hujiheshimu. Raia wote wanapotembea, viatu na nguo safi huvaa. Nyumba zote huwa safi na vyoo safi kutengenezwa, hilo ni kawaida kwa wananchi wote. Washauri wa kiafya hufanya kazi ya kuwaelimisha walio na udhaifu wa kuelewa kanuni na sheria zinazoongoza sekta ya afya. Kwa hakika, afya yetu ni jambo la thamani.

Nisikilizeni ndugu na marafiki! Ninawaambia kwamba nchi yetu ni zawadi kubwa tuliyopewa na Mwenyezi Mungu. Hebu tuilinde kwa kutunza usafi. Twendelee kuwahimiza wote hadi kuibadilisha dunia nzima, sisi mfano mzuri tuzidi kuirembesha nchi yetu, tutanufaika kwa kuimarisha usafi wa nchi yetu.

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Kwa sababu gani mwandishi anaisifu nchi ya Rwanda?
2. Kwa nini nchi ya Rwanda husemekana kuwa mfano mzuri?
3. Eleza umuhimu wa miti.
4. Ni kitu gani kinacholineemesha jiji la Kigali?
5. Taja vitendo vitano vinavyofanywa wakati wa Umuganda.
6. Wageni hushauriwa nini kila wanapofika nchini Rwanda?
7. Taja vitendo viwili ambavyo haviruhusiwi kulingana na desturi ya wananchi wa Rwanda.
8. Ni kwa sababu gani si vizuri kutembea bila viatu?
9. Toa mfano wa ugonjwa unaosababishwa na ukosefu wa usafi.
10. Ni somo gani ambalo umepata kutoka kifungu hiki?

## 15.2. Msamiati kuhusu Nchi Yetu

**ZOEZI LA 2:**

***Toa maana za maneno yafuatayo:***

1. Fahari
2. Ughaibu
3. Kuvutia
4. Mwanana
5. Pembezoni

**ZOEZI LA 3:**

***Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:***

1. Lami
2. Pundamilia
3. Mabango
4. Kufyeka
5. Magubiko

**ZOEZI LA 4:**

***Oanisha maelezo ya sehemu ya A na maneno ya sehemu ya B***

**MIFANO:**

8→ g

| A | B |
|---|---|
| 1. Fedha ya kulipa adhabu ya kosa ulilofanya | a. Neema |
| 2. Kupata faida | b. Kutema |
| 3. Hali ya mafanikio au ustawi | c. Kusifu |
| 4. Kufanya iwe katika hali mbaya au isifae | d. Kutwaa |
| 5. Jambo la kawaida linalotendwa kila siku | e. Kumetameta |
| 6. Kueleza hali ya uzuri wa jambo, kitu au mtu | f. Faini |
| 7. Kutoa mwangaza unaozima na kuwaka kwa mfululizo | g. Kustawisha |
| 8. Kuimarisha | h. Desturi |
| 9. Kutoa kitu kutoka mdomoni kwa makusudi na kukisukuma nje kwa kutumia ulimi | i. Kunufaika |
| 10. Kuchukua | j. Kuharibu |

## 15.3. Sarufi: Usemi wa Taarifa

**ZOEZI LA 5:**

***Chunguza muundo wa sentensi A na B zifuatazo, kisha utunge sentensi mbili zinazofanana nazo.***

A. "Nchi hii ya Rwanda ina usafi usio na kifani." Baadhi ya wanariadha walidai walipofika mjini Kigali.

B. Baadhi ya wanariadha walipofika mjini Kigali walidai kwamba nchi ya Rwanda ina usafi usio na kifani.

- Sentensi hizo zimebainisha mabadiliko kadhaa ya kisarufi ambapo sentensi A ni ya usemi halisi ilihali sentensi B ni ya Usemi wa taarifa.
- Katika usemi halisi au usemi wa asili, maneno yaliyosemwa na mtu hurudiwa na mwingine jinsi alivyoyasema bila kuongeza au kutoa kitu. Ni namna ya kunukuu maneno ya mwingine. Alama za vituo zinazotumiwa katika usemi huo ni hizi zifuatazo:
- Alama za mtajo na ndizo zinazofungua na kufunga maneno ya msemaji ("");
- Alama ya kuuliza (?);
- Alama ya mshangao au alama ya hisi (!).

**MIFANO:**

- "Wanangu, dunia ya leo inawapasa mfanye bidii kazini!" Mzee aliwaambia watoto wake.
- "Ndugu yangu, mbona unataka ushirikiano na watu wakatili?" Mariam alimwambia dada yake.
- Katika usemi wa taarifa, maneno ya mtu huyo hurudiwa lakini sisi tunabeba uhusika wake. Ni kusema kuwa tunaripoti taarifa iliyotolewa na msemaji halisi.

**MIFANO:**

- Mzee aliwaambia watoto wake kuwa dunia ya siku hizo iliwapasa wafanye bidii kazini.
- Mariam alimwambia dada yake kwamba alikuwa hataki ashirikiane na watu wakatili.
- Usemi wa taarifa unatii kanuni zifuatazo:

**Alama za vituo:**

- Alama za mtajo hazitumiki.
- Alama za kuuliza na mshangao hazitumiki.
- Nukta inatumiwa mara nyingi.

**Maneno mengine:** **"Kuwa"** au **"kwamba"** hutumiwa.

## ZOEZI LA 6:

***Yafuatayo ni mazungumzo halisi kati ya Mwalimu mkuu na mzazi. Geuza sentensi ziwe katika usemi taarifa.***

1. "Wewe ni mzazi wa nani?" Mwalimu mkuu alimwuliza mzazi.
2. "Mimi ni babake Yohana." Mzazi akajibu.
3. "Yohana ni mwanafunzi wangu mzuri sana, ambaye anazingatia mambo ya usafi shuleni." Mwalimu mkuu aliendelea kusema.
4. "Ndiyo! Na hata nyumbani anakuwa hivyo." Mzazi alihakikisha."Sasa ningependa unipatie nafasi ya mdogo wake Yohana katika kidato cha nne."
5. "Mtoto wako alikuwa akisomea wapi?" Mwalimu mkuu akamwuliza mzazi.
6. "Alikuwa akisoma kwenye Shule ya Sekondari ya Rukomo." Mzazi alijibu.
7. "Kwa nini unamhamisha kutoka huko?" Mwalimu mkuu aliuliza tena.
8. "Ningependa asomee karibu na nyumbani kwetu." Mzazi alijibu.

**ZOEZI LA 7:**

***Ziandike sentensi zifuatazo katika usemi wa taarifa.***

1. “Jitayarisheni kutunga insha ya wasifu.” Mwalimu aliwaambia wanafunzi.
2. “Ninataka darasa hili lisafishwe kila asubuhi.” Mwalimu alisema kwa sauti kubwa.
3. “Tujivunie utamaduni wetu.” Waziri wa utamaduni aliwaambia wanafunzi wa chuo kikuu.
4. Mkuu wa kijiji aliwaambia raia wenzake: “Toeni maoni yenu kuhusu jambo linalozungumziwa sasa.”
5. “Nduli huyu – kipindupindu – tutamshinda tu na kumtokomeza iwapo tutatumia kinga zote za kujiepusha na uchafu wa mazingira yetu.” Katibu Mtendaji wa Tarafa yetu alitwambia baada ya *Umuganda*.
6. “Hairuhusiwi kuwinda na kuwauwa wanyamapori.” Askari mmoja alisema.
7. “Sijaona nchi safi kama Rwanda!” Mtalii kutoka Uingereza alishangaa.
8. “Zingatieni taratibu za usafi kama zilivyopangwa na serikali yetu!”Afisa wa Uhamiaji aliwaambia watalii.
9. Mwalimu mkuu aliwaambia wanafunzi hodari: “Hali ya hewa itakapokuwa nzuri tutatembelea Mbuga ya wanyama ya Akagera.”
10. “Toeni mchango wenu ili tujenge nchi yetu!” Meya wa wilaya aliwahamasisha raia wake.

## 15.4. Matumizi ya Lugha: Aina za Insha

**ZOEZI LA 8:**

***Soma maelezo kuhusu aina za insha zifuatazo, kisha ujibu maswali yaliyotolewa chini yake.***

Kumbuka kuwa insha ni mtungo wa kinathari ambao unajigawa katika aina mbalimbali. Zifuatazo ni baadhi ya aina nyingi zinazopatikana:.

### 1. Insha za Wasifu

Insha za wasifu ni aina ya utungaji ambao huchora picha ya kitu kinachozungumziwa. Huonyesha waziwazi hisia za msanii. Aghalabu, kuna vitu vingi ambavyo tunaviona kila siku kama vya kawaida lakini mtungaji anaweza akavitungia insha za wasifu na tukaviona katika mtazamo tofauti kabisa. Katika insha za wasifu kuna usanii.

**2. Insha ya Mjadala/Mdahalo**

Inalenga mara nyingi kulieleza jambo na vilevile kuhimiza mtazamo fulani. Hata hivyo, jambo lililo muhimu zaidi si kueleza bali ni kujibidiisha kushawishi. Katika mdahalo shawishi, mwandishi hulenga katika kuathiri hisia na maoni ya msomaji kwa njia ya kumfanya achukue hatua.

**3. Insha Fafanuzi**

Katika aina hii ya insha, mwandishi hutumia mifano kufafanua au kutilia mkazo hoja yake. Anaweza kutumia mfano mmoja wenye uzito au mifano mingi yenye kuhusiana.

**MFANO:**

Bei ya viazi mviringo imepanda sana nchini Rwanda

**4. Insha ya Methali**

Insha ya methali ni utungo unaoandikwa kwa kuzingatia methali. Kisa au maelezo yatolewayo yanaongozwa na maana iliyomo katika methali husika. Kabla ya kuanza kuandika insha, ni bora kwanza kuielewa vema maana ya methali. Mbali na kufahamu maana ya kijuujuu ya methali, inambidi mtunzi wa insha kuelewa mazingira (miktadha mingine ambapo methali husika inaweza kutumiwa). Kwa mfano: Akili ni nywele kila mtu ana zake.

**5. Insha ya Mdokezo**

Insha ya mdokezo ni aina ya utungo ambao huandikwa kwa kuongozwa na maneno aliyopewa mtunzi wake. Maneno hayo yaliyotolewa ndiyo mwongozo wa kumwelekeza mwandishi kuhusu maudhui atakayoandika. Lililo muhimu ni kuhakikisha kuwa mtungo utakaoandikwa unaoana vizuri na maneno yaliyotolewa kama mwongozo.

**MFANO:**

Siku hizi Maisha ya Mjini Yamekuwa Magumu..........................

**6. Insha za Picha**

Insha za picha ni zile ambazo msingi wake wa kuzitunga ni picha ambazo huwa zimechorwa na ambazo humwongoza mwandishi kubuni hadithi au kisa kinachooana na picha hizo. Kimsingi, huhitaji ufasiri wa picha zilizo kwenye ukurasa na kuibuni hadithi kuzihusu. Hivyo basi huwa ni insha za kusimulia.

**7. Insha ya Mawazo au ya Kubuni**

Insha hizi zinahusu jambo la kufikiriwa. Jambo linalojadiliwa katika aina ya insha hii huwa halitokani na hali au tukio halisi katika maisha. Vipengele vyote vinavyoijenga hubuniwa na mtunzi wake. Maudhui, wahusika, mandhari vya

mtungo wa aina hii vyote hubuniwa katika fikra ya mtunzi.

**8. Insha ya Kitawasifu (Insha Elezi/ya Maelezo)**

Insha hii huwasilisha sifa za vitu, watu, hali, matendo, mahali au hata sherehe uliyohudhuria. Inalenga kutoa picha ya kitu katika akili zetu jinsi ambavyo kinamdhihirikia anayekiona. Ili kuandika insha ya maelezo, mwandishi wake anahitaji kwanza kabisa kukusanya habari za kina kuhusu jambo analoliandikia. Hategemei tu yale ambayo yanaonekana kwa macho bali pia aina nyingine za hisi kama vile kugusa, kuonja, kunusa, kusikia na kadhalika. Hali hii humwezesha msomaji kupata taswira kamilifu kuhusu jambo linaloelezewa kupitia viungo vya kuona, kuonja, kugusa na kusikia.

**9. Insha ya Masimulizi**

Insha ya masimulizi ni insha yenye kuhadhiria tukio au hali fulani. Ni utungo ambao husimulia au kuelezea kisa. Dhima yake ni kuburudisha au kuteka umakini wa msomaji. Kwa kuwa inalenga hadhira ni muhimu kufahamu na kuitambua hadhira yako kabla ya kuandika utungo wako.

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Insha ni nini?
2. Taja aina za insha.
3. Kifungu cha habari "*Nchi Yetu*" ni insha ya aina gani? Kwa sababu gani?
4. Kuna tofauti gani kati ya insha za wasifu na insha za maelezo?
5. Eleza umuhimu wa kujifunza utungaji wa insha.

## ZOEZI LA 9:

***Tafuta maneno kumi yanayohusiana na mazingira na usafi kwenye mraba ufuatao:***

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | C | H | A | F | U | Z | I | U | H |
| P | S | K | K | M | N | I | O | O | E |
| E | Y | A | B | A | Z | W | K | F | W |
| P | E | M | F | Z | M | A | W | B | A |
| O | D | I | Y | I | A | L | E | F | R |
| I | C | L | E | N | U | M | I | T | I |
| K | P | I | K | I | A | K | P | V | R |
| W | V | M | E | R | U | O | U | Y | L |
| I | H | A | O | A | W | I | G | A | H |
| N | Y | A | S | I | N | M | V | U | A |

## ZOEZI LA 10:

***Nyanja zifuatazo zimo chini ya wizara gani nchini Rwanda?***

1. Mbuga za wanyama
2. Barabara
3. Zahanati
4. Mbuzi
5. Jeshi

## ZOEZI LA 11:

***Chagua neno lisilo na uhusiano wowote na mengine:***

**MFANO:**

jamhuri, wanyama, taifa, nchi

**Jibu**: wanyama,

1. Mifugo, wanyamapori, mbwa mwitu, mimea
2. Mwindaji, kiongozi, katibu mtendaji, mkuu wa wilaya
3. Kondoo, paa, nyumba, nyumbu
4. Kusifu, kuchezea, kuimbia, kutukana.
5. Msanii, nahodha, mwimbaji, mchoraji.

## ZOEZI LA 12:

***Panga sentensi ili upate habari.***

1. Baada ya hapo, humeza maji mengi pamoja na samaki.
2. Akishafunga mdomo, husukuma nje maji aliyoyameza kupitia chujio lililoko mdomoni.
3. Akishameza maji na samaki,hufunga mdomo wake.
4. Ndipo samaki hubaki ndani.
5. Nyangumi anapohisi njaa, hutafuta sehemu yenye kundi la samaki.
6. Kisha, hupanua mdomo wake mkubwa.

## 15.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

**ZOEZI LA 13:**

***Jadili kuhusu mada zifuatazo:***

1. Umuhimu wa Usafi.
2. Namna ya Kuhifadhi Mazingira Yetu.

## 15.6. Utungaji: Uandishi wa Insha ya Wasifu

**ZOEZI LA 14:**

***Andika insha ya wasifu kuhusu mojawapo ya mada zifuatazo:***

a. Rafiki Yangu

b. Shule Yetu

c. Ziwa la Kivu

d. Wazazi Wangu

# SOMO LA 16: INSHA ZA MASIMULIZI

## ZOEZI LA 1:

***Chunguza michoro hii ifuatayo kisha ujibu maswali yaliyotolewa hapo chini.***







## MASWALI YA UFAHAMU

1. Ni kitu gani kinachoendelea kwenye mchoro wa kwanza?
2. Michoro hii miwili ina uhusiano gani?

### 16.1. Kusoma na Ufahamu: Siku Yangu ya Kwanza katika Shule ya Sekondari Kidato cha Nne

*Soma mfano huu wa insha ya masimulizi kuhusu* “Siku Yangu ya Kwanza katika Shule ya Sekondari’ *kisha jibu maswali yaliyotolewa hapo chini*

Mwanzo wa masomo yetu ulipokaribia kufika, wazazi wote walianza kujiandaa kwa kutimiza wajibu wao wa kuwanunulia watoto wao mahitaji kwa ajili ya masomo yao katika shule za Sekondari. Wazazi wangu nao waliwajibika kuninunulia mahitaji yote muhimu yaliyohitajika.Hivyo muda wa kuanza masomo ulipowadia, kila kitu kilikuwa tayari, hivyo nikaenda shuleni bila kuwa na wasiwasi wowote.

Ulikuwa wakati wa mwanzo wa mwaka, shule za msingi na za sekondari zilifungua tayari kwa kuanza masomo. Mimi niliamka asubuhi na mapema nikatoka nyumbani saa kumi na mbili kamili. Baba, mama, dada na kaka wawili walinisindikiza umbali wa takribani kilomita mbili toka nyumbani kabla ya wengine kurudi nyumbani isipokuwa baba. Baba yangu alichukua begi langu lililokuwa zito nami nikachukua ndoo na godoro langu tukaendelea mpaka kituo cha basi.

Tulipofika njiani baba yangu aliniambia kwa sauti ya upole akisema: “mtoto wangu, nenda ukasome kwa bidii na usipoteze muda wako. Kumbuka kuwa tumeuza mbuzi wetu wawili ili tuweze kukutafutia vifaa vyote unavyovihitaji.

Huko shuleni utakutana na vijana wengi wenye tabia tofauti. Tafadhali, usijiingize katika makundi ya wanafunzi wabaya ambao hawazingatii maonyo na mawaidha ya wazazi wao na walimu." Nami nilifikiria kidogo ili niweze kumpa baba yangu jibu kutokana na yale aliyoniambia. Hatimaye, nilipata cha kumuambia baba. "Baba! Sitakusaliti kamwe! Malezi uliyonipa tangu utotoni mwangu nitayazingatia na nitajifunza kwa bidii kama kawaida. Sitajiingiza katika makundi ya vijana hao wasio na maadlili mema." Baada ya kusikia hayo, baba yangu alitikisa kichwa kuonyesha kukubaliana nami kuhusu mwelekeo wangu wa maisha katika mazingira niliyotarajia kuingia. Tuliendelea na safari mpaka tulipofika kwenye kituo cha basi. Huo ulikuwa mwendo wa saa moja tu kwa miguu.

Kwenye kituo cha basi, kulikuwa na wanafunzi wengi lakini magari nayo yalikuwa mengi. Baada ya dakika thelathini, basi lilikuja tukaingia sote. Mimi nilikaa upande wa dirisha na baba alikaa karibu nami. Nilifurahia kuenda nikitazama miti na mimea ya aina mbalimbali iliyokuwa imepandwa kando kando ya barabara kubwa. Barabara hii ilikuwa na lami na taa kubwa ambazo zilitoa mwangaza wa kutosha wakati wa usiku. Tuliendelea na safari yetu mpaka shuleni. Kufika hapo, tulielekea kwenye ofisi ya mwalimu mkuu ili tujitambulishe na kujisajili. Hapo nje palikuwa na umati wa wanafunzi waliokuwa wakielekezwa kwenye mabweni yao na wengine wakifanya shughuli za usafi. Labda hao walikuwa wenyeji wa shule hiyo kwani walikuwa wakizungumza na kucheka kwa furaha kubwa pasipo wasiwasi wowote.

Tulipiga hodi ofisini tukapokelewa kwa mikono miwili. Mkurugenzi alituuliza habari kamili, tukamwelezea yote halafu nilielekezwa kwa katibu ambaye alinisajili baada ya kuonyesha stakabadhi ya malipo ya karo ya shule. Mfanyakazi huyu alimwita afisa wa nidhamu ili anipeleke bwenini na kunionyesha kitanda changu. Hapo hapo nilimuaga baba yangu, naye akarudi nyumbani baada ya kunitakia heri na fanaka katika masomo yangu.

Nilipofika bwenini nilishangaa sana kuona vitanda vingi katika ukumbi mkubwa ambapo kila kitanda kilikuwa na sehemu mbili za kulala, moja chini na nyingine juu yake. Nilitandika godoro langu kwenye sehemu ya chini ya kitanda. Hata hivyo, nilikuwa na hofu kubwa moyoni kuwa yule atakayelala juu yangu siku moja anaweza kuniangukia. Lakini nilijikaza kiume nikafikiria kwamba hayo yalikuwa mazoea yao na kwamba shule haingekubali kuendeleza hali hiyo kama kungetokea tatizo kama hilo. Baadaye, kengele ililia kuwaita wanafunzi wote kuingia bwaloni kupata chakula cha jioni. Chakula kilikuwa kizuri. Siku hiyo tulikula wali, maharage, mboga na matunda.

Hatimaye, tulimaliza kula tukaambiwa kuingia madarasani kwa masomo ya binafsi. Wanafunzi wote tuliingia darasani, kila mwanafunzi alichukua daftari fulani alilotaka na kuanza kujikumbusha yale tuliyokuwa tumesoma katika ngazi

ya chini ya Sekondari. Mimi nilichukua daftari langu la somo la Kiswahili nikaanza kupitia masomo yote tuliyojifunza katika muhula wa tatu. Shughuli hii iliendelea mpaka saa tatu ambapo kengele ililia tena kuashiria kuenda mabwenini kulala. Humo tulilala kwa utulivu mpaka asubuhi tulipoamka kuanza masomo yetu.

Kwa hakika, siku hiyo ilikuwa siku ya furaha na ugunduzi wa mambo mengi yanayohusu mazingira ya shule yangu ya sekondari katika kidato cha nne. Nilifurahia maonyo niliyopewa na wazazi wangu na jinsi nilivyopokelewa na kuelekezwa na kila mmoja niliyemkuta katika shule yangu.

## MASWALI YA UFAHAMU

1. Eleza shughuli za wazazi kila unapokaribia mwanzo wa masomo ya watoto wao.
2. Mwanafunzi anayezungumziwa katika kifungu hiki alikuwa ameanza kidato gani?
3. Nani ambaye alimsindikiza mwanafunzi hadi shuleni?
4. Ni mawaidha gani aliyompatia baba yake walipokuwa njiani?
5. Eleza sifa za mwanafunzi anayezungumziwa katika kifungu hiki.
6. Walipoingia ndani ya basi mwanafunzi alifurahishwa na nini?
7. Ni nini kinachokuonyesha kwamba mwanafunzi huyu alipokewa vizuri mara tu alipofika shuleni?
8. Kwa nini alishangaa alipofika bwenini?
9. Wanafunzi walipewa chakula gani wakati wa jioni?
10. Walipoingia darasani mwanafunzi huyu alifanya nini?
11. Wanafunzi walitakiwa kulala saa ngapi?

## 16.2. Msamiati Kuhusu Insha ya Masimulizi

### ZOEZI LA 2:

***Tunga sentensi fupi kwa kutumia maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu ulichosoma hapo juu.***

1. kujiandaa
2. kusaliti
3. kuuza
4. bidii
5. tabia
6. maadili
7. heri na fanaka
8. Ukumbi
9. kusajili
10. kuashiria

### ZOEZI LA 3:

***Tumia mshale kwa kuonyesha maana ya maneno yafuatayo:***

| Maneno | Maelezo |
|---|---|
| 1. hofu | a. ukumbi mkubwa unaotumiwa na wanafunzi au askari kulia chakula. |
| 2. mzazi | b. karatasi aliyopewa mtu baada ya kulipa. |
| 3. sauti nyororo | c. hali ya kutokuwa na ushujaa ama ni kuwa na woga. |
| 4. mwenendo | d. madini yanayonata sana na hutumika kwa kujengea barabara. |
| 5. mawaidha | e. nyumba za kulala wanafunzi katika shule au chuo. |
| 6. bwalo | f. mtoto wa kwanza kuzaliwa na mama/ mwanambee. |
| 7. umati | g. mlio laini. |
| 8. bweni | h. watu wengi sana. |
| 9. stakabadhi ya malipo | i. maneno ya maonyo au mafunzo, aghalabu ya kidini, na yenye mwongozo. |
| 10. kifunguamimba | j. mama au baba wa mtu. |
| 11. lami | k. matendo ya mtu yanayojirudiarudia. |

## ZOEZI LA 4:

***Chagua neno moja ambalo lina maana sawa na haya yafuatayo:***

## MIFANO:

***Tendo la kwenda mahali fulani ambapo ni mbali na pale mtu alipo***
***Jibu: safari.***

1. Baba na mama.
2. Mafundisho mazuri.
3. Wakati kutoka alasiri mpaka magharibi.
4. Kiongozi wa shughuli za shirika au taasisi fulani.
5. Neno la kubishia mlango ili kutaka ruhusa ya kuingia mahali.
6. Tamko la kuagana na kumtakia mtu heri na salama.
7. Tandiko nene la kulalia ambalo hutengenezwa kwa sponji, pamba au sufu na aghalabu huwekwa juu ya kitanda.
8. Kupokelewa vizuri pamoja na shangwe kubwa.

### 16.3. Sarufi: Usemi wa Asili na Usemi wa Taarifa.

## ZOEZI LA 5:

***Tazama kwa makini sentensi zinazofuata, kisha utoe maoni yako kuhusu muundo wake.***

1. Wakati huo njiani mama alikuwa ananiambia kwa sauti nyororo akisema: “Nenda ukasome kwa bidii, usisahau unapotoka.”
2. Mama aliendelea kuniambia: “Usiharibu maisha yako kwa sababu unapoelekea kuna vijana wengi wenye tabia tofauti.”
3. Baba alisema: “Unapaswa kufuata maadili unayopewa na mamako.”
4. Aliniuliza: “Wewe ni mtoto wa ngapi katika jamii?”
5. Alisema kwa sauti kubwa: “Kitu gani kisichoeleweka darasani mwenu?”

**Maelezo muhimu**

Muundo wa sentensi hapo juu unaonyesha kwamba kauli ya moja kwa moja kutoka kwa msemaji hadi kwa msikilizaji haikufanyiwa mageuzi yoyote. Sentensi hizi zinaonyesha maneno yanayotamkwa na mtu yakiwa katika hali yake ya kwanza. Kauli hii huitwa **usemi halisi au usemi wa asili.** Katika usemi huu hakuna kugeuza maoni ya mtu wala muundo wake wa kimatamshi.

Katika usemi halisi yafuatayo huzingatiwa:

- Alama za mtajo au alama za kufungulia na za kufungia maneno hutumiwa mwanzoni na mwishoni mwa maneno yaliyosemwa {"  "}.
- Kila baada ya alama ya kufungua, sentensi huanza kwa herufi kubwa. Mfano: "**A**limsomesha mtoto wake."Jirani alisema.
- Alama ya hisi au mshangao, kiulizo, koma na nukta huja kabla ya alama za kufunga na kufungua.

## ZOEZI LA 6:

***Tumia alama zinazofaa katika sentensi hizi zifuatazo.***

1. Alitoka mjini Kigali Kamariza alisema.
2. Umewezaje kuubeba mzigo huu peke yako Mama aliniuliza.
3. Utarudi kesho Mama yake alitaka kujua.
4. Malizeni kazi mliyopewa mwalimu alituamrisha.
5. Mtahitaji vikombe vingapi vya chai Mwenye hoteli alituuliza.

## ZOEZI LA 7:

***Tazama sentensi zinazofuata kisha utoe maoni yako kuhusu muundo wake.***

1. Wakati huo njiani mama alikuwa ananiambia kwa sauti ya upole akisema kwamba niende nikasome kwa bidii nisisahau ninapotoka.
2. Mama aliendelea kuniambia kuwa nisiharibu maisha yangu kwa sababu ninapoelekea kuna vijana wengi wenye tabia tofauti.
3. Baba alisema kuwa ningepaswa kufuata maadili ninayopewa na mamangu.
4. Aliniuliza kuwa mimi nilikuwa mtoto wa ngapi katika jamii.
5. Aliuliza kwa sauti kubwa kitu kisichoeleweka darasani mwetu.

Muundo wa sentensi hapo juu unaonyesha kwamba:

- Alama za kufungulia au kufungia maneno yaliyotamkwa hazitumiwi.
- Alama za kuuliza na za mshangao hazitumiwi.
- Maneno "**kuwa**" au "**kwamba**" hutumiwa.

Hivyo, iwapo mtu anataka kuwaambia wengine maneno ambayo yalizungumzwa na mtu mwingine bila ya kubadilisha, kupunguza au kuongeza maana ya jambo analotaka kulitolea maelezo, maneno hayo anayosema

huitwa **Usemi wa taarifa.**

Kuna mabadiliko ya kisarufi yanayojitokeza tunapogeuza sentensi kutoka usemi wa asili hadi usemi wa taarifa. Mabadiliko hayo ni kama yafuatayo:

| Usemi halisi | Usemi wa taarifa |
|---|---|
| -ngapi? | Idadi/jumla |
| Je,…? | Iwapo/ikiwa |
| …..je? | Jinsi/namna |
| Lini? | Wakati |
| Mbona? | Sababu |
| Kwa nini? | Sababu |
| Vipi? | Jinsi/namna |
| **Wakati** | |
| Mwaka ujao | Mwaka uliofuata |
| Leo jioni | Siku hiyo jioni |
| Wakati huu | Wakati huo |
| Sasa | Wakati huo |
| Kesho | Siku itakayofuata |
| Jana | Siku iliyotangulia |
| Juzi | Siku mbili zilizotangulia |
| Wiki ijayo | Wiki iliyofuata |
| Kesho kutwa | Baada ya siku mbili |
| Mtondoo | Baada ya siku tatu |
| **Nafsi** | |
| Mimi/ ni- | Yeye/ a- |
| Sisi/ tu- | Wao/ wa- |
| **Njeo** | |
| -na- | -li- |

| | |
|---|---|
| -me- | -li- |
| -ta- | -nge- |

**Mabadiliko mengine**

| Usemi halisi | Usemi wa taarifa |
|---|---|
| | **Matumizi ya**:<br>Kuwa<br>Kama<br>Kwamba<br>Ikiwa<br>Iwapo |
| Matumizi ya alama za: « » | Alama za: « » hazitumiwi. |
| Matumizi ya alama ya **?** | Alama ya **?** haitumiwi. |
| Matumizi ya alama ya **!** | Alama ya **!** haitumiwi. |
| **Viwakilishi/Vivumishi** | |
| Hapa | Pale/hapo/alipokuwa |
| Huku | Kule/huko/alikokuwa |
| Huyu | Huyo |
| Watu hawa | Watu hao |
| Kwangu | Kwake |
| Kwetu | Kwao |
| **Vihisishi** | |
| Tafadhali | Alisihi |
| Salaala! | alishangaa |
| Nkt! | alifyonza |
| Uuuuwi! | Piga mayowe |
| Alhamdullilahi | Alishukuru |
| Mungu wangu eeeh | Aliomba |

## ZOEZI LA 8:

***Geuza sentensi zifuatazo katika usemi wa taarifa:***

1. «Nimemruhusu kujenga nyumba nyingine.» Riziki alieleza.
2. «Unanipenda au hunipendi?» Mchumba wake alimuuliza.
3. «Sababu gani hasemi chochote leo kipindi hiki? » Yeye alijiuliza.
4. "Gasore atanitembelea kesho asubuhi." Uwera ananiambia.
5. "Sioni sababu yoyote ya kunisumbua." Mwalimu alisisitiza.
6. 'Hatutakuwa na mvua ya kutosha mwaka huu.'' Wakulima walisema.
7. ''Jua ni gimba kubwa lenye nuru kali lililoko angani ambalo hutoa mwanga na joto.'' Mwalimu alituarifu.
8. 'Tafadhali, msivute bangi kamwe kwani ni hatari kwa afya yenu.'' Mwalimu mkuu aliwasihi wanafunzi.

## ZOEZI LA 9:

***Geuza sentensi hizi ziwe katika usemi halisi:***

1. Baba alituahidi kwamba angetupeleka mjini kutembea tungeshinda mtihani mwaka ambao ungefuata.
2. Katibu alitangaza kuwa kungekuwa na mkutano wa wanachama wote ambao walikuwa wamesajiliwa mwezi huo Jumanne iliyofuata.
3. Mshauri aliwasisitizia watoto kuwa kuna umuhimu kuwatii wazazi wao kwani hili lingeongeza siku zao duniani.
4. Kiranja alitaka kujua sababu ya Afida kuchelewa darasani siku hiyo.
5. Mwenye hoteli alitaka kujua jumla ya vikombe vya chai tulivyohitaji.
6. Mwanafunzi alimwambia kwamba angefaulu katika somo la Kiswahili.
7. Mkuu wa shule alitahadharisha wanafunzi kutoharibu miti.
8. Mwalimu alitaka sote twende uwanjani tukashangilie timu yetu.
9. Kasisi alimshauri Kazimoto kuacha tabia zake za ulevi.
10. Chapakazi alisema kuwa aliyekuwa akimtesa hakuwa adui yake bali alikuwa rafiki yake wa karibu.

## 16.4. Matumizi ya Lugha: Sehemu za Insha

**ZOEZI LA 10:**

***Soma maelezo muhimu yafuatayo, kisha ujibu maswali ya hapo chini:***

- Insha huwa na sehemu kuu tatu ambazo ni **utangulizi**, **kiini** na **kimalizio**.
- Utangulizi ndio sehemu muhimu kwa sababu:
    - Huifahamisha insha na yote yaliyomo,
    - Hufafanua shabaha za insha na jinsi zitakavyofikiwa,
    - Humfanya msomaji avutiwe na yale yatakayojadiliwa katika insha nzima.
- Hapana njia maalumu ya kutanguliza insha. Njia ifaayo ni ile itakayokuwa ya kupendeza sana kwa msomaji. Kifungu cha kwanza kinaweza kuwa ni swali, msemo, methali au maelezo mafupi mradi kitakuwa cha kupendeza. Utangulizi hupaswi kuwa mrefu sana au wa kuchosha. Aya moja fupi inatosha. Iwapo sehemu hii haikuandikwa kwa ufasaha ufaao, inaweza kumfanya msomaji akose hamu ya kuendelea kuisoma insha hata ingawa insha inaweza kuanza kuvutia hapo baadaye.
- Sehemu ya kiini hutoa ufafanuzi na maelezo kuhusu kichwa au hoja. Aghalabu sehemu hii huwa ndefu na yenye aya nyingi za urefu tofauti.
- Katika sehemu ya kimalizio, mwandishi hujaribu kusisitiza hoja zote muhimu ambazo zimejadiliwa na kutoa msimamo wa insha yenyewe kuhusu jambo lililojadiliwa. Mwisho wa insha huonyesha uhusiano uliopo kati ya utangulizi na maelezo yaliyomo katika mwili. Hapa ndipo mwandishi hubainisha mawazo yake, huthibitisha, hushawishi, huhimiza na hufafanua.
- Mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha:

Bila kujali ni aina gani ya insha mtu anaandika, yapo mambo kadhaa ya kuzingatia wakati wa uandishi wa insha. Mambo hayo ni pamoja na:

1. Kubaini ni mada gani ya kuandikia insha na kuielewa vema,
2. Kupanga mawazo katika mtiririko wenye mantiki,
3. Kutumia mtindo unaoendana na kusudi la insha. Kwa mfano, mtindo wa masimulizi unafaa kwa hadithi au insha nyingine za kisanaa,
4. Kutumia lugha fasaha na inayoeleweka.
5. Kufuata kanuni za uandishi. Kwa mfano, matumizi ya alama za

uandishi, aya, herufi kubwa na herufi ndogo.

6. Kupanga insha katika muundo wake, yaani **kichwa**, **utangulizi**, **kiini** na **hitimisho**.

**1. Kichwa cha Habari**

Kichwa cha habari cha insha ni maneno machache, takribani matano, ambayo ndiyo jina la insha. Kichwa cha habari huandikwa juu, katikati kwenye ukurasa wa kwanza wa insha. Mara nyingi, huandikwa kwa herufi kubwa na hubeba wazo kuu la insha.

**2. Utangulizi wa Insha**

Utangulizi wa insha ni sehemu ya mwanzo yenye urefu usiozidi aya moja. Utangulizi hudondoa kwa ufupi kabisa kile kinachoelezwa kwenye insha.

**3. Kiini cha Insha**

Hii ni sehemu tunayoweza kusema ndiyo insha yenyewe. Kwenye kiini ndipo ufafanuzi wote hutolewa. Ufafanuzi huu hupangwa katika aya moja au zaidi. Hapa ndipo mwandishi hubainisha mawazo yake, **huthibitisha**, **hushawishi**, **huhimiza** na **hufafanua**.

**4. Hitimisho la Insha**

Hii ni sehemu ya mwisho ya insha ambayo nayo haizidi aya moja. Katika sehemu hii, mwandishi anaweza kurejea kwa ufupi sana yale aliyozungumzia kwenye insha yake, anaweza kuonyesha msimamo wake, anaweza kutoa mapendekezo, au kuwahimiza walengwa wake kuchukua hatua fulani.

**MASWALI**

1. Kwa sababu gani utangulizi mzuri ni muhimu katika insha?
2. Jadili sehemu kuu za insha.
3. Jadili mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha.

## 16.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**ZOEZI LA 11:**

***Chagua mada moja kati ya hizi, kisha uizungumzie kwa mapana na marefu:***

1. Harusi.
2. Mchezo uliohudhuria.

## 16.6. Utungaji

**ZOEZI LA 12:**

***Andika insha kuhusu mada zifuatazo kwa kufuata uandishi mzuri wa insha:***

1. Watoto Wawe na Uhuru wa Kuchagua Dini Wanayoitaka.
2. Rafiki yako anayesoma katika kidato cha tano amefukuzwa shuleni kwa sababu anatumia dawa za kulevya na kushiriki ulevi. Simulia kilichoendelea.

**TATHMINI YA MADA YA TANO**

***Andika insha inayoanza hivi:***

Mwanamke ni kiumbe mwanadamu wa jinsia ya kike ambaye hushika uja uzito na kuweza kuzaa. Mwanamke ana nafasi muhimu katika kuendeleza nchi yetu kutokana na kuwa mwanamke ndiye shule ya kwanza ya mtoto. Fikra za mwanamke ni muhimu sana, nguvu zake ni lazima na uwezo wake unahitajika katika kuendeleza nchi yetu.

Mwanamke ana nafasi kubwa katika kuendeleza nchi yetu kutokana…………

**(katika insha yako zingatia: matumizi ya usemi wa asili na usemi wa taarifa, msamiati unaofaa, hoja nzuri, mtiririko wa hadithi na kukamilika kwa kila aya).**

Kichwa cha habari kiwe "NAFASI YA WANAWAKE KATIKA KUENDELEZA UCHUMI WA NCHI YETU."

## MAREJEO


ABDILAHI, N. (1974).Tamrini za Kiswahili: Kitabu cha pili, Nairobi, Oxford University Press. Co-Publishing Committee (1987). Hadithi za kwetu, Nairobi, Co-Publishing Committee.

Kitula, K. (2014). Taaluma ya Uandishi. The Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi, Kenya.

Mdee, J. S. ,K. Njogu, A. Shafi (2011). Kamusi ya Karne ya 21. Longhorn Publishers (K) Ltd. Nairobi, Kenya.

MINEPRISEC (1982).Ikinyarwanda: Gusoma no Gusesengura Imyandiko, Kigali.

Mlaga. W. K. (2017). Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21. Heko Publishers Ltd. Dar es salaam.

MUJAKI, A.& KIZZA, G.G.(2000). MK Kiswahili kwa shule za msingi: Kitabu cha Kwanza-Darasa la Nne, Kiongozi cha Mwalimu, MK Publishers (U) Ltd, Kampala.

NDAYAMBAJE, L. & NIYIRORA, E. (2012), Kiswahili Sanifu kwa Shule za Sekondari kidato cha Nne. Tan Prints (India) Pvt.Ltd.

NGUGI WA THIONGO. (2003). Siri na Hadithi Nyingine. East African Publishers Ltd. Nairobi

NICKY STANTON (1996). Mastering Communication, Hampshire, Macmillan MasterSeries.

NIYOMUGABO, C. (2013). Mafunzo ya Kiswahili: Mwongozo wa Mwalimu, Kidato cha 5, Kigali, Fountain Publishers Rwanda Ltd.

NKWERA, V. M. F. (1978). Sarufi na Fasihi, Sekondari na Vyuo. Tanzania Publishing House Dar-es-Salaam.

Ntawiyanga S., na Kinya J.M. (2015). Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Kidato cha 2, Longhorn Kenya Ltd; Nairobi

Ntawiyanga, S. na Wenzake (2018). Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Kidato cha 3, Longhorn Kenya Ltd; Nairobi.

Rwanda Education Board (2015). Muhtasari wa somo la Kiswahili kidato cha 4-6 Michepuo mingine. Kigali-Rwanda.

Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari (1987).Kitabu cha Kiswahili III A, Kigali, Taasisi ya Elimu ya Sekondari.

Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari (1987).Kitabu cha Kiswahili III B, Kigali, Taasisi ya Elimu ya Sekondari.

Taasisi ya Mafunzo ya Sekondari, Kitabu cha Kiswahili IV-VA, Kigali, Taasisi ya Elimu ya Sekondari, Novemba 1987 \

TUKI (2006). English-Swahili Dictionary (3rd Edition). Dar-es-Salaam, Tanzania.

Wamitila, K.W. (2007). Mwenge wa Uandishi. Mbinu za Insha na Utunzi. Vide Muwa Publishers Limited. Nairobi, Kenya.